# KCSE 2024 KEY AREAS KISWAHILI

**{500+ KISWAHILI PREDICTION QUESTIONS}**

***{COMMONLY KCSE TESTED QUESTIONS}***

*A Series of KCSE 2024 Prediction Questions Prepared by a Pannel of Top KNEC Examiners HQ Nairobi*

**All KCSE 2024 Candidates are advised to take the questions Serious!**

**Confidential!!!**

**For Marking Schemes**

**Contact 0724333200/0795491185/0768321553**

**Or Order online at www.kenyaeducators.co.ke**

**KENYA EDUCATORS CONSULTANCY**

# SEHEMU YA 1 (102/1 KISWAHILI KARATASI YA 1)
# MASWALI YA INSHA

1. Andika insha itakayotamatika na ....kweli dunia ni mwendo wa ngisi, ina masalata wengi.
2. Elimu bila malipo nchini Kenya ina changamoto zake. Jadili
3. Eleza namna katiba mpya inavyofaa kutetea nafasi na hadhi ya jinsia ya kike.
4. Ajira ya watoto ina madhara mengi. Fafanua.
5. Zigo la kuliwa halilemei.
6. Andika insha itakayomalizikia kwa :
   ….mkuu wa askari aliwaeleza kuwa ikiwa njia hizo zingetumika, uhalifu ungezikwa kwenye kaburi la sahau
7. Mwenye kovu sidhani kapoa.
8. Elimu ya bure inayotolewa na serikali katika shule za msingi za umma humu nchini, imekuwa na athari mbalimbali. Jadili.
9. Andika insha itakayomalizikia maneno yafuatayo:-
   ....aliyakumbuka mashauri ya mamake ambayo aliyakaidi. Machozi yalimbubujika alipojiona kadhoofika kiafya jinsi ile; mguu mmoja duniani, mwingine kaburini.
10. Uhaba wa kazi ni tatizo sugu katika nchi zinazoendelea. Jadili.
11. Andika kisa kinachodhihirisha ukweli wa methali: "**subira huvuta heri**"
12. Andika insha itakayoishia kwa maneno haya:- ...........nilipiga magoti chini na kumshukuru Maulana kwa kuyanusuru maisha yangu.
13. Kumekuwa na kilio kila uchao. Pendekeza njia mbalimbali za kutokomezea mbali umaskini katika jamii yako. Fahali wawili wapiganapo, nyasi huumia.
14. Andika insha itakayoishia kwa maneno yafuatayo:-
15. ....hapo ndipo nilipoapa kwamba sitawahi kumfungulia mtu yeyote yule mlango usiku.
16. Asifuye mvua imemnyea.Thibitisha ukweli wa methali hii kwa kisa.
17. Utovu wa nidhamu shuleni umesababishwa na mabadiliko katika sekta ya Elimu. Jadili.
18. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno ...ama kweli dunia ni mti mkavu; ukiuegemea utaanguka. Nilikuja kutambua kwamba ni heri uwe maskini wa mali na tajiri wa fadhili kuliko tajiri wa mali na fukara wa utu.
19. Licha ya kufaulu kiasi, utoaji wa elimu ya bure katika shule za msingi na upili umekumbana na matatizo si haba. Jadili
20. Mchuma janga, hula na wa kwao.
21. Andika insha itakayoishia kwa maneno haya………… moyo ulinidunda nilipoona gari letu likibingiria kuelekea ufuo wa bahari, machozi yakanitoka kwa wingi nikakumbuka yote niliyokuwa nimetenda ulimwenguni, nikayafunga macho yangu.
22. Udongo uwahi/upatilize ungali maji.
23. Kuavya mimba ni uovu usioweza kuvumiliwa , jadili.
24. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya:

.................ndipo nilipogundua kuwa mtu ambaye siku yake imefika hana budi kufa hata akafanyiwa dawa za aina gani.

25. Wewe kama Mwalimu ambaye amehitimu katika chuo kikuu cha Kenyatta, kuna nafasi ya kufundisha katika shule ya upili ya Angeko. Andika wasifu-kazi utakaoandamana na barua yako.
26. Mgema akisifiwa tembo hulitia maji.
27. Vizingiti \Vikwazo vya kuundwa na kupatikana kwa katiba mpya nchini Kenya sio wanasiasa pekee.Fafanua.
28. Andika insha itakayomalizikia kwa: **. . .** Na katika uchaguzi wa marudio uliofanywa baada ya kisa hicho, Hidaya akapata ushindi mkubwa na kuwa mbunge wa eneo bunge la Kubali.
29. Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo
30 Uavyaji wa mimba ni suala sugu hapa nchini Kenya. Jadili
31. Ilikuwa mara ya kwanza kufikishwa mahakamani…………….. endeleza
31. Kisa cha mwanafunzi kilingane na chanzo hiki na aonyeshe ubunifu na matumizi mazuri ya lugha
32. Eleza jinsi haki za watoto zinavyokiukwa katika jamii huku ukipendekeza suluhu.
33. Cha Mchama huchama, cha Mgura hugura.
34. Rais Julius Kabarage Nyerere ni mtu anayejulikana katika taifa la Afrika kusini na Mataifa mengine. Alipozaliwa...........................................................................
35. Shughuli ya kuavya mimba iharamishwe. Jadili
36. Ganga ganga ya mganga humlaza mgonjwa na matumaini.
37. Andika insha itakayomalizikia kwa: Baadaye niligundua kuwa kutotii wazazi kunaweza kuwa na madhara ya muda mrefu sana.

38. Bandu bandu huisha gogo.
39. Suluhu kwa matatizo yanayoikabili nchi yetu ni katiba mpya. Jadili,
40. Kamilisha mtungo wako kwa kifungu kifuatacho.
……………………………………………. Ni uso wa nani usiotahayuri kwa kisa kama hiki?
41 Mchumia juani hulia kivulini.
42. Uhalifu umekithiri sana humu nchini. Jadili sababu zinazochangia hali hii na upendekeze njia za kukabiliana nao.
43. Andika insha itakayomalizikia maneno haya----------------------niliketi nikishika tama. Iliyokuwa nyumba yangu ikawa jivu tu! Sikuyazuia machozi yalionibubujika.
44. Andika Mtungo unaothibitisha ukweli wa methali: Jitihada haiondoi kudura.
45. Simu za rununu zina madhara mengi kuliko manufaa . Jadili.
46. Andika insha itakayoisha kwa maneno yafuatayo: ..............nilipogutuka niliangaza macho huku na kule. Aah! kumbe nilikuwa nikiota!

47. Fafanua njia mbalimbali za kukabiliana na umaskini nchini mwetu.
48. Samaki mkunje angali mbichi.
49. Hauchi hauchi unakucha. Naam, siku njema niliyosubiri kwa hamu na ghamu iliwadia. Nilifurahi ghaya ya kufurahi……. (endeleza insha hii).

# SEHEMU B (102/2 KISWAHILI KARATASI YA 2)
# {Ufahamu, Ufupisho, Lugha & Isimu Jamii}
**Karatasi ya pili 102/2**

## UFAHAMU

**1.** ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Panografia ni tendo, maandishi, picha au michoro inaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, magazeti, vitabu, muziki, televisheni, tovuti na kanda za kunasia picha na sauti.

Ponografia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea kote ulimwenguni mithili ya moto mbugani wakati wa kiangazi. Kuenea kwake kumechangiwa na mambo kadha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi ukiwa umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. Hata hivyo, kazi hii hubuniwa au kutengenezwa na makundi mbalimbali ya watu. Miongoni mwa hawa ni watu wasiojali maadili. Pili, kuna wale wenye matatizo ya kisaikolojia na kijamii. Wao hutengeneza na kueneza uchafu huu kwa lengo la kuvuruga madili katika jamii au kuchukiza wanajamii waadilifu.Kundi lingine ni lile la wanaoichukulia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Kwa mfano, baadhi ya wanamuziki hutumia **<u>ponografia</u>** kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji wa ponografia kuna athari kubwa kwa jamii hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri, upo ushaihidi kuonyesha kuwa wale wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kwamba kinachoonekana kwa jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kisasi ikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama vile masomo, watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera, huyaiga wanayoyaona na kuyasikia. Hii ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Hivyo basi wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokeo yake ni ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa huku wengine wakiambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo yanaweza kuwaletea mauti.

Yasemekana kuwa akili za binadamu hunasa zaidi mambo yanayowalishwa kwa picha na hivyo basi matusi haya yaweza kudumishwa katika kumbukumbu zao. Tabia mbaya kama vie ushoga, ubasha na usagaji huwa matokeo yake na hata matokeo ya vijana hugeuka wanapoanza kuiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika, lugha, ishara na miondoko inayohusiana nanmgono huibuka. Yote haya yanakinzana na desturi za mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kuchapo. Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama vile unywaji pombe na matumizi ya vileo ambavyo huchochea uchu wa ngono na kuibua tabia za kinyama.

Kuendelea kuzitazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, huondoa makali kiasi kwamba hata katika uzima mtu hupoteza mhemko na kugeuswa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mjini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na malezi haya yasiyo na kizuizi.

Kuuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi, watu wazima kuwajibika kwa kuwalinda na kuwahimiza vijana kuhusu maovu haya na wale wenye midahilishi, video na sinema kutowaruhusu vijana kutazama uchafu huu kunaweza kuwa maana ya kuyakinga au hata kuyaepuka madhara ya ponografia. Ni sharti pia sheria izuie na kupiga marufuku utengenezaji na uenezaji wa upungufu huu. Bila shaka, sheria na hatua kali za ziweze kuchukulia dhidi ya waivunjao. Hali kadhalika, wazazi wasijipweteke tu bali wawaelekeze watoto wao ipasavyo na ila mtu alitekeleze jukumu lake.

**Maswali**

(a) Yape makala uliyosoma anwani mwafaka
(b) Toa sababu za kusambaa kwa uchafu unazozungumziwa katika taarifa
(c) '**Bendera hufuata upepo**'. Thibitisha ukweli wa usemi huu kulingana na makala
(d) Ni kwa nini ni muhimu kuwakanya vijana dhidi ya uchafu huu?
(e) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa dhidi ya aina ya uozo unaozungumziwa na mwandishi?
(f) Fafanua msamiati huu kimuktadha
(i) **uchu** …………………………………………………………………
(ii) **wasijipweteke** ………………………………………………………………….
(iii) **nishai** …………………………………………………………………

**2.** ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Ilikuwa Jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa Taarifa ya Habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe pesa za kiinua mgongo. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi laki mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki. Watu wengi walinishawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, Waziri wa Kilimo alitangaza bei mpya. Shilingi 1,500 kwa kila gunia. Nami nilikuwa naanza kuumakinikia mradi huu.

Baaada ya taarifa, nilikoga, nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichukua mara moja.. Usingizini niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kilimo nilitenga ekari kumu za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikakati ya mwezi wa Machi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa manyakanga wa kilimo, nilipa shilingi elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejeo. Kwanza, nililipa shilingi 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunua magunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilingi 3,300 kila gunia. Mwezi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda. Ili nipate mazao bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilingi 1,000 kila ekari. Mvua ilinyesha vizuri na baada ya siku saba mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mbegu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua wa kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilia kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yananifikia magotini. Hii ikawa ishara kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo 'amonia.' Gharama yake ikawa shilingi1,300 kila gunia. Hivyo, nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano..

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa mashina. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapita njia waliajabia mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siwanawaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanis wangu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno nitakayopata kukadiria faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa 'Usikate majani, mnyama hajauawa.'

Bila taarifa wala tahadhari mvua ikatoweka. Hayakupita majuma mawili mahindi yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahindi, shamba likageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makasio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi ufanyavyo moshi. Lakini 'Muumba ndiye Muumbua.' Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha. Muda is muda mahindi yalianza kunawiri. Kumbe tukio lililonivunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwaa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafhuku majani ya mahindi yamechanika kama nyuzi. Niliugua. Baada ya wiki moja, nilipata nafuu. Nilipotazama upande wa shamba nikaona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli.

Muda si mrefu mahindi yalirudi hali yake tena, kisha yakakomaa. Harakati za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli hii ikawa shilingi 5,000. Kuvuna, kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500.

Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. Habari motomoto siku hiyo ilikuwa: 'MAHINDI GUNIA 900/=.' Niligutuka usingizini.

**Maswali:**

a) Andika kichwa mwafaka kwa kifungu hiki cha habari.

b) Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika?

c) Taja matatizo **matatu** yaliyotisha mradi wa msimulizi wa kukuza mahindi.

d) **Eleza maana ya methali zifuatazo:**

(i) Usikate majani, mnyama hajauawa.

e) Eleza mambo **mawili** yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia.

f) Kwa nini msimulizi alisema maumbile ni kitu cha ajabu?

g) **Eleza maana ya:**

(i) kiinua mgongo.

(ii) manyakanga wa kilimo.

3. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Mtoto anapozaliwa huwa ni malaika wa Mungu. Hutaraji kuongozwa kwa kila njia ili awe mwana mwelekea. Jukumu la kulea mtoto huanzia nyumbani. Wako baadhi ya watu ambao wanaamini kuwa

jukumu hili muhimu hutekeleezwa bora na mama; wengine husema kuwa ni jukumu la baba. Ni kweli kwamba mtoto huwa na mama yake kwa muda mrefu zaidi ya baba lakini kivuli cha baba hakikosi kumwandama na **kumwathiri** maisha yake.

Uongozi wa mama huanzia siku ya mwanawe kuingia ulimwenguni. Kwa hivyo, mama zaidi ya baba huwa ndiye **chanzo cha chemichemi** ya maisha ya mwanawe. Mtoto kwa kawaida ana tabia ya kuiga kila jambo analoliona na kusikia na mambo ya awali ajifunzayo hutokana na mamaye.

Je; mtoto huiga kutokana na mama pekee? Kila utamaduni hasa huku kwetu Afrika, una taratibu zake zilizopangwa kuhusu malezi ya watoto. Kwa mfano; akina baba wengine wanaoishi maisha ya kijadi huonelea kwamba ni jukumu lao kuwalea watoto wa kiume. Kwa hivyo mvulana anayekulia katika mazingira haya **akishachuchuka** kiasi cha kujua lipi zuri lipi baya huanzia kuwa mtoto wa baba zaidi ya kuwa wa mama. Baba humuathiri mtoto wake kwa kumshauri kuhusu maneno ya kiada ya wanaume. Hupenda kukaa naye katika uga wake kwa kumshauri kuhusu maneno ya kiada ya wanaume huku akimkataza kukaa jikoni na kumsisitizia kuwa wanawake ni tofauti naye. Aidha, humfunza sifa kama vile ushujaa na uvumilivu kwa namna ambayo huona kuwa ni ya kiume. Pindi mtoto anapoonyesha tabia za kikekike, baba hujiandaa kuzitadaruki kwa kumkaripia. Baba hutaka kujiona mwenyewe katika hulka ya mwanawe.

Baba kama huyu humpa nafasi ndogo sana mkewe ya kumwongoza mtoto wake wa kiume kwa jambo lolote hata kama wakati mwingine ni la heri. Kwa upande mwngine baba huyu huwa na machache ya kuzungumza na bintiye kwa kuwa huona kuwa si stahili yake kufanya hivyo. Mtoto wa kike huachiwa mamake. Lakini kutokeapo jambo la kulipima mama huona linampita kimo, humwita baba kuingilia kati na aghalabu baba naye humwagiza dadake aje atoe suluhisho mwafaka.

Ulezi kama huu una nafasi yake katika jamii, lakini ni lazima tukiri kuwa pia unaendeleza maisha ya fawaishi na kuanzisha **taasubi** ambayo hatima yake ni mwanamke kukandamizwa na mwanaume. Wazazi walio na mwelekeo huu katika malezi yao hufikiri kuwa wataishi na watoto wao katika mazingira finyu na kwa hivyo waendelee kuwapulizia pumzi za kuhilikisha. Lakini ni sharti wakumbuke kuwa wao sio walezi peke yao na wala mtoto hawezi kuishi peke yake na kuwa na tabia ya kipekee. Leo ataishi kwao lakini kesho itambidi atoke aone ulimwengu. Kila atakapotia mguu ataona mambo mapya yatakayompa tajriba mpya na mawazo mapya ambayo aghalabu yataendelea kuiathiri **hulka** yake. Iwapo tabia alizozipata kwa wazazi wake hapo awali zilikuwa na misingi isiyokuwa madhubuti na mielekeo finyu, zinaweza kuwa pingamizi katika maingiliano yake na watu wengine. Mambo haya yanatuelekeza katika kufikiri kwamba maisha ya siku hizi hayaruhusu ugawaji wa kazi ya malezi ya namna ya baba na mama wa kijadi. Baba na mama ni walezi wa kwanza ambao kwa pamoja wanapaswa kuwaelekeza watoto wao katika maisha ya ulimwengu uliojaa bughudha na ghururi. Ni lazima wazazi watambue tangu awali kuwa katika malezi hakuna cha ubaguzi. Hakuna, mambo ajifunzayo mtoto wa kiume ambayo hayamhusu mtoto wa kike. Uvumilivu, bidii, utiifu na kadhalika ni sifa zinazomwajibikia kila mtoto kama vile upishi, ukulima na usafi. Mwanamke tangu azali ameumbwa kuwa mama na haipasi kulazimishwa kuchagua baina ya mtoto wa kike na kiume. Mapenzi na wajibu wa wazazi yapaswa yasiwe na mipaka bali yawe maridhawa kwa watoto wote.

**Maswali**

(a) Toa kichwa mwafaka cha makala haya

(b) Kulingana na kifungu hiki, taja mambo **mawili** ambayo yanaweza kuwa hatari kwa malezi ya watoto

(c) Kwa nini baba humpa nafasi ndogo sana mkewe ya kumwongoza mtoto wa kiume katika jambo lolote hata kama wakati mwingine ni la heri

(d) Eleza mambo **mawili** ambayo ni ya manufaa katika ulezi jadi

(e) Kulingana na makala haya, ushahidi gani unaonyesha kwamba kuna kutegemeana katika ulezi jadi?

(f) Taja sifa **mbili** ambazo baba humfundisha mwana wa kiume

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kaktika kifungu hiki:

(i) **Chanzo cha chemichemi**...

(ii) **Akishachuchuka**...

(iii) **Hulka**.

4. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Habari kuwa watoto chini ya miaka mitatu 'huwindwa' kitandani na kuraushwa na wazazi wao waende shuleni mwendo wa saa kumi na moja asubuhi ni za kusikitisha.

Kwa mujibu wa ripoti za wataalamu wa elimu ya watoto wachanga (ECD), watoto hao hutakikana kuwa darasani kabla ya saa kumi na mbili asubuhi.

Wanapowasili wao huanza kufukuza ratiba ya masomo ambayo huwapatia muda mfupi mno wa kula, kucheza, kupumzika na hata kuchunguza afya na usalama wao.

Badala ya kuondoka mapema kuelekea nyumbani, wengi wao hufika saa za usiku pamoja na wazazi wao wakitoka kazini. Wanapowasili nyumbani wanapaswa kuoga na kupata chakula cha jioni kwa pupa ili wafanye mazoezi waliyopewa na walimu wao.

Mazoezi hayo huwa ya masomo yote matano huku kila somo likiwa na zaidi ya maswali thelathini. Badala ya kupumzika mwishoni mwa juma, watoto hao huhitjika kuhudhuria shule siku nzima ya Jumamosi. Jumapili wanatakiwa Kanisani na hali hii hujirudia mpaka muhula umalizike. Ikiwa ulidhani watapewa nafasi ya kupumzika wakati wa likizo , umekosea kwa sababu watoto hao huhitajika kuhudhuria shule. Hili limekuwa likiendelea hata baada ya Wizara ya Elimu kupiga marufuku kusomesha wakati wa likizo.

Wazazi-hasa wale wanaofanya kazi mijini- wamekuwa wakiunga mkono mtindo huu kwa sababu unawaondolea mzigo wa malezi na gharama ya kuwaajiri walezi.

Wataalamu wanasema matokeo ya hali hii ni watoto **wakembe** wenye afya na **maadili** mabaya kutokana na kuchanganyishwa akili na walimu wanaowataka wajue kila kitu wakiwa na umri mdogo.

**Kuwashinikiza** watoto wakembe wahudhurie shule na zaidi ya hayo wajue kila kitu kuna madhara mengi. Kwanza kabisa, kuraushwa kwa watoto macheo waende shule kunawanyima fursa ya kulala na kupumzika. Utafiti unaonyesha kuwa watoto wanahitaji kulala na kupumzika kwa zaidi ya saa 12 kwa siku. Hii ina maana kuwa mbali na muda mfupi wanaolala na kupumzika mchana kutwa, watoto wanapaswa kutumia usiku mzima kwa usingizi.

Hii huwasaidia kukua wakiwa na afya nzuri hasa kiakili. Matokeo ya kuwarausha watoto hao waende shule saa hizo huwafanya wakose furaha mbali na kuwafanya wachanganyikiwe kiakili.

Pili, kuwalazimisha watoto wakae darasani kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni huwa kunawanyima fursa ya kucheza na kutangamana. Wataalamu wa afya ya watoto

wanapendekeza kuwa watoto wachanga wanapaswa kucheza ili viungo vya miili yao kama moyo, akili, mapafu na kadhalika vifanye kazi vizuri.

Kinyume na watu wazima ambao hufanya kazi nzito nzito na kuwawezesha kufanya mazoezi, watoto huwa hawafanyi kazi hizo. Wazazi na walimu wanapaswa kufahamu kuwa kazi ya watoto ni mchezo na wana kila haki ya kupewa furaha ya kucheza wakiwa shuleni na hata nyumbani.

Tatu, wazazi wengi ambao hufurahia kuwaachia walimu jukumu la kuwalea watoto wao huku wao wakiwa kazini huwa wanasahau kuwa sio kila mwalimu ana maadili yanayopaswa kuigwa na mwanawe. Ingawa tunawatarajia walimu wawe mifano bora ambayo inaweza kuigwa na kila mtu, ukweli ni kwamba baadhi ya walimu hawajui maana wala hawana maadili. Hatari ni kwamba watoto **wakembe** husoma kwa kuiga wakubwa wao na ikiwa walimu wanaoshinda nao shule wamepotoka kimaadili, kuna uwezekano mkubwa wa watoto hao kupotoka pia. Hii ndiyo sababu wazazi wengi wamekuwa wakilalamika kuwa wanawao tabia mbaya ambazo hawaelewi zilipotoka.

Kila mzazi anayejali maisha ya mwanawe anapaswa kutekeleza jukumu lake la kumlea na kumwelekeza jinsi anavyotaka akue. Ni kinaya kuwa wanawatarajia wanawao wawe na tabia na maadili kama yao ilhali hawachukui muda wa kukaa nao na kuwaelekeza.

Nne, kuwawinda, kuwaamsha, kuwaosha na kuwalazimisha watoto waende shule kila siku hata ingawa hawataki huwa kunawafanya wawe wategemezi wasioweza kujipangia na kutekeleza mambo kivyao.

***(TAIFA LEO, IJUMAA, FEBRUARI 5, 2010)***

**MASWALI.**

(a) Ipe taarifa anwani mwafaka
(b) Mwandishi anatoa maoni gani kuhusu ratiba ya masomo?
(c) Eleza athari za mfumo wa elimu unaoangaziwa hapa
(d) Ni ushauri upi unaotolewa kwa wazazi ?
(e)Taja mbinu zozote **mbili** za lugha alizotumia mwandishi
(f) Eleza **maana** ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa.
(i) **'huwindwa' kitandani**
(ii) **Maadili**
(iii) **Kuwashinikiza**…
(iv) **Wakembe**…

5. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma.

Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho n.k. kwa raia, kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya. Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini.

Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharibu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia

maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyi kazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma kupeleka vituo vyao vyaafya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umaa wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, whandisi, mawakili, walimu na mahesibu ambao hukwepa **majukumu** yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi.. Wengine wasio wataalam huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwinginehulazimika kusalimu amri na kutoa hongo hili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale **wasiojimudu** kifedha hubaki **wakilia ngoa**. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza hudumia jamii.

Ufisadi **umekita mizizi** na **kushamiri** katika sekta za umma za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyikazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyikazi wasiohitimu na wasiohitimu na wasiowajibika kazini.

Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufisadi. Kwa hivyo, wafanyikazi wenye biddi hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishaia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimeteuliwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya Kuchunguzavisa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza **Kashfa** ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni ya shilingi) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia siziso halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo.

Serikali pia imeunda kamati ya kupikea malalamiko kutoka kwa wananchi **waliohasiriwa** na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa wakalipa, au wakilipwa kuwatetea mahakamani wanakwepa jukumu hilo ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

**Maswali**

1. Eleza aina **nne** za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma
2. Kulingana na kifungu ulichosoma, ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani?
3. Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi?
4. Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini?
5. Toa msamiati mwingine wenye maana sawa na rushwa
6. Eleza mana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kifunguni;
   (a) Majukumu
   (b) Kashfa
   (c) Shamiri
   (d) wakilia ngoa
   (e) Waliohasiriwa
   (f) Kita mizizi

6. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

Aibu kubwa ya taifa kushindwa kukabiliana na tatizo sugu la ajali za barabarani bado inaendelea. Wahusika katika sekta ya uchukuzi na mawasiliano licha ya matumizi ya vidhibiti mwendo na kanda za usalama. Ajali za barabarani zinaangamiza idadi kubwa ya watu kila mwaka, wakiwemo viongozi na watu mashuhuri.

Miongoni mwa sababu ambazo zinaleta maafa barabarani ni pamoja na uendeshaji kasi kupita inavyotakikana, yaani kukiuka masharti yaliyowekwa na wizara ya uchukuzi na mawasiliano. Madereva wengi hung'oa vithibiti mwendo vilivyowekwa hawarekebishi mikanda ya usalama, wala hawa peleki magari yao kwa ukaguzi mara kwa mara kama inavyopaswa kutekeleza kanuni zilizowekwa kwa hivyo hutegemea hongo kuwa barabarani. Fauka ya hao, madereva wa malori na matrela mara nyingi huendesha magari hayo wakiwa walevi. Dawa za kulevya kama vile miraa na bangi, hutumiwa sana na watu hawa, na matokeo yake huwa ajali mbaya.

Hata hivyo, lawama haiwezi kuelekezewa madereva pekee. Ukiangazia barabara nchini utapata kuwa barabara nchini Kenya haziko katika hali nzuri . Zile za lami zimekuwa na mashimo makubwa ambapo mvua ikinyesha hufanya vidimbi mithili ya machimbo ya madini yaliyojaa maji baada ya kuachwa wazi. Na zile barabara zisizokuwa za lami zimeharibika kiasi kwamba ni vigumu kuzitofautisha na njia za ng'ombe kwenye maeneo kame.Kinachohitajika ni serikali kuzifanyia ukarabati ili kuzirudisha katika kiwango ambacho zitaweza kufaa tena.

Wananchi pia inafaa waelimishwe ili wasikubali kuingia kwenye magari ambayo tayari yamejaaa kupita kiasi. Hili litawasaidia wananchi wenyewe kudumisha usalama wao barabarani. Pia inafaa watambue ya kwamba wana jukumu la kuwaarifu walinda usalama endapo dereva anaendesha kwa kasi sana kuliko ile ya kilomita 80 kwa saa iliyokubaliwa.

Inafahamika kuwa maafisa wa uslama ndio wafisadi zaidi, hivyo basi huchangia katika kuongeza idadi ya vifo barabarani. Katika vita dhidi ya ufisadi na ajali za barabarni, ni mwananchi mwenyewe ambaye alawezesha kukomesha hali hii. Kwa mfano, afisa wa usalama akipatikana akichukua hongo, yeye pamoja na yule aliyetoa hongo wapelekwe kwenye vituo vya kukabiliana na ufisadi na wachukuliwe hatua kali, matatizo haya yataisha.

Lakini kabla kufika hapo, ni muhimu kumhamasisha mwananchi kuhusu haki zake na namna ya kukabiliana na suala hili la ufisadi. Hali hii inatuonyesha kwamba mipango maalum inapaswa kufanywa na serikali ili kuwaelimisha wananchi kama hatua ya kwanza ya kukabiliana na ufisadi hatimaye izilainishe sekta zote wala si ya uchukuzi na mawasiliano pekee.

**Maswali**

1. (a) Mbali na ajali za barabarani, taja, tatizo lingine sugu ambalo linakumba nchi ya Kenya

(b) Ajali za barabarani zinasababishwa na nini?

(c) Mwandishi anapendekeza hatua zipi zichukuliwe na serikali ili suluhisho la kudumu lipatikane?

(d) Taja hatua ambazo serikali imechukua ili kuimarisha uchukuzi

(e) Ni kitu gani ambacho kinaonyesha kuwa serikali imeshindwa kukabiliana na ajali barabarani?

(f) Eleza maana ya maneno haya:-

(i) Tatizo sugu.

(ii) Vithibiti mwendo.

(iii) Machimbo.
(iv) Ukarabati.
(v) Hongo.
(vi) Kuhamasisha..

7. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

Nchini Kenya, pamoja na kuwa mwanamke amepewa hadhi kubwa ikilinganishwa na hapo awali, kumetokea visa vingi vya unyanyasajiwa wanawake. Visa hivi haviwakati wengi maini, bali ni vyombo vya kuwazindua viongozi kuona kwamba hali haijafika kiwango cha kuridhisha. Visa vya ubakaji wa watoto wa kike na wazee, na wakati mwingine baba zao, vimetokea katika miaka ya hivi karibuni. Isitoshe, akina mama wengi wamekuwa wahasiriwa wa mivua ya makonde kutoka kwa waume zao, hata kwa makosa madogo madogo. Hivi majuzi mmoja wa wanawake hawa, ambao maisha kwao ni shairi tu, alichomwa vibaya na mumewe, kisa na maanaamejitia kujua kuwa kuna siku ya wapenzi, yaani Valentine day. Mwanamke huyu, baada ya kutoa mashambani kuja kujumuika na mumewe kusherehekea siku ya wapenzi, alipata sherehe za kuchoma moto huku mumewe akilalamika kuingiliwa uhuruwake. Mama huyu bado anauguza majeraha ya mwili na moyo!

Mwanamke aliyesoma na kupewa fursa ya kufanya kazi na ajira ofisini naye amekabiliwa na changamoto nyingi. Huyu lazima atekeleze majukumu yake kama mama, mke na mfayikazi. Wengi wa wanawake wanaofanya kazi mjini hulalamika wanafanya kazi maradufu ya wanaume. Mwanamke kama huyu, kama alivyolalamika mmoja wao ambaye ni afisa wa utawala wa mikoa, huanza siku yake alfajiri na mapema kuitayarishia familia staftahi, kisha kuelekea ofisisni ambapo anakabiliwa na migogoro mingi ya kusuluhisha. Arejeapo nyumbani jioni, hali huwa hiyo hiyo, kutayarisha chajio, kushughulikia kazi za shule za watoto na kuichangamsha familia. Maisha yake huwa hivyo, siku nenda siku rudi. Utashangaa mja huyu atayabeba mangapi?

Hali huwa mbaya zaidi kwa wanawake ambao wameingia siasa. Hawa mikasa yao haihesabiki. Mara watupiwe mabezo ya kila aina na wanasiasa wenzao, mara washutumiwe na kutiwa midomoni na wanajamii kwa kuonekana wakichapa kazi na kuwa na uhusiano wa karibu na wazalendo wenzao wa kiume. Maisha yake hupigwa darubini hata nyakati ambazo hayahitaji kuangazwa.

Mwanamke amekuwa kinyago cha kufanyiwa mzaha. Juzi karibu mbingu zianguke alipojitokeza mwana vitimbi mmoja aliyejitia kufanyia utani yasiyohitaji. Alimwasiri mwanamke kama aliyechangia kukosewa heshima kwake kwa kule kutamani kufanywa hivyo. Ingawa wanawake walimshinikiza mhusika huyu kuomba msamaha, upayukaji wake haupaswi kuchukuliwa kama mzaha. Ni ishara ya hisia ya ndani za watu wengi kuhusu mwanamke; kwamba ingawa wakenya wamejitahidi kupigania haki za wanawake; baadhi yetu bado wana zile fikira za kijadi kuhusu wanawake.

Uchumi wa nchi kamwe hauwezi kuendelea bila kumhusisha kila mtu. Nchini humu, baada ya kutambua haya, mwanamke amepewa nyadhifa mbalimbali katika serikali. Ingawa kuna baadhi ya wanawake waliohusika na kashfa mbalimbali za kifisadi, Kuna wale ambao wametumia nyadhifa zao kuhifadhi nchi. Mmoja wa wanawake amejaribu kwa jino na ukucha kuyalinda mazingira dhidi ya mapapa. Nani asiyekumbuka matusi na mabezo aliyopata mwanamke huyu anayejitoa mhanga kuikinga sehemu Fulani ya burudani dhidi ya kunyakuliwa na wanaostahili? Hakuyajutia yaliyompata. Aliowatisha walijaribu kummeza mzimamzima lakini mwishowe walisalimu amri na kuliacha eneo hilo. Hiki kilikuwa kitendo cha ujasiri na uzalendo mkubwa. Matunda yake yamewafaidi wengi, vijana kwa wazee. Kila mwisho wa wiki huwaona watu wakimiminika kwenye eneo hili kujipumbaza. Hii si

fahari kwake tu, bali kwa nchi kwa jumla. Wale waliompinga na kumwita punguani wakati huo wamebaki kuinamisha nyuso tu; bila shaka wamefunzwa mengi.

Wanawake sasa wana haki ya kumiliki mali mathalani shamba. Kutokana na hili tumeshuhudia ongezeko kubwa la uzalishaji wa chakula mashambani na kwa hivyo kupunguza njaa na umaskini.

Biashara ndogondogo zinazoendelezwa sokoni na mitaani, kwa kiasi kikubwa, huhusisha wanawake. Biashara hizi huchangia pakubwa katika kuimarisha uchumi wa nchi kwani hutoa ajira ya kibinafsi kwa maelfu ya watu. Ushuru na leseni zinazokatiwa biashara hizi huongezea serikali pato la ndani.

Mgala muuwe na haki umpe. Ni ukweli kwamba tumekuwa na visa vya hapa na pale vya ukiukaji wa haki za wanawake. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba nchi hii imejitahidi mno kuendelea kumkwamua mwanamke kwayo. Hata mashirika ambayo hapo awali hayakupenda kuwaajiri wanawake, sasa yanawapa nafasi sawa na wanaume. Vyuo vikuu vya kibinafsi vimeanzishwa kuwasajili wanawake. Jijini humu, mna chuo kikuu cha sayansi cha wanawake. Aidha kumeanzishwa kituo (shule) cha kuwasajili wasichana kutoka familia maskini kujiunga na kidato cha kwanza. Wasichana hawa watapata wadhamini kutoka mashrika na watu mbalimbali ili kujiendeleza kimasomo.

Kumheshimu mwanamke ni miongoni mwa haki za kibinadamu ambazo shart zitekelezwe. Hata hivyo, wanawake wakumbuke kwamba hata wanapopuliza siwa kuhusu pupewa haki, lazima wao pia wawajibike. Wao ndio walimu wa kwanza wa wanao; ikiwa basi wataonekana kwenye vyombo vya habari wakining'inia juu ya magari ya wachunga magereza kwa kuzitafutia pesa za mayatima maumizi bora, watakuwa wanapotosha watoto wao. Wawe watu wa vitendo zaidi ya upayukaji.

<u>Maswali</u>

a) Kwa mujibu wa taarifa, ni mambo yapi yanayoonyesha ukiukaji wa haki za wanawake

b) Fafanua jinsi mwanamke aliyesoma huteseka maradufu zaidi ya mwanamme

c) Ni faida gani ambazo zimepatikana kutokana na wanawake kupigania haki zao?

d) Hatimaye wanawake wanahimizwa kufanya nini?

e) Eleza maana ya msamiati ufuatao jinsi ulivyotumiwa katika nakala

Kinyago…

Mabezo

f) Andika mfano wa mbalagha na uhuishi uliotumiwa katika makala haya

i) Mbalagha…………

ii) Uhuishi…………

8. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:-***

Uundaji wa istilahi – hasa za lugha ya Kiswahili ni shughuli nyeti na nzito hivi kwamba, haipaswi kupapiwa na mtu yeyote. Hii ni shughuli inayohitaji umakinifu zaidi kwa wanaoshiriki katika mchakato wa uundaji istilahi za kutufaa katika mawasiliano na kukuza Kiswahili kwa jumla. Ufanisi wa watu binafsi, vyombo vya habari kama vile Shirika la Habari la Kenya (KBC), Taifa Leo na mashirika mengineyo katika ukuzaji wa lugha hutegemea mno sera na utayarishaji wa serikali katika

kugharamia shughuli hii. Aidha, shughuli za kukuza lugha hukwama kwa sababu ya ukosefu wa fedha pamoja na sera maalum ya serikali kuhusu lugha.

Hata hivyo, katika kuyakwepa matatizo haya, pamekuwepo na hatua za kimataifa za kujaribu kusawazisha shughuli ya uundaji wa maneno. Hatua hii ilichochea kubuniwa kwa shirikisho la kimataifa la vyama vya usanifishaji istilahi mnamo 1936. Lengo la kitengo hiki lilikuwa ni kufafanua msingi madhubuti ya uundaji wa istilahi duniani. Kwa hakika, shirikisho hilo limesaidia mno katika kuweka misingi ya shughuli za ukuzaji wa istilahi. Misingi hiyo ni ya jumla na haihusu taaluma yoyote mahususi. Katika makala hii, tunapiga darubini baadhi ya misingi hiyo pamoja na mapendekezo yake.

Mosi, uundaji istilahi unafaa uanzie kwenye dhana na wala sio neno. Hii ina maana kwamba, kwanza pawepo na dhana au hali ambayo inahitaji itafutiwe neno au istilahi ya kuielezea. Inasikitisha sana kwamba pana wataalamu ambao wanaukaidi au kuukiuka msingi huu. Wanataaluma hawa hufanya mambo kinyume kwa kujibunia maneno yao na kuyahifadhi kwenye mikoba yao – halafu wakasubiri dhana izuke ndiposa waipachike istilahi yao. Pili, dhana zinabuniwa au kutolea istilahi au maneo ni muhimu zielezwe kwa ukamilifu na uwazi. Istilahi zinazoundwa zinafaa ziwe fupi iwezekanavyo na ziwe na uwezo wa kuelezea dhana kwa njia inayoeleweka bila utata. Tatu, maneno yanayoundwa sharti yawe na uhusiano wa aina fulani na dhana zinazowakilishwa na maneno hayo.

Uhusiano huo unaweza kuwa ama ni wa kimaumbile au wa kiutendaji. kwa mfano, Mzee Sheikh Nanhany wa Mombasa alipobuni istilahi 'uka' kwa maana ya 'ray'. Neno hili latokana na kupambauka au (kupambazuka kwa lafudhi ya kiamu. Neno 'image' ni jazanda kwa Kiswahili. 'Mirage' kwa Kiswahili ni 'mangati' (kutoka kwa mang'aanti) – yaani kung'aa kwa nchi. Mtaalamu mwingine aliyewazia uendajikazi wa kifaa na kubuni istilahi inayokubalika mpaka sasa ni Prof. Rocha Chimerah ambaye alibuni istilahi 'tarakilishi'. Pengine Prof. Chimerah alifikiria kazi ni kifaa husika na kuunda neno la Kiswahili linaloakisi kazi hiyo. Tunajua kwamba kompyuta hufanya kazi inayohusu tarakimu kwa haraka kama umeme. Labda Chimerah ameegemea sifa hii kuibuka na istilahi hii.

Maneno mengine ambayo yamebuniwa kufuatana na msingi huu ni ya Mzee Nabhanymathalan 'barua pepe' (e-mail), na wavuti (website). Tukiegemea maumbile, neno 'kifaru' lina maana ya vita ilihali tuna zana ya vita iliyopewa jina hilo kwa sababu ya labda kuwa na maumbile sawa na kifarumnyama. Nne, istilahi zinaweza kukopwa kutoka lugha nyingine. Yamkini hakuna lugha hata moja ulimwenguni-zikiwemo lugha duniani kama vile kiingereza zinazoweza kujitosheleza. Takriban asilimia 80 ya maneno katika kiingereza ni ya kukopwa. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili inapokopa, hali hiyo haipaswi kuchukuliwa kuwa ni lugha dhaifu.

Hata hivyo, istilahi zinazokopwa zi-nafaa zichukuliwe zilivyo katika umbo lao asili. Umbo hili linaweza kufanyiwa marekebisho machache tu, kulingana na sarufi na matumizi ya lugha kopaji.
Mifano ya istilahi kama hizi ni 'televisheni' (television), kopmpyuta (computer), kioski (kutokana na jina 'kiosk' la Kijerumani) na redio (radio), Tano, pale istilahi haiwezi kukopwa, lugha husika ijaribu kubuni msamiati ufaao, kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba, lugha inastawi. Lakini tahadhari inapaswa kuchukuliwa hivi kwamba, Kiswahili kisikope maneno kiasi cha kupoteza upekee wake. Mwisho, uundaji wa istilahi uzingatie mofolojia ya kawaida ya lugha. Istilahi zinazoundwa kwa kuzingatia mofolojia huwa rahisi kuiua maneno yenye uhusiano wa istilahi asili kwa njia ya mnyambuliko.

**Maswali**

(i) Taja mambo ambayo huchnagia ukuaji na ufanisi wa jumla wa lugha ya Kiswahili

(ii) "Lugha ya Kiswahili ni dhaifu na isiyotosheleza" Je, mwandishi wa makala haya ana msimamo upi kuhusu kauli hii?
(iii) Tahadhari zipi zinazofaa kuchukuliwa kabla ya kukopa istilahi kutoka lugha zingine?
(iv) Yape makala haya anwani mwafaka
(v) Eleza maana ya maneno yafuatayo:
(a) Dhana-
(b) Takribani –
(c) Istilahi – .
(d) Mofolojia –... .

**9.** ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:-***

Kitabu kinaeleza Mungu kamuumba mwanamke kutokana na ubavu tu wa mwanamume. Na hapa bila shaka ndipo linapojisalimishia shina lisilokuwa na mzizi thabiti la ubinafsi wa kiume – mwanamume akijijadilia kimoyomoyo. Ikiwa huyu mwanamke alitokana na ubavu wangu, yeye awe nani kwangu? Hakuna shaka ni wangu, mali yangu. Kwa sababu hii, miaka nenda miaka rudi mwanamke amekuwa akiugua na kuguna chini ya uonevu wa mwanamume.

Swala la kitabu kumleta duniani mwanamke kupitia ubavu wa mwanamume laweza kueleweka katika muktadha wa kile ambacho kimekuja kujulikana kama taasubi ya kiume. Na ili tuelewane barabara kuhusu maoni haya, tujisitishe kidogo katika kunusa tumbako huku tukijiuliza: ni nani au ni kina nani walihusika katika kubuni au kuandika hadithi ya asili ya mwanamke kitabuni? Ni kawaida ya binadamu kutazama na kueleza jambo kibinafsi. Asili ya mwanamke ilivyoelezwa kitabuni katika mkururo wa fikra hii yaweza kutambulikana kama uzushi tu.

Kiutamaduni, hasa wa Kiafrika, huku akiwa yuakua, mtoto wa kike husombezewa kasumba ya mawazo akilini, na kwa bahati mbaya sana, aghalabu na mamake au nyanyake, kuhusu namna anavyotarajiwa kutabasamu, kujinyenyekeza, na jumla kujidunisha mbele ya mvulana. Ni mwiko kwake kudhihirisha tabia za kimabavu, sitaji kujitetea, ili asije **akatiwa mdomoni** mitaani! Msichana atacharazwa na wazazi wake kwa ujasiri licha ya kuthubutu kupigana na mvulana. Na hapo ndipo ilipojificha siri ya kuwa anapoolewa na akosane na mumewe, daima yeye hutolewa makosa na kupatikana na hatia mbele ya wazee.

Wavulana kwa upande wao ni wanaume na lazima afanye mambo kiume. Si ajabu kuwa kinyume cha yale yanayowafika wasichana, wavulana wengi **huonyeshwa mbovu** na baba zao kwa sababu wamepigwa na wenzao. Ni vibaya baba kusikia mtoto (mvulana) wake amepigwa.

Nyumbani msichana hutarajiwa kujilindia heshima kimwili hasa kwa kuhifadhi ubikira mpaka aolewe. Anapotembea na wanaume huitwa Malaya. Ni ajabu kuwa hakuna bikira wala Malaya mwanaume. Mvulana ambaye hajajuana kimwili na mwanamke kabla ya ndoa huchukuliwa kuwa zuzu; ilhali anayetembea ovyo na wanawake ndiye dume.

Fauka ya hayo, inasikitisha kabisa kuwa mwanamke hana mahali pa kutua kikamilifu duniani. Kabla hajaolewa nyumbani, huchukuliwa kuwa mpita njia tu. Na anapoolewa ni poa kaolewa. Isitoshe mwanamke huolewa, haoi wala yeye na mume hawaoani. Mwanamke mahali pake ni jikoni pia anaonekana tu; ni hatia kwake kujaribu kusikika.

Mkutano kuhusu mwongo wa wanawake uliofanyika miaka miwili iliyopita jijini Nairobi ilinuiwa kupalilia vizuri mwamko juu ya ukweli kuwa binadamu ni binadamu na hakuna haja ya wao kubaguana. Tofauti za kimaumbile haziwezi kuwa hoja. Tusiupigie makelele ubaguzi wa rangi huko

Afrika kusini ilhali kwetu tuna ubaguzi wa kimaumbile. Tusipozingatia ushauri huu daima tutakuwa kwenye kile kinaya cha kuchekwa katika muktadha wa methali kuwa **nyani haoni ngokoye**.

Ni kweli kosa lilifanyika tangu awali ambapo kufumba na kufumbua, mwanamke akapigwa jeki na kuachwa akilewalewa katika hali ambayo hangeweza kujitetea hivyo basi akachukuliwa kuwa kiumbe duni. Lakini haidhuru, **yaliyopita si ndwele**, tugange yajayo. Kinachohitajika ni wanawake kuwa na nia na msimamo imara. Ni lazima wajifunge kibwebwe na kujitoa mhanga na kupambana dhidi ya taasubi ya kiume.

**Maswali**

(a) Andika kichwa kinachofaa kutokana na taarifa uliyoisoma

(b) Taasubi ya kiume ilianzaje?

(c) Katika utamaduni wa mwafrika ni kasumba gani anayosombezewa mtoto wa kike anapokua?

(d) "**Wavulana walidekezwa na utamaduni".** Eleza

(e) Taja kwa ufupi mambo muhimu yaliyoshughulikiwa katika mkutano wa mwongo wa wanawake mjini Nairobi

(f) ***Eleza maana ya semi zifuatazo kama zilivyotumiwa katika taarifa uliyosoma:-***

(i) Nyani haoni ngokoye .

(ii) Akatiwa midomoni

(iii) Huonyeshwa mbovu

(iv) Wajifunge kibwebwe

(v) Yaliyopita si ndwele ganga yajayo

**10.** ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

Asifuye mvua imemnyea. Huu ni msemo wenye hakika isiopingika, na kutilia shaka ni sawa na kudai jua linaweza kubadilika na kuchomozea upande wa magharibi badala ya mashariki. Huu ndio ukweli uliodhihirika juzi katika vyombo vyetu vya magazeti.

Lisemwalo lipo, na kama halipo li njiani. Waama, pafukapo moshi pana moto. Mwanafunzi mmoja wa kike kwa jina P.N. katika chuo kikuu kimojawapo nchini alishangaza umma wa Kenya na ulimwengu kwa jumla alipodai kuwaambukiza wanafunzi wenzake wa kiume mia moja na ishirini na wanne virusi vya Ukimwi.

Kisa na maana? Aliambukizwa Ukimwi na mwanafunzi mwenzake aliyekuwa akifanya majaribio ya ualimu katika shule yao ya upili. Baada ya kushawishika sana alijuana naye kimwili, na matokeo yakawa kifo ambacho sasa alikuwa anawagawia wenzake.

Kisa kama hiki kinachangia kueleza kina **kirefu cha kutamauka** na upweke ambao maisha ya waja wengi yameingia kiasi cha kuwaacha wanyama ijapo wanaenda kwa miguu miwili bado. Katika mojawapo ya mafunzo ya kidini ambayo Padre alinifunza mimi na wanafunzi wenzangu, tuliambiwa kisasi ni chake Mola, sisi waja wetu ni kushukuru tu. Mbona basi mwanafunzi kama huyu kutaka kulipiza?

**Ima fa ima**, na waswahili husema, "mlaumu nunda na kuku pia". Huyu mwanafunzi hawezi kuachiwa atende alivyotenda. Aliyekula naye raha alikuwa mtu aliyefahamika vizuri sana kwake. Isitoshe, huenda wakati huo alikosana na mama na baba kulala nje. Huenda alikosana na ndugu zake kwa kuepa nyumbani usiku wa manane kwenda kumwona huyu kalameni. Huenda alikosana na

mwalimu wake kwa sababu kiburi kilianza kuingia. Kwa vyovyote vile, alikula raha na hastahili kuwaadhibu watu wasio na hatia **kufidia makosa yake**. Je, kama yeye na huyo jamaa wasingekuwa na Ukimwi, raha kiasi gani wangezila hadi leo?

Jamii na watu wote kwa jumla hawana budi basi kulaani vitendo vya P.N. vya kuambukiza wanafunzi wenzake virusi huku akijua. Hili ni kosa ambalo linastahili adhabu ya kifo. Dawa ya moto ni moto ni adhabu inastahili kuchukuliwa haraka ili P.N. ambaye tayari amekiri hatia, atiwe nguvuni na adhabu itolewe.

Barua ya P.N. inafafanua jambo jingine sugu. Kwamba kiwango cha maadili katika vyuo vyetu kimezorota kiasi cha kufanyiana unyama usiosemeka. Vijana wengi siku hizi wanashiriki tendo la ndoa bila haya. Huu upotofu wa maadili katika jamii wapaswa kushutumiwa na wote. P.N. hana sababu yoyote ya kibinadamu, kidini au kitu chochote kile kudai haki kwa uovu huo wake.

**Maswali**

1.Taja kichwa kwa makala haya
2. Katika aya mbili za kwanza, mwandishi anamlaumu mwanafunzi kwa kosa gani?
Eleza chanzo cha tabia za P.N
4. Mwandishi wa taarifa hii anataka P.N achukuliwe hatua gani? Kwa nini?

5. Barua ya P.N. bila shaka imeonyesha uvumbuzi mpya. Utaje
6. Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumiwa katika taarifa:
(a) Kina kirefu cha kutamauka
(b) Ima fa ima
(c) Kufidia makosa yake

11. ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali*** **CHIMBUKO LA USHAIRI**

Ushairi ni fani kongwe kama mwanadamu mwenyewe alivyo mkongwe duniani. Na mashairi yamekuwepo kitambo sana hata kabla ya lugha ya Kiswahili bado haijanawiri na kushamiri kama ilivyo hivi leo. Ndipo tunasikia kuna mashiri ya kipemba, mashairi ya kimvita, mashairi ya kivumba, mashairi ya kipate, mashairi ya kiyunani, ya kirumi na kadhalika,. Almradi kila jamii na kila kabila lilikuwa na mashairi yake.

Katika utafiti na kongomano zao, wataalam wa arudhi za Kiswahili asili wamechambua na kufafanua kwamba mashairi ya Kiswahili asili yake ni nyimbo za jadi zilizokuwa zikiimbwa na manju, wangoi au waimbaji stadi wa tangu na tangu walipojumuika katika matukio na hafla mbalimbali kama za jando, arusi, matanga, ngoma na shangwe zao za maishani.

Nyimbo hizi zilitumiwa na watangulizi wetu, kidhamira hazikuhitalafiana hata kidogo na mashairi ya Kiswahili tunayohimiza wakati huu. Farka iko katika lugha na umbo kwani kila jamii ilitumia lugha yake na lahaja ya mazingira yake. Na kwa upande wa umbo, tungo hizo za awali kabisa hazikuwa na sanaa kwa maana ya ushauri tunauona leo. Bali tungo hizo zilijengeka katika nguzo mbili kuu. Kwanza ni uzito wa mawazo maadilifu ambayo yalitaamaniwa sana. Na pili ni mizani ya sauti ya manju kulingana na lahani, pumzi zake pamoja na madoido katika uimbaji ambao ulikuwa burudani naathari katika noyo za wasikilizaji wake.

Kwa kifupi ni kwamba, nyimbo hizo ziliuhifaid umma kwa njia mbili, mawaidha kwa mapana na taathira au jadhba kutokana na sauti tamu ya manju.

Kama utakubalika, basi huo ndio ushairi wa awali kabisa ullioambatana na nyimbo zetu za kienyeji. Kila kabila katika nchi zetu lilikuwa na ushauri wake au nyimbo zake zenye undani uliolenga sababu maalum na tukio maalum katika jamii.

Nyimbo kama hizo kwa jina la sasa tunaweza kuita mashairi ndizo zile zilizoitwa 'mwali' na wakamba; gichandi kwa 'wakikuyu'; 'gigia gi sigele' kwa waluo na 'wagashe' kwa wasukuma zilikuwa na undani wa kipekee tena uliodidimia ambao si bure kutolewa hadharani.

Aina za mashairi ya watu wa mwambao ni kama lelemama, misemele, gungu, nyiso, kongozi n.k.

***(Walla Bin Walla – Malenga wa Ziwa Kuu , E.A.E.P)***

1. Ni nini haswa chimbuko la ushairi?
2. Kulingana na kifungu hiki, ni nini umuhimu wa ushairi ?
3. Ni maswala gani yaliyowapendeza wasikilizaji wa tungo hizo za zama ?
4. Tofauti kati ya nyimbo za zama na ushairi wa leo upo kwenye vipengele gani viwili ?
5. Kifungu : '**haijanawiri na kushamiri'** ina maana gani katika lugha nyepesi ?
6. **Eleza maana ya :**

   (a) Kongamano …

   (b) Jadhiba (c) Farka (d) Awali..

12. ***<u>Soma taarifa hii kisha ujibu maswali</u>***

Chamkosi alipiga goti huku machozi yakimdondoka njia nne nne. Mbele yake, palikuwa na makaburi mawili. Waliokuwa wamelala mle hawakuwa na habari juu ya kihoro na simanzi ya aliyepiga magoti pale. La kwanza, lilikuwa kongwe kiasi na lilikuwa limemea vichaka na magugu. La pili lilionyesha upya kwani shada za maua zilizowekwa na waombolezaji zilikuwa bado kukauka. La kwanza, ndimo babake mzazi alipolala. Nalo la pili, ndimo mamake alimolazwa kiasi cha siku mbili zilizopita.

Kwa Chamkosi, maisha hayakuwa na maana tena. Alikuwa mwanafunzi wa miaka kumi na miwili. Hakuwa amehitimu kujitegemea na kukimu mahitaji yake. Aliokuwa akiwategemea sasa wamemwacha akiwa yatima. Hakuna yeyote ambaye angejaza pengo la wazazi wake wawili kwa kipindi cha mwaka mmoja. Haya yalikuwa kama donda sugu lisilopona.

Kwa sasa, Chamkosi anayakumbuka mengi. Anakumbuka maisha ya babake. Alikuwa jibaba nene, zito lenye sura jamala na sifa nzuri. Baba mtu alikuwa na chake na alijiweza kiuchumi. Wengi pale mjini walimheshimu na kumstahi kutokana na uwezo wake wa kiuchumi. alitunza familia yake vizuri. Chamkosi hakumbuki siku moja aliyokosa chochote alichohitaji kutoka kwa babake. Alikuwa na bidii kazini mwake pia.

Walakini, kama mja asiyekamilika, baba mtu alikuwa na dosari moja. Aliyapenda maisha ya anasa na kufukuzia wasichana wadogo pale mtaani. Mamake Chamkosi aliyajua haya. Alijaribu kuzozana na mumewe ili aachane na tiabia hizi lakini kila akitaka ushauri, mama mtu alikemewa na kufokewa kuwa aache upuzi wa wanawake. Akafikia kufyata ulimi na kumwachia Mungu aongoze maisha ya bwanake.

Hata hivyo hakuna marefu yasiyo na kikomo. Baada ya kuponda raha na vimada si haba, baba mtu alianza kuugua. Maradhi yake yakawa ni msururu. Mara, alipata mafua yasiyopona, mara kuendesha, mara maradhi ya ngozi. Haya yalimtia wasiwasi. Baada ya kukaguliwa na daktari, alipatikana kuwa *ameumwa na mbuzi.* Hakuamini haya. Baba aliyekuwa bashasha na mcheshi aliingiwa na upweke na kutotaka kutangamana na yeyote hata jamaa zake.

Waliosema kuwa hakuna msiba usiokuwa na mwenzake, hawakukosea. Maradhi ya baba mtu yaliifilisi jamaa huku waking'ang'ania kumtafutia tiba. Wakaenda kwa waganga si haba. Waganga nao wakafaidi tamu.

Muda si mrefu, mama mtu naye akaanza kuugua. Baada ya uchunguzi, alipatikana kuwa na maradhi yayo hayo ya bwanake. Ikawa ni kama mji umelogwa. Baada ya muda mfupi baba mtu aliaga dunia, mama naye hakukawia. Naye akasalimu amri na kumfuata bwanake kaburini. Familia ikawa kama inaangamia. Chamkosi kijana mdogo akaachwa pweke.

Kama kawaida, mja hakosi neno. Wengi walisikika wakisema hili na lile kuhusu vifo hivi. Wengi walieneza uvumi. Lakini, Chamkosi alijua ukweli wa vifo vya wazazi wake.

Sasa hapa alipo aliyatambulia macho makaburi ya wazazi wake, anasononeka. Anaomboleza zaidi kifo cha mamake ambaye alimwona hana hatia na hakupaswa kufa kwa maradhi yale. Anaukumbuka vizuri wema wa mamake usio na kifani. anakumbuka alivyojitunza kama mke na mzazi.

Anakumbuka jinsi mamake alivyomshughulikia babake katika siku zake za mwisho licha ya baba mtu kuungama maisha yake maovu. Chamkosi alishindwa kujua kwa nini mamake akawa msamehevu kiasi hicho. Hakukosa kukumbuka wasia wa mama yake. Haya yalimfariji. Faraja hizi zilimpa nguvu mpya za kuyakabili maisha.

Chamkosi aliwaza juu ya maisha yake. Akaona kuwa, kama yatima atawategemea wafadhili miongoni mwa jamaa na marafiki wenye huruma iwapo wapo. Aliwaza jinsi anasa za babake zilivyowaathiri watu wengi.Alitambua kuwa Ukimwi haumwathiri aliyeupata tu, bali na wengine wengi. Kweli, mtego wa Panya huingia waliokuwemo na wasiokuwemo. Lakini akiwatazama watu, hakuelewa kwa nini walidhamiria kuishi ujingani. Aliwaona baadhi ya vimada wa babake wakishikana viuno na vijana wadogo. Akawasikitikia. Akabaki na swali kwa nini watu wengine wanafikiria kuwa virusi hivi haviwezi kuwapata. Kwani wanafikiria kuwa vinabagua na kuwa wao hawahatarishi maisha yao? Alishindwa kufahamu watu watabadili vipi mienendo yao miovu na waweze kukabili janga hili lini?

Kwa wakati huu, Chamkosi alikata shauri kusomea Taaluma ya Uelekezi na Ushauri kutokana na vifo vya wazazi wake. Alitaka kupata ujuzi utakaomwezesha kuwashauri na kuwaelekeza vijana wenzake ambao wanahatarisha maisha yao. Kama mshauri, alinuia kuhamasisha na kuzindua jamii juu ya hatari za Ukimwi.

Alitaka kuhakikisha kuwa hatua zimechukuliwa na kila mtu katika jamii kukabili janga hili n kuliangamiza

Chamkosi aliomba dua fupi. Akainuka na kuondoka huku akiwa na faraja na matumaini moyoni kutokana na azimio lake lile.

(a) Toa kichwa mwafaka kwa makala haya

(b) Eleza madhara mawili ya ugonjwa sugu uliotajwa katika makala haya

(c) Taja mifano ya tabia zinazoweza kumfanya mtu aathiriwe na ugonjwa wa Ukimwi

(d) Tofautisha tabia za baba na mama wa Chamkosi

(e) Chamkosi baada ya kufikwa na madhila hayo yote aliamua kufanya nini? Toa maoni

(f) ***Eleza maana ya:***

(i) Tumbulia macho ..........................................................................................................
(ii) Ameumwa na mbuzi.........................................................................................

13. ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

Licha ya kuwa na historia ya kiasi, maisha ya binadamu ni kioja kikubwa. Hebu jiulize jinsi uhai wako wewe mwenyewe ulivyoanza sembuse unavyoweza kupumua na kuishi siku nenda siku rudi.

Dini zimefahamisha kuwa sisi binadamu tumeumbwa na Mwenyezi Muumba. Hata hivyo muumba hutumia mume na mke kutuanzishia maisha yetu humu humu duniani. Uhai wa hapa duniani huanzia katika tumbo la mwanamke muda mfupi tu baada ya mume na mke kushirikiana katika tendo la kujamiana. Katika ngono hii yenye ufanisi, mbegu moja ya manii kutoka kwa mwanamume, hudunga na kujiingiza katika yai la mwanamke huku ikilirutubisha. Tangu hapo mtu huwa na mama akawa mjamzito. Hatua ya kwanza ya uhai!

Wanasayansi wametuthibitishia kuwa mbegu katika shahawa kutoka kwa mwanamume ina kromosomu ishirini na tatu (23) nalo yai la mwanamke lina idadi iyo hiyo ya kromosomu. Basi katika hatua ya kwanza ya uhai wake, binadamu ana kromosomu arubaini na sita (46).

Kromosomu hizo zote ndizo humfanya mtu kuwa mkamilifu kwa kukadiria mambo mbalimbali adhimu. Kwa mfano, kukadiria kama kiumbe kitakuwa cha kike au cha kiume, mtu mweupe au mtu mweusi, mwerevu au wa wakia chache, mwenye nywele za singa au za kipilipili, atakuwa na damu ya namna gani, michoro ya vidole vyake itakuwa vipi na hata utu wake utakuwa wa namna gani katika siku za usoni.

Elimu yote anayopata mtu kutoka kwa jamii na mazingira huweza tu kujenga juu ya yaliyokwisha kuanzilishwa na kromosomu katika yai lililorutubishwa tumboni.

Haihalisi kabisa kufikiria kwamba huwa katika **hali ya ukupe**. La hasha! Yeye hujitegemea kwa vyovyote na ana upekee wake. **Hatangamani na mama yake**. Roho yake humdunda mwenyewe na damu yake ambayo huenda ikawa tofauti kabisa na ya mama yake, humtembea na kumpiga mishipani mwake. Isitoshe, yeye si mojawapo katika viungo vya mwili wa mama yake vinavyomdhibiti katika **himaya** yake ndogo.

Amini usiamini, hapana binadamu hata mmoja ambaye amewahi kuwa sawa kimaumbile na mwingine na wala hatakuweko. Hata watoto pacha kutoka yai moja la mama hawawi sawa, lazima watofautiane. Si nadra kusikia mtu amepata ajali akahitaji msaada wa damu, na pakakosekana kabisa mtu hata mmoja kutoka jamaa yake wa kimwauni. Basi ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni.

**Maswali-**

1. Ipe taarifa uliosoma anwani mwafaka
2. Mwandishi ana maana gani anaposema '**ngono yenye ufanisi**'?
3. Uchunguzi wa sayansi umekita mizizi imani gani ya kidini?
4. Taja majukumu yoyote **matano** yanayotekelezwa na kromosomu
5. Katika makala, elimu kutoka kwa jamii na mazingira yaelekea kuwa bure ghali. Kwa nini?
6. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala:-
   (i) huwa katika hali ya ukupe…
   (ii) himaya
   (iii) hatangamani na mama yake

14. ***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali***

Kwa zaidi ya mwongo mmoja uliopita, ulimwengu mzima uliathiriwa na masaibu ya kifua kikuu kwa kiwango cha kuogofya kiasi kwamba katika mwaka wa 1993, shirika la afya duniani (WHO) lilitangaza ugonjwa huu kuwa swala dharura la kimataifa.

Ongezeko kubwa la visa vya kifua kikuu lililotokana na kuchipuka kwa **viini** vinavyosababisha maradhi hatari ya Ukimwi na magonjwa yaliyohusiana na punde baadaye ilibainika kuwa bara la Afrika lilikuwa ndilo lililoathiriwa zaidi na Ukimwi pamoja na maradhi ya kifua kikuu. Hii ndiyo hali inayotawala sasa ulimwenguni. Afrika likiwa bara linaloongoza kwa wagonjwa walioambukizwa viini vya Ukimwi lilikuwa likishuhudia visa vya maradhi ya kifua kikuu.

Viini vya Ukimwi vinapunguza uwezo wa mwili wa mgonjwa kupigana na vijidudu vya maambukizi. Swala linalowafanya wagonjwa hawa kutodhibiti maambukizi ya magonjwa mbalimbali. Katika hali ya kawaida mwili wa mtu kama huyo unaweza kujikinga dhidi ya viini kama hivyo. Maambukizi kama haya kawaida hujitokeza kukiwa na nafasi duni ya kinga mwilini. Katika baadhi ya mataifa kama vile Kenya, maambukizi ya kifua kikuu hufanyika mapema katika umri mchanga maishani.

Kwa kawaida, viini hivyo huwa havisababishi ugonjwa wenyewe. Badala yake, kinga katika mwili wa aliyeambukizwa unaweza **kusitiri** maambukizi hayo bila mhusika kuwa mgonjwa kutokana na sababu mbalimbali. Viini hivyo baadaye vinaweza kuwa hai tena na kumfanya mgonjwa kukumbwa na ugonjwa. Swala hili kwa kawaida hujitokeza wakati mgonjwa anapoambukizwa virusi vya Ukimwi. Virusi hivyo pia huongeza hatari ya ugonjwa kujitokeza baada ya maambukizi au pengine kujitokeza tena baada ya mgonjwa kupokea tiba ya kwanza.

Kulingana na utafiti, inakadiriwa kwamba mmoja kati ya wagonjwa wawili au watu wenye virusi vya Ukimwi watapata kifua kikuu wakati mmoja katika maisha yao. Inakadiriwa kwamba karibu asilimia 50 hadi 60 ya wagonjwa wenye maradhi ya kifua kikuu nchini Kenya pia wameambukizwa viini vya Ukimwi. Kwa upande mwingine, maradhi ya kifua kikuu hujitokeza kama kawaida kwa wagonjwa wenye virusi vya ukimwi. Kwa hivyo, wakati wa kushughulikia wagonjwa ni lazima pia wafanyiwe uchunguzi wa kubaini ikiwa wameambukizwa kifua kikuu.

**Maswali**

(a) Ipe taarifa uliyoisoma kichwa mwafaka
(b) Ni nini hasa kilichochangia kuongezeka sana kwa maradhi ya kifua kikuu?
(c) Kwa kifupi, eleza ni kwa nini ugonjwa wa Ukimwi ni hatari mwilini
(d) Ukimwi na kifua kikuu una uhusiano mkubwa, eleza uhusiano huu kulingnana na taarifa uliyoisoma
(e) Andika urefu wa neno 'Ukimwi"
(f) Eleza mambo mawili ambayo yametokana na utafiti
(g) Ni jambo lipi ambalo ni la kushangaza kuhusiana na kifua kikuu
(h) Andika maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu hiki
(i) Kusitiri
(ii)Mwongo
(iii) Swala la dharura.
(iv)Viini

15. ***Soma makala yafuatayo kisha kisha ujibu maswali:-***

Waajiri wengi wanazilaumu taasisi za elimu kwa kukosa kutoa wafanya kazi wenye ujuzi tosha, hasa wa kiteknolojia za kisasa kama kutumia kompyuta kutenda kazi mbalimbali. Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha sana.

Ujuzi wa kuweza kutumia Kompyuta unaweza kumfaa mwanafunzi hata anapokosa nafasi ya kujiunga na chuo kikuu kwa vile anaweza kuendelea na elimu yake kupitia kwa elimu mtandao. Pia anaweza kufanya utafiti wa kina kupitia intaneti na kwa njia hii akaimarisha elimu yake.

Mojawapo ya njia ya kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia ni kuanzishwa kwa mikakati mipya ya kufunza. Somo la Kompyuta laweza kuimarika mashuleni endapo kwanza walimu watahamasishwa juu ya faida za ujuzi huu.

Kwa kutumia Kompyuta kufunza, walimu wanaweza kufunza madarasa kadhaa katika kipindi kimoja bila kulazimika kuyahudhuria. Hii itapunguza kiwango cha kazi kwa walimu kwa vile watapata muda wa kufanya utafiti mpana. Aidha, watapata habari na ufahamu zaidi wa mambo kwa kutumia mitambo ya Kompyuta kutoka kwenye intaneti, kupitia tovuti.

Hata hivyo mipango hii inakabiliwa na changamoto kama vile bei za juu za mitambo na vifaa vya Kompyuta, ukosefu wa miundo msingi itakayowezesha utumiaji wa mitambo hii na ukosefu wa walimu waliohitimu somo la Kompyuta.

Pia, kuna tatizo la ukosefu wa nguvu za umeme hasa maeneo ya mashambani; vile vile, katika maeneo yaya haya, wanafunzi na wazazi wengi huvichukulia somo la Kompyuta kuwa gumu na linalofaa wakaazi na wanafunzi kutoka maeneo ya mijini na linalofaa wakaazi muhimu kwao mashambani.

**<u>Maswali</u>**

(a) Ipe taarifa uliyoisoma anwani inayoifaa

(b) "Hali hii imekuwa ya kuhuzunisha." Ni hali gani inayozungumziwa katika aya ya 1? (c) Ujuzi wa kutumia Kompyuta unaweza kumfaidi vipi mwanafunzi?

(d) Mikakati mipya ya kuimarisha elimu kuhusu maswala ya teknolojia inakabiliwa na vizingiti vipi?

(e) Taja manufaa **mawili** ambayo mwalimu anaweza kupata kutokana na ujuzi wa teknolojia ya Kompyuta

(f) Andika msamiati mwafaka zaidi kwa maneno yafuatayo:

(i) **Kompyuta**

(ii) **Intaneti**

# Ufupisho

1. ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

Umaskini ni tatizo sugu katika jamii. Binadamu wengi hujikuta katika hali hii kwa sababu hawakubahatika kusoma. Baadhi yao huenda walijaribu kusoma wakashindwa mapema kujipandisha kielimu. Ukosaji wa elimu huchangia sana katika kukuza ukata. Elimu huweza mtu kupata tonge kwa kujipatia kazi za kumwezesha kuyakidhi mahitaji ya maisha. Hali kadhalika, elimu humsaidia binadamu kupata maarifa mengi ya kutendea shughuli zake za kimaendeleo. Kwa mfano, kama ni wakulima wanaweza kutumia **pembejeo** zifaazo ili kuboresha uzalishaji wa mazao. Wakulima wenye elimu hawatapendelea njia duni za kuendeleza kilimo kama vile kutumia visagilima na mbinu nyingine za kijadi. Badala yake watatumia njia za kisasa za kuvunia mazao yao.

Umaskini mwingine huwa mwiba wa kujichoma. Baadhi ya watu ni mikunguni. Kulaza damu kwao kunawafanya kuwa wategemezi katika familia na jamii kwa jumla. Kwa vile hawajazoea kuinamia cha mvunguni, hata wakifunzwa kuchakura hawawezi. Ili kujaribu kuutibu uwele wao na ufukara baadhi yao hutafuta njia za mkato kama vile upwekuzi wa vitu vya wale waliojitahidi. Wakifanikiwa huweza **kufurisha vibindo vyao.** Hata hivyo mkono mrefu wa walinda usalama ukiwakumbatia wao hubakia kusagika kwa dhiki isiyomithilika ndani ya magereza.

Majanga ya kimaumbile kama vile mitetemeko ya ardhi, mikurupuko ya maradhi hatari, moto, ukame na mafuriko huchangia na kuzidisha umaskini. Matukio hayo yakiandama kidindia watu wengi huhasirika. Licha ya mali nyingi kupotea, manusura huachwa wakiwa maskini hohehahe. Matumizi yao hupotea kwani wengi huhitajika kuanza maisha upya.

Vijana ni nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote ile. Endapo watajiingiza katika uraibu wa dawa za kulevya, wataathirika wao wenyewe na jamii kwa jumla. Pamoja na kuwa vijana hawa hufuja pesa nyingi katika ununuzi wa dawa hizi, dawa zenyewe huwadhoofisha na kuwapoka nguvu za kushiriki katika uzalishaji mali. Kutokana na hali hii,umaskini hupaliliwa na kushamiri zaidi.

Umaskini huzua matatizo mbalimbali katika jamii. Ufukara huchachawiza juhudi za serikali za kuwapa raia wake mahitaji ya kimsingi kama vile huduma za afya. Pia umaskini husababisha maovu mbalimbali ya kijamii kama vile mauaji na ukahaba.

Baadhi ya wanajamii huona kwamba njia ya kipekee ya kukabiliana na changamoto zinazosababishwa na hali ya ulitima ni kupitia kwa biashara haramu. Hali hii huchochea zaidi kudorora kwa maadili ya kijamii.

Mataifa mbalimbali ulimwenguni yamezua mikakati mahsusi ya kukabiliana na umaskini. Baadhi ya mataifa yamebuni utaratibu maalum wa kupunguza mwanya mkubwa uliopo kati ya matajiri na maskini. Mojawapo ya mipango hiyo ni kupandisha viwango vya kodi inayotozwa wenye mishahara minono na wafanyibiashara wenye pato kubwa. Aidha huduma za burudani hutozwa kodi ya kiwango cha juu. Kupitia kwa kodi hizo, na njia nyinginezo, serikali za nchi hizo hupata pesa za kuwahudumia maskini.

Mataifa yanayoendelea yanaweza kuwakwamua wananchi kiuchumi kwa kuwapa wahitaji mitaji ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo. Mifano ya miradi hiyo ni viwanda vya ‘Jua kali’, ususi wa vikapu na uchongaji wa vinyago. Hali kadhalika, serikali inaweza kuwatafutia masoko ya nje wafanyi biashara wadogo wadogo. Aidha, serikali inaweza kupunguza ushuru kwa bidhaa zinazoagizwa na masoko ya nje wafanyibiashara wa aina hiyo. Mathalan, ushuru unaotozwa nguo kuukuu zinazoingizwa nchini ukipunguzwa, wauzaji wa nguo hizi watafaidika zaidi na hali ya umaskini itaendelea kupungua.

Sehemu za mashambani ni mhimili mkubwa wa uchumi. Ingawa kumekuwa na juhudi za kuzistawisha sehemu hizi kwa kusambaza huduma za umeme na maji kwa gharama nafuu, bado hali haijawa ya kuridhirisha. Ili kuimarisha sehemu hizi na kukabiliana vilivyo na tatizo la umaskini, hatuna budi kusambaza huduma hizi hasa katika sehemu kame. Sehemu hizi zikipata maji, kilimo chenye natija kitaendelezwa na umaskini utakuwa karibu kuzikwa katika kaburi la sahau. Ikiwa tutazitekeleza sehemu hizi, vijana wanaoweza kusistawisha watahamia mjini kutafuta maisha ‘bora’. Hali hii itazidisha msongomano wa watu mjini.

Umaskini ni nduli ambaye lazima aangamizwe ima fa ima. Vijana hawana budi kubadili mtazamo wao hasa kuhusu kazi za mashambani na kujitahidi kuimarisha kilimo. Fauka ya hayo, mifumo mwafaka ya elimu ibuniwe ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi ya taifa. Badala ya kuhimiza elimu ya kinadharia, elimu tekelezi isisitizwe zaidi ili wale wanaokosa kazi za kiafisi waweze kujiajiri katika kazi za kiufundi. Ukusanyaji wa ushuru uimarishwe zaidi. Hali ya usalama iendelee kustawishwa ili kuzidi kuwavutia wawekezaji, na hivyo kubuni nafasi zaidi za kazi.

**Maswali**

(a)Kulingana na kifungu '**umasikini ni hali inayoletwa na udhaifu wa mtu binafsi'**. Jadili (maneno 30-40)

(b)Jamii ina uwezo wa kukabiliana na hali ya umaskini inayowakumba raia wake. Thibitisha kwa mujibu wa kifungu (maneno 40-50)

2. **MENO YA BINADAMU**

Kila mara tunapokula, meno yetu huuma, kutafuna na kusaga chakula tunachokula. Meno yanatuwezesha kukivunja chakula ili kuwezesha mwili wetu kukitumia. Ili mwili uweze kukitumia chakula hicho, pana vitu fulani vinavyokifanyia chakula hicho kazi mpaka kikaweza kuingia kwenye mwili wenyewe. Hivi hujulikana kama vimeng'enya. Binadamu ana meno ya aina nne kuu. Kwanza, kuna meno ya mbele au makato ambayo kazi yake ni kuuma au kukata chakula. Haya yanasaidiana na mengine yanayojulikana kama michonge; yanakata pia lakini yako sehemu ya nyuma. Michonge hufuatwa na meno mengine yanayosaga chakula na ambayo hujulikana kama masagego. Masagego hufanya kazi na meno mengine yajulikanayo kama magego. Kazi ya aina hizi mbili za meno ni kutafuna na kusaga chakula kabisa kabla ya kukimeza. Idadi ya meno ya mtu mzima ni thelathini na mbili. Bila ya kuwa na meno mazuri, binadamu hukabiliwa na matatizo makubwa wakati wa kula. Meno huweza kuharibika kwa sababu ya kutopigwa mswaki vizuri mara kwa mara. Ili kuhakikisha kuwa meno yetu ni mazuri, pana umuhimu wa kudumisha afya nzuri ya meno. Kila baada ya kulala, lazima tuhakikishe tumeyapiga mswaki vizuri bila ya papara ili kuondoa mabaki ya chakula yanayoweza kuwa chanzo cha viini vinavyoharibu meno. Pili, lazima tuhakikishe kuwa hatuharibu ufizi wa meno, yaani ile nyama inayoshikilia meno hasa kwa vijiti katikati ya meno baada ya kula. Afya ya meno ni muhimu ili kuhakikisha kuwa meno yetu yanadumu na kuendelea kutufaidi katika uhai wetu.

. (a) Kwa nini ni muhimu kudumisha usafi wa meno?
(Tumia maneno yasiyozidi 25)

(b) Fupisha taarifa uliyosoma. (Tumia maneno yasiyozidi 80).

**3.** ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Nchi nyingi za ulimwengu wa tatu huathirika na biashara ya kimataifa.Biashara hiyo inaweza kuwa inafanya kwa uagizaji ama uuzaji wa bidhaa za nchi nyingine.

Biashara ya kimataifa ina umuhimu mkubwa. Kwanza, inawezesha nchi kupata bidhaa ambazo haitengenezi mbali na kusaidia kuwepo na uhusiano kati ya nchi mbalimbali. Uhusiano huu huiwezesha nchi kupata bidhaa kwa bei rahisi kuliko ambavyo ingekuwa kama zingetengenezwa kwao, hasa ikiwa nchi inayohusika haina malighafi yanayohusika katika utengenezaji wa bidhaa hizo. Pia husaidia wakati nchi imekumbwa na dharura au majanga kwani itaauniwa na nchi nyingine ingawa hali kama hii haihakikishwi, ushirikiano huu vile vile huchochea upatikanaji wa nafasi za kazi kwa wengi.

Kwa sababu za kushughulikia utengenezaji wa bidhaa na utoaji huduma nyingine kutokana na uzoefu wa muda na kuwepo raslimali, nchi huwa na uzoefu fulani. Ni kwa sababu hii nchi inawezeshwa kupata pesa za kigeni na kuuza bidhaa za ziada.

Hata hivyo kuna matatizo yanayozikumba nchi za kiafrika katika biashara hii. Kwanza, biashara ya aina hii hutatiza viwanda vichanga katika nchi zinazoendelea kwa ushindani usio sawa. Ajabu ni kwamba nchi zilizoendelea zimetumia bishara hii 'kutupa' bidhaa za hali ya chini ama zenye athari kwa hali za kijamii.Urafiki haukosi. Ikiwa nchi inategemea uagizaji wa bidhaa,

haitaweza kuikosea ama kuhitilifiana na nchi ambayo inategemea, hivyo kuathiri uhuru wa nchi kama hiyo.

Hata hivyo, nchi mbalimbali zimeweka mikakati ya kulinda viwanda kutokana na athari ya biashara kama hii. Baadhi zimeweka ushuru wa juu kwa bidhaa zinazoagizwa utoka nje kwa wasio washirika wa kibiashara. Licha ya hayo, baadhi ya bidhaa zinazonuiwa kwa nje kwa matumizi ya kielimu, utafiti wa kisayansi nabidhaa za maonyesho huagizwa bila ushuru huo. Wakati mwingine ni benki kuu ndiyo hutoa leseni kwa niaba ya serikali kama njia ya kudhibiti bidhaa kutoka nje. Njia nyingine ya kuvisaidia viwanda nchini ni kuuza bidhaa kwa njia ya kuvipunguzia ushuru, usafirishaji nafuu na kuvipa ushuru.

Serikali nyingine huhakikisha kuwa ni bidhaa kiasi fulani tu ambazo zinaweza kuagizwa kwa kipindi fulani. Kwa mfano, kuna idadi fulani ya magari kutoka nje yanayoweza kuagizwa kuja Kenya kwa mwaka mmoja. Hata hivyo, wakati mwingine, serikali husitisha uagizaji wa bidhaa kama vile dawa, sinema, maandishi ya kisiasa na vitabu kutoka nje; bidhaa ambazo zinachukuliwa kuwa hatari kwa nchi. Licha ya matatizo haya, biashara imekuwepo na inaendelea kujiimarisha.

**Maswali**

(a) Kwa mujibu wa mwandihsi wa makal haya, bishara ya kimataifa itaendelea kujiimarisha.
Eleza (al. 6) (maneno 40-50)

(b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya mbili za mwisho. (maneno 40-50)

**4.** ***Soma taarifa inayofuata kisha ujibu maswali yaliyoulizwa***

Usafiri ni upelekezi wa watu na bidhaa au mizigo kutoka mahali pamoja hadi mahali pengine. Tuseme kutoka kituo A na kuenda kituo B.

Katika ulimwengu wa leo, watu na bidhaa husafirishwa barabarani kwa mabasi au motokaa za kila aina au kwa kutumia magari moshi yanayopita juu ya reli, au meli zinazopita majini, kadhalika, usafiri unaweza kufanyiwa hewani.

Hivyo, hali haikuwa hivyo zamani. Usafiri uliojulikana sana kale ni usafiri kwa miguu. Watu waliposafiri kutoka eneo moja hadi jingine walilazimika kufanya hivyo kwa miguu. Kadhalika, watu waliposafirisha mizigo mizito kutoka eneo moja hadi nyingine, iliwabidi kuibeba mizigo hiyo wao wenyewe. Mpaka leo usafiri huu upo.

Wanyama vilevile walitumiwa kama njia moja ya usafirishaji. Huku Afrika ya mashariki kulitumika wanyama wengine kama vile punda. Punda ni mnyama anayependwa sana kwa sababu anaweza kuenda mwendo mrefu pasipo na kunywa maji. Mpaka leo, mnyama huyo hutumika sana na wamaasai, wagala, warendile na wengine.

Mnyama mwingine aliyetumika sana, na mpaka leo anaendelea kutumika ni ngamia. Ngamia anafaa sana katika usafiri wa jangwani. Kwato za ngamia huweza kusafiri kwa urahisi jangwani ama popote penye mchanga mwingi kwa sababu kwato zake hazizami kwenye mchanga. Isitoshe ngamia wanaweza kwenda mwendo mrefu bila maji au chakula huku wakitegemea mafuta yaliyohifadhiwa kwenye nundu zao.

Katika ulimwengu wa kisasa, binadamu amepiga hatua kubwa sana katika masuala ya usafiri. Baadhi ya maendeleo hayo ni ya kustaajabisha. Kwa mfano, binandamu anaweza kuruka kwa kutumia vyombo vya angani kwenda kwenye anga za mbali. Katika karne iliyopita binadamu anaweza kuruka kwa kutumia vyombo vya angani kwenda kwenye anga za mbali. Katika karne iliyopita binadamu amefika mwezini kwa kutumia vyombo hivyo. Kuna tetesi kwamba sasa anajaribu kuzizuru sayari zilizoko mbali na ardhi.

Ama kwa hakika, usafiri bora in kipimo kimojawapo cha maendeleo ya nchi yoyote katika ulimwengu wa sasa. Bila njia ya kisasa za usafiri, baadhi ya mambo yanayofanyika katika nchi zetu hayangefanyika.

(a) Katika habari hii, punda na ngamia wana sifa gani muhimu zinazowawezesha kutumiwa kwa usafirishaji? (maneno 30-40) (ala. 6, 1 mtiririko))

(b) Kwa mujibu wa taarifa, usafiri wa zamani unatofautiana vipi na ule wa siku hizi?
(maneno 40-50) (al. 7, 1 mtiririko)

**5.** ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

Sisi vijana wa Kenya inatupasa tuwajibike kufanya kazi kwa bidii na kwa dhati ya mioyo yetu uweze kupata ufanisi na uwezekano wa kuinua nchi yetu changa katika kiwango cha juu. Tukumbuke, “Ajizi ni nyumba ya njaa”. Kwa hivyo basi haifai kulaza damu ikiwa matatizo chini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja. Sharti tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani katika nchi yetu.Tunahitaji taifa la watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo. Tupende tusipende lazima tuzidishe mazao mashambani, kwani kila kukicha idadi ya watu inaongezeka. Ni sharti tuweze kujitosheleza katika vyakula. Zaidi ya hayo lazima tujishughulishe na biashara ambapo kwa sasa ni Wakenya wachache sana ambao wanatambua umuhimu wake. Wengi ni wale wenye mawazo kwamba lazima kila mmoja aajiriwe maishani. Yatupasa tujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaachia wageni .

Mafunzo tunayopata nyumbani, shuleni na hata katika jamii, lazima yatuwezeshe kutambua mbinu za kupitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itamfanya mwana Kenya kujua wajibu wake katika jamii. Tumesinywa na elimu pumbao; inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele. Sisi vijana tukiwa viongozi wa siku zijazo tuwe kielelezo chema kwa wengine. Watu wazima washirikiane na kufikiria kwamba wao ni wamoja, “Utengano ni uvundo”. Lugha ya taifa ndicho chombo cha pekee ambacho kinatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu ,wakati tunapokosea na kufanya masahihisho mara moja kwani, :Usipoziba ufa, utajenga ukuta. “Tusikasirike kwa sababu tumesahihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi.

Sisi tukiwa vijana sharti tujishughulishe na kuyaangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia za kutatua matatizo hayo. Siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashtumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu shuleni na majumbani mwetu. Utamaduni wa asili unakariri sana kuwa tuwe na nidhamu shuleni na nyumbani mwetu. Ili watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, amani na upendo; lazima tuwe na bidii, ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo. Tukiwa viongozi ambao hawajishughulishi na maendeleo, basi tutabaki nyuma kama mkia siku zote. Bahati mbaya ni kwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo ama kwa utajiri wake. Kwa hivyo basi, tuchagueni viongozi ambao watatuletea ufanisi badala ya viongozi wanaotokana na nasaba au ya utajiri.

a) Dokeza mambo muhimu yaliyomo katika aya ya kwanza. (Maneno 65 – 70)
b) Fupisha aya ya mwisho kwa kuzingatia mambo muhimu yanayowapasa vijana kufanya
(Maneno (maneno 35 – 45)

**6.** ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:***

Usawa wa wanadamu upo kimaumbile – maumbile ya mtu kamwe hayatakosewa na yale ya mnyama wa mwituni. Lakini fikira, tabia, kimo, uwezo na mahitaji huwa tofauti kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Kwa mintarafu hii yapasa wakufunzi na wazazi kuwapa watoto wao widhaa mapema ili wachague kwa wakati unaofaa kazi watakayoifanya maishani.

Watoto wanapopelekwa chuoni, wazazi wao huukilia kuwasomesha hadi kiwango fulani cha masomo kisha wajitafutie kazi ambayo itawapa masurufu na pesa za shughuli zingine maishani.

Katika nchi yetu tangu tupate uhuru mtindo wa kutoa kazi umekuwa ni ule wa kuchukua watu waliofaulu mitihani ya viwango fulani na kuwapa kazi moja kwa moja. Mwenendo huu wa kuajiri watu kazi umeendelea muda mrefu lakini sasa yamkinika utasitishwa na njia mpya kufuatwa. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa nafasi za kazi zimekuwa finyu sana. Kabla na punde baada ya uhuru nafasi hizo zilipatikana kila mahali. Nyingi ya hizo ziliachwa wazi na wageni walioihama nchi hii tulipojitawala. Siku hizi wanafunzi wanaokomea darasa la saba, kidato cha pili na hata cha nne huwa

hawazioni ahadi za kupata kazi za madaraka fauka ya kazi yoyote. Wanaoiona tabasamu ya kazi mbele yao ni wale wanaotasawari masomoni wakifuata taaluma fulani.

Tatizo la kazi laeleweka vema kwa serikali na ni kwa ajili hii serikali imemtasulia kila mwananchi kuwa wakati wa kuania kazi za utanashati umetimiuka. Wakati uliopo ni wakati wa kujifunga vibwebwe kisaki na kuchapa kazi zile ambazo hadi sasa zafikiriwa kazi chafu na zisizofaa wasomi. Dhana kama hiyo ni ya kibwanyenye, na ubwanyenye hauji ila kwa sulubu. Usemapo kuna kazi nzuri na mbaya huwa unazusha maswali mengi. Utatakiwa ueleze kinaganaga kazi nzuri au mbaya kwa nini? Kazi huwa nzuri kwa upande wa tija au kwa upande wa wepesi wake? Kujibu maswali ya namna hii kutahitaji wekevu mwingi, waima mtesi ataonekana dufu.

Zipo kazi aina mbili. Ipo kazi ya kuajiriwa na ya kujiajiri. Kazi ya kujiajiri kwa kulinganishwa huonekana ngumu na yenye matatizo mengi mwanzoni. Lakini itakubalika pato lake ni kubwa zaidi ikishapata msingi imara. Msingi imara huwekwa kwa juhudi za mwanzoni zikiambatana na ujasiri. Mtu asiyejasiri kutenda tendo lolote maishani ni sawa na yule asiyejua atokako na kule aendako; yuaishi kungozwa. Ardhi ni thawabu, tena thawabu tunu. Ukiwa na kipande cha ardhi ifaayo kwa kilimo ufakiri ukikutawala ni wewe mwenyewe kupenda: la sivyo ufa umo ubongoni unaohitaji bwana mganga

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya ya kwanza na ya pili. maneno 60-70)

(b) Kwa kuzingatia aya mbili za mwisho. Eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi. (maneno (50-60)

7. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ufupishe taarifa hii kulingana na maswali yanayofuata:-***

Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, tumeshuhudia mabadiliko na maendeleo makubwa kuhusu vyombo vya habari nchini Kenya. Hapo awali, redio ndicho chombo cha habari cha kipekee kilichotamalaki kote nchini. Familia nyingi ziliweza kumiliki chombo hiki. Runinga ilikuwa miliki ya wachache, hasa mabwenyenye. Sasa hivi, hata akina yahe nchini na mashambani wanamiliki chombo hiki.

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasilianao kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundisha. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkem kwa mtu wa kila rika. Hali kadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji ya kufundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemichemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo wa vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia , kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanayowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa wanafamilia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii ukilinganisha na

vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa na kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalan, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya madawa ya kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaoutumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya waelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

**<u>Maswali</u>**

(a) Ukitumia maneno 50-60, fupisha manufaa ya runinga

(b) Fupisha hasara za runinga ukitumia maneno 70-80

**8.** ***Soma taarifa kisha fupisha kwa mujibu wa maswali yafuatayo.***

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kutoka kwa mtu yeyote yule aliye hai. Uwezo huu wa kukumbuka ni mojawapo ya shughuli changamano za ubongo. Ubongo wa mwanadamu hutekeleza shughuli hii kwa namna tatu. Kwanza ubongo hunasa jambo kisha huliihifadhi. Baadaye huanzisha mfumo wa kutoa kilicho hifadhiwa. Ubongo ukiathirika kwa namna yeyote katika moja wapo ya njia hizi, basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminika kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine, wataalamu wa maswala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa. Uimarishaji huu huhitajika mikakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka. Vyakula kama hivi ni mboga, nyama (hasa maini), bidhaaa za soya, matunda, maziwa, ,bidhaa za ngano, samaki, pamoja na mayai. Vyakula vingine muhimu katika ustawishaji huu ni vile vyenye madini ya chuma. Madini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi. Vyakula ambavyo vina madina haya ni mboga za kijani, mawele, ndengu, soya, matunda kama maembe, ufuta (simsim) pamoja na nyama, hasa maini na mayai.

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati awe macho au amelala. Utendaji kazi wake huendeshwa na glukosi mwilini. Kwa hivyo, vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa. Hata hivyo, lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili una kiwango cha sukari kisicho hatarisha maisha. Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikotini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni muhimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa jina na kile kinacholengwa.

Woga na kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati. Ni kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mtihani au mahojiano. Lakini anapaswa kuwa makini. Woga huo usikiuke mpaka na kumvuruga kiakili. Vurugu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na pia namna ya kukitoa.

Halikadhalika, mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu. Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa na mazoezi ya kunyoosha viungo hustawisha ubongo na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo. Ni muhimu kuwa na taratibu ya kunyoosha viungo kila wakati. Fauka ya hayo, mazoezi ya kiakili, kama vile kusoma makala yanayovutia, kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo, vitenzi ndimi ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo kuyakumbuka mambo ni ya jamii iliyopiga hatua kimaendeleo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

**Maswali:**

a) Kwa maneno 60 – 65 fupisha mchango wa chakula katika uimarishaji wa uwezo wa kukumbuka.

b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno 80 – 90

9. ***Soma taarifa kisha fupisha kwa mujibu wa maswali yafuatayo.***

Faragha ni muhimu kwa binadamu kwani huwa ndio wakati ambapo mtu atakuwa akitulia pekee mahali na huku akijiuliza ni mema mangapi ameyatenda siku hiyo, maovu mangapi ameyafanya, na kama siku hiyo ilikuwa ya manufaa au la.

Si binadamu wote ambalo wanapendelea kutumia wakati wao wa faragha kwa kupiga domo, nyumbani, kustawisha mabustani yao ya maua au mimea, au hata kuchukua kitabu au magazeti ya kusoma na kujifunza. Watu kama hawa huwa na fikira na mawazo mbalimbali juu ya umuhimu wa thamani ya wakati wa faragha. Watu kama hao utawakuta wakikusanyika katika makundi kwa matarajio ya kujinufaisha kwa mapato fulani au kujiingiza katika upigaji wa kamari. Wengine hunufaika wakasifu mafanikio yao ya siku ya mkusanyiko na baadhi yao ambapo hufanya mhanga wa michezo hii huibuka huku wakilaani na kuapiza bahati zao mbaya.

Kuna kundi jingine ambao hustahabu vilabu vya usiku kwa kujiliwaza au kujitumbuiza ili wapate kujituliza mawazo yao, wakayatafuta makali na kileo. Mwanzo wa ushirika kama huu huwa mzuri, watu huongea na kutoleana mawaidha yenye muafaka kiungwana kabisa. Lakini mara tu baada ya kuyakata makali haya kwa muda hivi, washiriki wake hupumbazwa na huanza kuyakata matindi mithili ya komba mpaka kiasi cha kubwata maneno ovyo ovyo na hatimaye kupoteza mbali fahamu. Ndipo kuruka kwa akili na kuanza zahama zenye kuonyesha utoto badala ya utu uzima. Kadiri makali hayo yanavyosiliwa kwa kuiva kwake, ndivyo wafuasi na mashabiki wake huyatumia kwa wingi na hata kuyaabudu, huyaabufu; huyabugia bila kujali uzito.

Na iwapo ndio kwanza wapokee mabunda yao, hakuna la kutia kikomo tafrija hizo ila uzito wa matendo ya ubadhirifu hujitokeza baada ya kurudi nyumbani, kulala fofofo na wazindukanapo siku ya pili yake ndipo wagundue walivyo taabani.

Mtindo wa matumizi ya faragha hutokea tangu mwanzo wa mazingira ya mtu; hivyo tangu utoto wake; tabia njema na zipasazo huhitajiwa kufunzwa. Sehemu kubwa ya mafunzo haya muhimu hutokana na malezi ya nyumbani chini ya uongozi wa mama na baba. Kama wasemavyo wahenga, mtoto akuavyo ndivyo alivyolelewa. Na mama mtu awe nyoka, hapana budi kuwa mwanawe naye atainuka kustahabu unyoke" wa mama yake. Hivyo ni wajibu wa wazazi kujenga mazingira yanayofaa kwa vizazi vya kesho kwa kuelekezwa namna yake. Ingewezekana himizo kubwa lingesisitizwa katika marekebisho ya tabia za wazazi kuwezesha manufaa yake. Ingewezekana, himizo kubwa lingesisitizwa katika marekebisho ya tabia za wazazi kuwezesha watoto kuiga mtindo au mitindo ya maisha yanayofaa. Kielezo chema ni kuwa na mzazi mwenye tabia njema kwa mtoto wake, rafiki zake na kwa jamii yake.

(a) Ni nini umuhimu wa faragha kwa binadamu kwa mujibu wa aya ya kwanza?(maneno 20)

(b) Eleza jinsi watu wengine wanavyoharibu wakati wao wa faragha kwamambo ya upotovu kwa kurejelea aya ya pili na ya tatu (maneno 30) (al. 5 al. 1ya utiriko)

(c) Eleza mchango wa mzazi kwa mwanwe kuhusu matumizi bora ya wakati wa faragha.

Zingatia aya ya mwisho

**10.** ***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kulingana na maagizo***

Imesemwa na kurudiwa tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umaskini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya wakenya milioni kumi wamo katika hatari ya kufa njaa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuatia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo. Imesahaulika kuwa karibu asilimia sabini na tano ya wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa wananchi na pia huletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mauzo ya mazao katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa maswala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linalotokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja.

Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia sabini na tano ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idadi hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo. Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo haya umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya uchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia kilimo ili kumaliza njaa na umaskini. Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kuhusu mihimili ya zaraa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga, ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kufadhili kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo. Bila hilo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yaliyostawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu ya njaa.

(a) Fupisha aya mbili za mwanzo (maneno 50 -55)

b) Bila kubadili maana, fupisha aya mbili za mwisho (Maneno 55-60)

Utiririko ni alama 3

**11.** ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Kwa hali nyingine , tunaweza kusema kuwa uchafuzi wa mazingira ni uharibifu wa vile vitu vinavyowazunguka binadamu na wanyama maishani mwao. Kuna uchafuzi wa aina mbalimbali na kila uchafuzi humhusu binadamu kwa njia fulani.

Maendeleo ya viwanda duniani ni sababu mojawapo ya uchafuzi wa hewa. Mitambo katika karakana huwa inatoa moshi mwingi wakati bidhaa zinapotengenezwa. Moshi husambaa eneo kubwa na kuchanganyika na hewa inayovutwa na binadamu. Uchafu hutupwa ovyo ovyo na kuwa hatari kwa afya ya binadamu. Maji machafu huweza kutiririkia mtoni, maziwani na hata baharini. Yale yanayotiririka mitoni na maziwani huchafua maji ambayo hutumiwa na watu wa eneo hilo kwa kunywa, kupika na kunywesha mifugo wao. Yale yanayotiririka baharini huwa ni hatari kwa samaki wanaotegemewa na binadamu kuwa kitoweo muruwa.

Ongezeko la watu pia ni hali nyingine ya uchafuzi wa mazingira. Halaiki ya watu hufanya uharibifu wa misitu ya asili. Hii ni kwa sababu ya kutaka kuongeza ekari za mashamba. Hili husababisha mmomonyoko wa udongo ; hivyo basi kuiacha ardhi bila rutuba yoyote. Katika hali hii, kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa nchi nyingi duniani huzoroteshwa. ''Maisha ya binadamu

hutegemea kilimo kwa kila hali kwa hivyo kilimo kinapozoroteka hata uchumi nao huathirika. Kila uchao tunasikia kwamba nchi fulani imekabiliwa na njaa.

Ufugaji wa wanyama wengi bila mpango maalum pia huharibu mazingira ya asili kama nyasi na vichaka. Watu wengi hufuga ng'ombe, mbuzi na kondoo. Kwa kuwa hawana mahali maalum pa kuwalisha, huzunguka nao huku na huko kutafuta nyasi na majani ya kuwalisha. Wanyama wanaotangishwatangishwa namna hiyo humaliza majani na nyasi zote na kuacha ardhi tupu ambayo hatimaye huyabisika kwa jua. Ardhi ya namna hii haishiki maji mvua inyeshapo. Nchi iliyoneemeka huweza kuwa jangwa lililo na chungu ya mchanga.

Watu wanapoongezeka huko mashambani huwabidi wakate misitu ili waanzishe maskani mapyapamoja na mashamba yao. Miti hukatwa bila hadhari na mabiwi ya matawi pamoja na majani huchomwa moto. Jambo la kusikitisha ni kwamba miti hiyo inapokatwa hakuna mingine inayopandwa kuchukua mahali pake.

Mahitaji ya binadamu ya kuendeleza njia za mawasiliano pia huzusha balaa nyingine. Barabara zinazidi kuongezeka na pia watu wanaozidi kuongezeka pamoja na mazao yao. Kwanza, barabara zinapotengenezwa misitu hukatwa mahali zinapopitia. Pili, wingi wa magari huzidi na baadhi ya hayo hutoa moshi unaoharibu hewa.

Njia kadha wa kadha za kuzuia uharibifu wa mazingira zimependekezwa. Ingawa suluhisho timamuhalijafikiwa, Serikali nyingi duniani zimo katika harakati za kutafuta suluhisho la uchafuzi huo.

Njia mojawapo ni kukomesha ujenzi wa viwanda katika miji mikuu na mahali palipo na watu wengi.Wenye viwanda pia wanahimizwa kufikiria jinsi ya kutupa takataka na maji machafu bila kudhuru afya ya binadamu.

Watu wakizingatia suala la upangaji wa uzazi na kuwa na familia ndogo ndogo, idadi ya watu haitaongezeka kwa kasi kwa hivyo itakuwa hakuna haja ya kuanzisha makao mapya mara kwa mara.

Serikali nyingi zimechukua jukumu la kuwaelimisha raia juu ya madhara yanayotokana na uharibifuwa mazingira. Raia wanahimizwa kupanda miti kwa wingi.

Jitihada zinazofanywa kuzuia uchafuzi wa mazingira hukumbana na matatizo. Tatizo kubwa ni fedha za kuendeleza miradi inayopendekezwa. Shida nyingine ni kwamba juhudi zingine huwa zinamwingilia binadamu na mali yake.

**<u>Maswali.</u>**

(a) Fupisha aya za kwanza sita za taarifa uliyosoma (maneno 50-60)

(b) Fupisha aya za mwisho tano kwa maneno 40-45

12. ***<u>Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali</u>***

Vijana wa siku hizi hujifikiria kuwa wao ni bora kuliko wazee wao. Wao hujifikiria kuwa wameelimika zaidi, wana busara zaidi, wanauelewa ulimwengu vizuri zaidi na wanaweza kujiamulia hatima yao bila uongozi wa wazazi wao. Wazee kwa upande wao, hawakubali kabisa madai ya aina hiyo. Kwao ni maasi tu. Wanachojua wazee kwa hakika ni kuwa vijana wa siku hizi hawaajibiki kwa lolote, wamedekezwa mno na wanapenda sana nafsi zao. Kwa sababu hiyo, vijana wanahitaji uongozi na ushauri wa wazeee.

Je, kuishi kwingi ni kuona mengi? Ingawa wazee wanafikiria wanajua mengi kwa sababu ya umri wao, vijana hupenda sana kukosoa fikira za wazee wao. Hawakubali imani na itikadi za wazee wao. Kwa mfano; vijana hupendelea mitindo ya mywele ambayo wazee wao hufikiria kuwa kichaa tu.

Wazee husifiwa sana enzi zao. Husifia jinsi walivyolelewa kwa kuchapwa na kufanyishwa kazi zinazohitaji uvumilivu mkubwa kama vile kuchanja kuni, kufyeka misitu, kutayarisha mashamba, kuwinda na kadhalika. Kwa sababu ya malezi hayo, wazee husema wao walirithi nidhamu nzuri na ushujaa. Vijabna kwa upande wao hawaoni chochote cha kujivunia katika zama za wazee wao; wao hufikiria kuwa wazee wao walilelewa kwa ukatili kwa sababu zama zao zilikuwa enzi za giza, kabla ya majilio ya uungwana na ustaarabu wa kisasa.

Wazee husifia kuwakumbusha vijana ule msemo mashuhuri wa wahenga usemao kuwa 'mwacha mila ni mtumwa.' Kwa maoni ya wazee, vijana wengi wamekuwa watumwa kwa sababu

wao huonyesha kwa vitendo kuwa hawadhamini desturi za wazee wao. Ka mfano; vijana hawafuati miiko ya jadi, hawapendi kuhudhuria sherehe za kienyeji, kwa mfano sherehe za kutoa makafara. Vijana pia hawapendi ngoma za kitamaduni, na isitoshe vijana hawazionei fahari koo zao. Vijana hawakubali kuwa wao ni watumwa wa mtu yeyote. Mila wanazosifia wazeee wao si vitu vyenye umuhimu wowote kwa vijana. Kwa mfano; baadhi ya miiko ni kisayansi. Kuhusu ukoo, si vijana wengi wanaona umuhimu wake. Ukoo na kabila zilikuwa muhimu zamani wakati ambapo kulikuwa hakuna serikali, bima na hata kazi ya mtu binafsi. Mambo haya sasa ni kama masalia ya zamani ambayo yamepitwa na wakati.

Je, vijana hupenda sana burudani na anasa tu kama wanavyodai wazee! Wazee wengi hufikiria kuwa vijana hupoteza muda wao mwingi kujitafutia anasa na burudani kwa mfano vijana wengi hurandaranda barabarani au mitaani wakisingizia kupunga hewa. Wengine huenda sinema na kuhudhuria dansi na karamu zisizo na manufaa. Vijana kwa upande wao hawaoni kinachowawasha wazee wao; pilipili wasioila yawashia nini?

1. Katika makala haya wazee wana malalamiko yapi kuhusu vijana? (maneno 50-60)
2. Msemo unaosema "Mwacha mila ni mtumwa" unathibitishwa vipi katika maoni ya wazee katika makala haya? (maneno 15- 25)

13. ***<u>Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali</u>***

Uchumi wa soko huria ni hali ya kiuchumi ambapo itokeapo amali, shughuli na harakati zote za kiuchumi ghairi ya zile ambazo ni za lazima kwa serikali au dola kama ulinzi, sheria na mpangilio wa jamii huwa huria kwa watu binafsi. Msingi wa soko huria, sifa kuu ya utandawazi, ni kuibua na kudumisha mazingira na hali zinazochochea na kumruhusu mtu yeyote kuongozwa na hawaa, au matamanio ya kibiashara anayoyaona sawa pasi na hofu ya kuingilia na udhibiti wa serikali.

Mazingira hayo yanawapa watu satua ya kufanya maamuzi kuhusu hatima yao ya kiuchumi, uamuzi kuhusu suala la ajira yao, matumizi ya mtaji kipato na harija zake, na uwekezaji mzima. Suala mojawapo linaloibuka kuhusiana na mfano wa soko huria ni kuweka mipaka bainifu na wazi baina ya amali na shughuli zinazohusishwa na serikali na zile ambazo huachwa huria kwa watu. Kwa mfano, inaaminiwa kuwa haki ya kuishi na kulindwa dhidi ya shambulizi, liwe la kijambazi au la kigaidi, ni ya kimsingi ambayo haiwezi kuhusishwa na uwezo wa kiuchumi wa mtu binafsi. Aidha huduma za kimsingi za afya nazo zinaingia katika kumbo hili. Ikiwa huduma hizi zitaachwa huria pana uwezekano mkubwa kuwa zitaishia kuwa istihaki ya wenye mtaji na kipato cha juu tu.

Licha ya kuwepo kwa sheria au kanuni huria kutoka nyanja maalum, hutokea hali ambapo adhibiti wa kiserikali ni lazima. Hii hutokea pale ambapo ipo haja ya kuyalinda mazingira hasa kutokana na uchafuzi wa viwanda au tasnia. Aidha udhibiti huo ni lazima pale ambapo haki za watu wengine zinahusika: yaani ikiwa uhuru wa hata mtu mmoja unaadhirika kutokana na sera hizo pana haja ya kuingilia ili kuisawazisha hali yenyewe.

(a) Andika kwa muhtasari maana ya uchumi wa soko huria kulingana na taarifa hii.
(maneno 25-30) (al. 5, 1mtiririko)
(b) Eleza mawazo makuu yanayojitokeza katika aya ya pili na ya tatu.
(maneno 70-75) (al. 10,3 za mtiririko)

**14.** **<u>WAJIBU</u>**

Sisi vijana ni wa taifa. Hatuna budi kutumikia umma kwa moyo wetu wote.Hakuna haja ya kulaza damu ikiwa taifa linatuhitaji. Ni lazima tuwe shupavu kwa mambo yote. Tuwe wenye busara, adabu njema na ari ya kutenda kazi kwa moyo wa utu. Ni muhimu kabisa kulinda, kutumikia na kuendeleza taifa hili changa katika mbinu zake na mipango yake yote kuhusu zaraa, elimu, uchumi, ulinzi na mipango yote ya maendeleo ya ustawi wa nchi na jamii. Inatupasa tuelewe ujamaa wetu na jinsi ya kupambana na ubepari, ukabila, ukupe, unyonyaji na ukoloni mamboleo. Hii itaondoa kabisa jasho letu. Inatubidi sisi vijana tujifunze jinsi na namna ya kuwa watu bora.

Elimu tuipatayo kutoka nyumbani, shuleni na katika jamii, lazima igeuze fikira zetu. Elimu hiyo lazima tuitumie ili itupatie uwezo wa kuelewa mema na mabaya maishani mwetu. Ni bora tujue

wajibu wetu katika kufikiri, kusema na hata kutenda kufuatana na wajibu huo kwa mioyo na dhamiri safi. Tuwe vielezo kwa wengine. Hasa tujitayarishe kuwa wazazi na viongozi bora wa kesho. Mno mno tuwe wazalendo na raia wema wa taifa hili changa. Tuhimize na kuendeleza utamaduni wetu wa lugha yetu ya taifa. Hatimaye tutambue usawa wa kila binadamu, popote alipo bila kujali taifa, kabila, rangi na hata dhehebu yake.

Tujifunze kujishutumu. Pia tukubali kusahihishwa makosa yetu na watu wengine. Hasa tuwe nguzo, kinga na ngao ya nchi yetu inapopigwa adharusi.

Acha nirudie kusema tena kuwa ni shabaha yetu sisi vijana kuwa na nidhamu njema. Nidhamu njema ni chanzo cha asili cha siha ya ujamaa na kujitegemea. Kwa hivyo, uongozi bora na bidii, ushirikiano mzuri na kujishughulisha. Uchaguzi bora wa viongozi na mifano mizuri ni kurunzi ya maendeleo ya ustawi wetu.

(i) Ni nguzo zipi ambazo kifungu hiki kimezipa kipaombele kwamba zitasimamisha ustawi na maendeleo ya nchi kutokana na vijana? Jadili kwa maneno thelathini

(ii) Vijana wameshauriwa wafanye mambo mengi mema. Jadili kinyume cha ushauri huu ukitumia maneno yako mwenyewe

# <u>Matumizi ya lugha</u>

1. (a) **Badilisha sentensi ifuatayo iwe mazoea kwa kutumia kirejeshi** "**O**"

Mtoto anayelia huchapwa

(b) **Andika kinyume**

Wavulana watatu wanaingia darasani kwa haraka.

(c) **Andika sentensi tatu ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii:-**

Kule ndimo alipoingia

(d) **Taja aina za vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi iuatayo**

Mama <u>amewahi</u> <u>kupika</u> jikoni

(e) **Eleza maana ya misemo ifuatayo** :-

(i) Giza la ukata…

(ii) Meza mate machungu

(f) **Unda vitenzi kutokana na :-**

(i) Mkufunzi

(ii) Maeneo

(g) **Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, taja aina za sentensi za kiswahili**

(h) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vishale**

Mwalimu huyu mzuri anafundisha darasani.

(i) **Eleza maana mbili za sentensi :-**

Mama alimlimia mwanawe shamba

(j) **Akifisha sentensi ifuatayo:-**

ah huu ndio upuuzi aliotuitia mmoja wao akaropoka.

(k) **Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano**

(l) **Andika sentensi ifuatayo katika msemo halisi :-**

Mshtakiwa alidai kwamba alikuwa ameonewa kwa kuwa hakuwa ameshiriki ulevi kutoka mwaka uliokuwa umetangulia.

(m) **Pambanua viungo vya kisarufi katika kitenzi kifuatacho**

Tuliwalimia

(n) **Andika upya sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo:**

Mizizi ya mibaruti hii iliwaponya watu ambao walikuwa na shida kama hii yenu (**kanusha kwa umoja**)

(o) **Tunga sentensi ukitumia neno "Vile" kama:**

(i) Kiwakilishi
(ii) Kivumishi
(iii) Kielezi

(p) **Bainisha matumizi viambishi "ku" na "Ji" katika sentensi zifuatazo**:-

(i) Mwanafunzi hu<u>ku</u>soma kwa bidii
(ii) Ata<u>ku</u>piga
(iii) Ame<u>ji</u>kata
(iv) Mcheza<u>ji</u> huyu ni hodari

(q) **Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa huku ukikanusha**

Kijibwa changu ni kikali sana

2. (a) **Jaza mapengo**:-

| **Kutenda** | **Kutendesha** |
|---|---|
| (i) Chota | |
| (ii) Lewa | |

(b) **Taja sauti moja ya;**

(i) King'ong'o

(ii) Kiyeyusho

(c) **Tumia neno "*shujaa*" katika sentensi kama**:-

(i) Kivumishi

(ii) Kielezi...

(d) **Tambua vitenzi katika sentensi hii kwa kuvipigia mistari:-**
Sisi tulikwisha kutambua alikuwa na nia mbaya. Yeye ndiye mwizi .

(e) **Andika wingi wa sentensi hii katika hali ya ukubwa**:-
Kichinjio hiki kilikarabatiwa kwa pesa nyingi

(f) **Eleza maana zinazojitokeza katika vifungu vifuatavyo**:-
(i) Jambazi kutoka dukani liliiba.
(ii) Liliiba jambazi kutoka dukani.
(iii) Kutoka dukani jambazi liliiba.
(iv) Jambazi liliiba kutoka dukani.

(g) **Jaza neno ambalo ni kinyume cha lile lililopigwa mstari katika sentensi:-**
(i) Vile vitu **ulivyovichanganya** itakubidi
(ii) Bomba hili l**imeziba** mwite fundi aweze

(h) **Unganisha sentensi hii kwa kutumia *'O'* rejeshi :-**
Wavu umekatika. Wavu ni wao

(i) **Eleza matumizi mawili ya "*ka*" na utunge sentensi kwa kila mojawapo**

(j) **Yakinisha sentensi hii**:
Sijafahamu kwa nini hawamkaribishi mpwa wao.

(k) **Andika katika usemi halisi:-**
Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo

(l) **Akifisha sentensi ifuatayo**:-
Sijaona kitabu kizuri kama mayai waziri wa maradhi, utaniazima siku ngapi bashiri alimwuliza rita

(m) **Changnanua kwa njia ya mishale**
Mama anapika na baba akisoma gazeti

(n) **Tunga sentensi moja na uonyeshe kwa mstari**;
(i) Shamirisho kipozi
(ii) Shamirisho kitondo
(iii) Shamirisho ala/kitumizi

(o) **Tungia vitenzi vifuatavyo sentensi katika hali zilizobanwa**:-
(i) Fa(**mazoea**)
(ii) La**(kutendeka**)
(iii) Pa (**kutendea**)

(p) **Tambulisha kishazi tegemezi na kishazi huru**
Wanafunzi walifoanya vyema walituzwa jana

(q) **Pambanua viambishi mbalimbali katika sentensi ifuatayo**
Waliwapendezea

3. a) **Onyesha viwakilishi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani:-**
i) Unamjua vyema kweli?
(ii) Hicho wanachokitaka hakipo

(b) **Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi**:-
(i) Minghairi ya
(ii) Wala

(c) **Yakinisha sentensi ifuatayo**:-
Chakula hakipikiki vizuri

(d) **Jibu kulingana na maagizo kwenye mabano:-**
(i) Hatujui ambako alitorokea (**tumia 'O' rejeshi**)
(ii) Angekuwa na pete, angekupatia (**ibadilishe katika wingi kisha uikanishe**)

(e) **Bainisha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo:-**
Maksuudi alimjengea Tamima Kasri kwa matofali mazuri

(f) **Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale/mistari:-**
Watoto wote wameamka mapema na wazazi wanatayarisha staftahi

(g) **Unda nomino moja moja kwa kila kitenzi**

Shuku
Vumilia
shona
lia

(h) **Eleza maana ya '<u>jinsi</u>' kama inavyojitokeza katika sentensi zifuatazo**

(i) Naomba unionyeshe jinsi ya kuendesha gari
(ii) Wakenya hawapendezwi na jinsi viongozi wanavyoendeleza ufisadi

(i) **Bainisha aina za nomino zilizopigiwa mistari katika sentensi hii:-**

**<u>Uhodari</u>** wa **<u>wanariadha</u>** wa **<u>Kenya</u>** unahitajika kote duniani

(j) **Tunga sentensi ukitumia mzizi – choyo kama** :-

(i) nomino
(ii) Kivumishi
(iii) Kiwakilishi

(k) **Eleza matumizi <u>mawili</u> ya kila mojawapo wa alama za uakifishaji zifuatazo**:-

(i) msitari
(ii) Parandesi

(l) **Geuza zentensi zifuatazo katika kauli kwenye mabano**:-

(i) Fundi ameharibu saa (**kutendea)**
(ii) Umemwona mgeni? (**kutendewa**)

(m) **Andika kwa udogo:-**

Gari la Mzee Maritu limegonga ng'ombe wa jirani wake

4. (a) ***Andika sifa bainifu za sauti***

(i) e:-
(ii) n:-

(b) ***Eleza maana ya :-***

(i) Kiimbo:.
(ii) Shadda…

(c) ***Tunga sentensi moja moja kudhihirisha ngeli zifuatazo***:-

(i) U-U
(ii) Pokomo /Pa-ku-mu

(d) ***Unda kitenzi kimoja kutokana na nomino*** '**Mtubia**"

(c) Eleza matumizi mawili ya kiambishi '***ku***'

(f) Tunga sentensi ya maneno manne ambayo ina sehemu zifuatazo. Kielezi cha namna, kivumishi,kitenzi na jina

(g) ***Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi***:-

Ng'ombe aliyeletwa juzi ameuzwa leo jioni.

(h) ***Onyesha matumizi mawili mawili ya alama zifuatazo:-***

(a) Alama ya mshangao
(b) Mshazari

(i) **Tunga sentensi sahihi ukitumia –*wa*- katika kauli ya kutendeana**

(j) ***Andika udogo wa sentensi:-***

Ndama wa ng'ombe yule ameuzwa.

(k) ***Onyesha tofauti ya vitate vifuatavyo kwakuvitungia sentensi***

(i) Dhamani
(ii) Thamani

(l) ***Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi***

Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari

(m) ***Ainisha shamirisho /yambwa katika sentensi ifuatayo***:-

Mchezaji alimpigia mwenzake mpira kwa mguu wa kushoto.

(n) Huku ukitumia mifano mwafaka, eleza tofauti ya sentensi sahili na ambatano

(o) ***Onyesha aina za viambishi katika sentensi hii***:

Nitajisomea

(p) ***Andika katika usemi wa taarifa:-***

Tutaanza mashindano kesho, Mwalimu alimwambia mwanafunzi.

(q) ***Eleza maana mbili ya sentensi***:-

Tumetengeneza barabara

(e) ***Tumia mifano mwafaka kueleza aina za mofimu***

5. a) Unda nomino za/lm,k, dhahania kutokana na maneno yafuatayo :-

i) Kwea .

ii) Himarisha …

b) Huku ukitoa mifano eleza miundo mitatu ya silabi za Kiswahili

c) Tunga sentensi ukitumia kinyume cha kitenzi: 'umba'

d) Andika katika

Meza ii hii ndiyo aliyotumia kulia

e) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendewa

i) cha …

ii) nywa

f) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo:

atakuajiri

g) Sisi tunajua sheria ingawa tu wafisadi

Anza: Japo………….

h) Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo:-

i) Wanafunzi wote wameingia darasani

ii) Jaribu kujitahidi kisabuni usianguke mtihani

i) **Changanua sentensi ifuatayo ukitumia njia ya matawi**:-

Amekuja kuwatembelea manusura waliopata ajali ya ndege

j) Taja sifa mbalimbali za sauti zifuatazo:

**/Z/**

**/K/**

k) Huku ukitumia mifano ya sentensi eleza matumizi **mawili** ya kiambishi, **'ji'** l)

**Andika udogo wa:**

Magari yote yaliyobakia yatauzwa na mzee yule mwembamba

m**) Sahihisha:**

i) Kila mwanafunzi alipewa ndazi na mayai moja

ii) Nipee huo mkoba nitoemo vitabu zangu

n) **Tumia – 'ako' katika sentensi kama**:

i) Kivumishi

ii) Kiwakilishi

iii) Kitenzi

o) Bainisha aina **mbili** za vishazi katika sentensi hii :-

Shamba lile kubwa litauzwa kesho

p) **Andika katika usemi wa taarifa** :

"Karibu Rahma, tafadhali kaa," Musa akasema . Ahsante, je, habari za hapa?' Rahma aliuliza

q) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi tofauti ya neno: '**somo'**

**6.** (a) Taja sauti **mbili** ambazo hutamkwa nyuma ya ulimi kati ya hizi

/h/,/o/,/y/,/u/,/kh/,/g/,

(b) Ng'oa kisiki hiki haraka askari akaamrisha mahabusu

(**Andika kwa msemo halisi**)

(c) **Badili sentensi zifuatazo katika kauli iliyoonyeshwa kwenye mabano**

(i) Si vizuri mwanafunzi kumwibia mwenzake pesa (**Kutendeana**)

(ii) Mpishi aliharibu mchuzi huu kwa kuongeza chumvi nyingi. (**tendeka**)

(d) **Bainisha matumizi ya "po" katika sentensi ifuatayo**:-

Alipowasili alionyeshwa walipo.

(e) **Andika kwa usemi wa taarifa:-**
“Wasichana wakielimishwa wataweza kuwa bora kuliko wavulana,” Naibu wa Chansela wa chuo Kikuu aliwaambia mahafala.

(f) **Tunga sentensi ambayo ina aina za maneno uliyopewa:-**
N + V + V + T

(g) **Tumia ‘‘O’’ rejeshi ya kati**
Lisemwalo silo liwalo

(h) ‘Msipokuwa wenye bidii hamtayapata mafanikio maishani.’ Yakinisha katika umoja

(i) **Changanua kwa kutumia mishale**
‘Mimi sikumwona wala Mwenda hakumwona’

(j) **Tunga sentensi ukitumia maneno haya katika kinyume**.:-
(a) afikiana
(b) sifu

(k) **Unda nomino mbili mbili kutokana na vitenzi vifuatavyo:-**
(i) abudu
(ii) fisidi

(l) **Andika katika hali ya ukubwa**
Mwanamke huyu amezaa watoto wanne.

(m) **Bainisha matumizi ya maneno yaliyopigwa mstari**
(i) **Mbio** hizi hazitakufikisha mbali
(ii) Mwambie Abedi asifanye **mbio** kuhusu hiyo kazi.

(n) **Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi**
Msichana aliyeitwa alikuwa mkorofi

(o) **Eleza dhana zinazowakilishwa na viambishi awali katika sentensi zifuatazo:** -
(i) Aliitwa
(ii) Hakupata

(p) **Tunga sentensi mbili kubainisha maana tofauti ya maneno yafuatayo:-**
(i) Kuna
(ii) guna

(q) **Taja mianzo mitatu** tofauti ya ngeli ya **U-ZI**

(r) **Eleza maana ya semi hizi :**
(i) Kunja jamvi
(ii) Piga kambi

7. (a) ***Andika sentensi ifuatayo bila kutumia*** “**amba**”:-
(i) Jitu ambalo linatusumbua sharti liadhibiwe vikali
(ii) ***Weka sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea***:-
Mmea ambao unapandwa katika msimu wa masika unamea

(b) ***Badilisha sentensi hizi hadi usemi wa taarifa:-***
(i) “Nitarudi tu ikiwa mtakubali kuomba msamaha”. Juma alisema
(ii) “Elezeni vile mlivyokuja hapa na namna mtakavyokwenda.” Mwalimu mkuu alisema

***(c) Fuata maagizo uliyopewa baada ya kila sentensi ili kujibu maswali haya :***
(i) Aliogopa kumwangalia simba aliyekula mzoga. (Tumia neno ‘Ogofya’ bila ya kubadililsha ya sentensi:-)
(ii) Mti wa zambarau ni rahisi kukatwa ukiwa unatumia msumeno. (***Anza*** **Ni rahisi...**)

(d) **Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii** :-
Alimlilia mwanawe

(e) (i) **Kanusha sentensi hii:-**

Tungewalaki kama tungejua watakuja

(ii) **Sahihisha sentensi ifuatayo na uiweke katika wingi**:-

Ningalifanya kazi ningekuwa tajiri

(f) Tunga sentensi **nne** kuonyesha matumizi na maana nne za kijineno '**ki**'

(g) **Tumia kivumishi kilichoko kwenye mabano kukamilisha sentensi:-**

(i) Bibi yule alinunua gari ________________________(-pya)

(ii) Mti (-ingine) ________________________uliangushwa badala ya ule wa kwanza.

(h) **Unda majina mawili mawili kutoka vitenzi hivi na utumie katika sentensi ili kubainisha maana**

(i) Safiri

(ii) Zaa

(i) **Akifisha kifungu hiki**:-

Yohana na Emanueli walifunga safari wakielekea mashariki kusini na hatimaye magharibi walifikia huko novemba mwaka jana walipokuwa wakirudi walimkuta mwalimu mkuu njiani ambaye alishtuka kuwaona pale

(j) ***Geuza sentensi hii hadi udogo***:-

Nyoka yule mrefu alifukuzwa na watu wengi

(k) ***Andika upya sentensi hii kwa kuandika kinyume cha kila neno lilipigwa mstari***:-

Wifi **alipovaa** nguo na kusimama ajuza yule **alikaa**

(l) Sauti hizi ni za aina gani na hutamkwa wapi?

(i) **gh**

(ii) **j**

(m) Mahabusu walifyeka uwanja vizuri

**Andika sentensi hiyo upya ukimaliza kwa neno mahabusu**

**8.** (a) **Onyesha maneno yaliyokopwa toka lugha za kigeni na kuswahilishwa kwa kuyaongezea irabu** ***k.m. Bint (Kiarabu) – Binti***

Toa mifano minne

(b) *Andika sentensi ifuatayo kwa usemi halisi:*

Mwalimu alipoingia darasani aliuliza kitabu chake kilipokuwa.

(c) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi nafsi huru umoja

(d) **Kanusha sentensi hizi kwa wingi**:-

(i) Mtoto huenda shuleni kila siku

(ii) Mwalimu amemfunza mwanafunzi vizuri

(e) **Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo**

Wanafunzi waliandikiana barua

(f) **Ziandike sentensi hizi bila maneno yaliyopigiwa mstari:-**

(i) Mwanafunzi **ambaye** alituzwa ni wa shule yetu

(ii) Sikuziona nyuzi **ambazo** huzitengeneza ngoma **ambayo** huiona pale

(g) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vielelezo vya vishale:**

Kiarie ni mwanafunzi mtiifu

(h) **Bainisha ngeli za nomino hizi :-**

(i) Kisu

(ii) Nyavu

(iii) Chai

(i) **Ainisha viambishi katika neno lifuatalo** :-

Kilichokikata

(j) **Nyambua kitenzi 'oa' katika hali tatu zifuatazo: tendewa, tendwa, tendea**

(k) **Eleza matumizi manne ya nukta**

(l) **Onyesha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo**:

Kamau alimlimia mamake shamba kwa trekta

(m) **Unda nomino kutokana na vitenzi hivi**:-

(i) Chapa (ii) Goma

(n) **Tambua kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii :-**

Chakula ambacho ni muhimu, huweza kujenga au kobomoa mwili wako.

(o) **Sahihisha sentensi ifuatayo:**

Ukienda mle pao atakuweko

(p) **Andika sentensi ifuatayo katika udogo:**

Mbwa mdogo amekanyagwa na gari.

9. (a) **Andika katika usemi halisi**

Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo

(b) **Andika kwa umoja**

Uovu waliotuonyesha hautasahaulika

(c) Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo:

(i) Pamba

(ii) Bamba

(d) Sauti zifuatazo hutamkiwa wapi?

(i) /f/

(ii) /v/

(e) Onyesha matumizi **manne** ya kistari kifupi

(f) **Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo**

(i) Nafsi ya tatu umoja

(ii) Wakati uliopita

(iii) 'O' rejeshi

(iv) kitendwa

(v) mzizi

(vi) kiishio

(g) **Tambulisha aina za vitenzi vilivyotumika katika asentensi hizi**

(i) Kazi hii **<u>ni</u>** nzuri.

(ii) Mazingira **yamekuwa yakihifadhiwa.**

(h) Pigia mistari chini ya viwakilishi katika sentensi zifuatazo

(i) Ambaye ni mjinga hatafaa kwa shughuli hizi

(ii) Nani anaye huzunisha?

(i) Ngeli ya LI-YA hujumulisha nomino za vitu vya aina mbalimbali. Toa mifano **minne** ambayo ni tofauti na uelezee

(j) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo na ueleze ni shamirisho ya aina gani?

Wazazi wanalipia watoto karo kwa hundi;

(k) Neno **'tikiti'** hupatikana katika **ngeli mbili** tofauti. Taja ngeli hizo na utunge sentensi

(l) **Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale.**

Hakimu alimwadhibu kinyama.

(m) Nyambua vitenzi hivi kulingna na kauli ya kutendua na kutenda

| **Kutenda** | **Kutendua** | **Kutendama** |
|---|---|---|
| Ficha | | |
| Tanda | | |

(n) Ni nini maana ya neno kirai ?

**10 .** (a) Kati ya nomino za Kiswahili taja **ngeli mbili** ambazo nomino zake hazibadiliki katika umoja na katika wingi. Kisha utoe mfano mmoja kwa kila ngeli

(b) **Yakinisha:** Waumini wale hawaimbi wala hawaombi

c) **Andika kwa umoja**

Nguo zile uzionazo zilinunuliwa Ulaya

(d) Taja na kutolea mifano aina nne za silabi za Kiswahili

(e) **Unda nomino moja kutokana na nomino hizi**

(i) Mtu. (ii) Mhasibu..

(f) **Andika kwa ukubwa**

Kipaka hiki hakitosheki kwa maziwa haya kimezoea kipanya

(g) Onyesha shamirisho kipozi na shamirisho kidondo katika sentensi hii:-

Mama amempikia moto chakula kizuri

(h) **Tunga sentensi ya neno moja inayoonyesha sehemu zifuatazo**:-

(i) Kiambishi kikanushi nafsi
(ii) Kiambishi kiwakilishi cha hali timilifu
(iii) Kiambishi kiwakilishi cha kitendwa (nafsi)
(iv) Kauli
(v) Kiishio

(i) **Sahihisha sentensi hii kwa njia tatu tofauti**

Mtoto mwenye alicheza ameteguka

(j) **Andika visawe vya maneno haya**

(i) Rabsha..... (ii) Damu..

(k) Jaza mchoro ufuatao kwa irabu inayofaa

(i) (ii)

(v) (iii)

(iv
)

(l) Tunga sentensi ukitumia **'ni'** kama

(i) kitenzi (ii) kielezi

(m) Andika katika msemo halisi

Johana alisema kuwa angepata alama zote katika majaribu ya wiki iliyotangulia

(n) Tumia '**O'** Rejeshi ya mazoea katika sentensi ifuatayo;

Jembe ambalo lilinunuliwa limepotea

(o) Changanua ukitumia mtindo wa mishale

Mtoto anayelia sana ameadhibiwa leo asubuhi

(p) Onyesha matumizi mawili katika sentensi ya alama (**'**)

(q) Wafuatao wana ulemavu upi?

(i) Toinyo . (ii) Huntha ..

**11.** (a) Andika vinyume vya vitensi vilivyopigwa mistari

(i) **<u>Alikashifiwa</u>** kwa kazi aliyofanya
(ii) Kuimba **<u>kulifurahisha</u>** hadhira

(b) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi

(i) Abiria waliojeruhiwa sana walipelekwa hospitali haraka

(c)Eleza maana **mbilimbili** za sentensi zifuatazo ;

(i) Bibi yake amefika
(ii) Alimpigia mpira

(d) Kwa kutoa mifano, onyesha namna mbili vile kiambishi –j- hutumiwa

(e) irabu **a, i,** na **u** hutamkwa wapi kwenye ulimi?

(f) Kamilisha na kueleza maana ya methali hii

(i) Mfinyanzi -.......................................

**(g) Andika usemi huu kwa usemi wa taarifa**

"Kefule! Mtoto huyu ni kaidi kama kirongwe. Hamheshimu babake!" alisema mzee Kamau.

(h) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentenzi ifuatayo

(i) Darasa lililojengwa limefunguliwa rasmi
(ii) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo;

(j) Kanusha sentensi ifuatayo kwa udogo

(i)Mbuzi wake ana manyoya mengi na harufu kali

(k) Onyesha maana **mbili** ya neno taka (ala. 2)

**(l) Andika kwa umoja** (ala. 2)

(i) Tumewaondoleeni matatizo yenu, yafaa mtushukuru

(m) Eleza maana ya misemo:- (ala. 2)

(i) Fuga mtu –

(ii) Kuwa na faragha -

(n) Panga nomino hizi katika ngeli mwafaka (ala 2)

(i) Kipofu- .

(ii) Uyoga- .

(o) Bainisha viwakilishi katika sentenzi kisha useme ni vya aina gain. (alama

i) Mimi nitaondoka kesho

(ii) Huyo alichaguliwa na wengi

12. (a) Tumia kiulizi kifaacho kukamilisha maswali yafuatayo:

(i) Waashi wale wanaishi kwa

(ii) Mtoto alitaka majina…

(iii) Wanitania hivyo

(b) Tambua mzizi katika neno:

Tuliwalimia :

(c) Andika sentensi **tatu** ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii

Pale ndiko alimoingia

(d) (i) Nini maana ya yambwa (shamirisho)

(ii) Taja aina ya yambua iliyoipigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:

**Mama amempikia baba wali kwa sufuria**

(e) Neno "**mlango**" lina maana ya "uwazi wa kuingilia nyumba." Tunga sentensi **mbili** kubainisha matumizi mawili ya neno hili

(f) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya **"ndivyo**"

(g) Chai hiyo iliwavutia watahi **(*Anza* : Watahi…………..)** (al. 2)

(h) Tumia neno **"haraka**" katika sentensi kama: (al. 2)

(i) Nomino (ii) Kielezi

(i) Andika maana **mbil**i za sentensi:

(i) Nenda ukamwone mwenyewe, usiogope.

(j) Onyesha maana za '**ni**' zilizopigiwa mstari

Nihamrishe "**Tokeni darasani**"

(k) Atakapokuja atamletea mlinzi uta na upote

(l) Maneno hayo yako katika ngeli gani?

(i) Ridhaa (ii) Nanasi

(m)Andika mifano ya sauti zenye sifa zifuatazo:

(i) Kipasuo cha kaakaa laini (ii) Nazali ya ufizi

(n) Tumia neno "**ngali**" kutunga sentensi kuonyesha

(i) Kitenzi kisaidizi (ii) Kitenzi kishirikishi

(o) Tumia kirejeshi kuonyesha mazoea katika sentensi ifuatayo:

(i) Mtoto anayelia ni huyu (ii) Neno maana ya kiwakilishi?

(q) Tambulisha viwakilishi katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani?

1.Nani alikukasirisha?... 2. Huyu huwashinda wote

(r) Tunga sentensi **moja** itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano

13. (a) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi

(i) Kishirikishi kipungufu

(ii) Kikuu

(b) Akifisha

je, unaipenda hali ilivyo mwenzake alitaka kujua

(c) Eleza matumizi ya '**ka**' na '**hu'** katika sentensi zifuatazo.

(i) Nilienda kanisani nikamkuta, nikamwamkua, nikamwomba msamaha.

(ii) Baba hufika nyumbani usiku wa manane

(d) Yakinisha sentensi ifuatayo :
Mama hakutuchapa, hakutupa chakula wala maji

(e) Tofautisha kati ya sauti ghuna na sauti si ghuna huku ukitolea mifano miwili kwa kila aina

(f) Tunga sentensi mbili kutofautisha matumizi ya vitate hivi: Dua na tua

(g) **Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo wingi**
Njia nyembamba ni hatari kwa usafiri wa gari

(h) **Changanua sentensi ifuatayo ukitumia matawi**
Mzee ambaye hukuza pamba amefaidika sana

(i) **Ainisha mofimu zinazojitokeza katika kitenzi hiki**
Waliochekeshwa

(j) **Andika sentensi zifuatazo kulingana na kauli ulizopewa katika mabano**
(i) Ugonjwa wa saratani hufanya watu **wafe** polepole. (kauli ya kutendesha)
(ii) Mkulima **alisuka** kamba ndefu. (Kauli ya kutendata)

(k) **Tunga sentensi moja inayojumulisha sehemu hizi, Ala, kipozi, kitondo na chagizo**

(l) Neno kijana linaweza kutumiwa kama kivumishi au nomino, tunga sentensi kudhihirisha***U**
(i) Kivumishi
(ii) Nomino

(m) **Sahihisha sentensi zifuatazo**
(i) Mtoto ambaye aliyekuwa anacheza ameanguka.
(ii) Vitabu hizi ambazo zimesahihishwa ni za wanafunzi.

(n) Tunga sentensi mbili ukitumia vielezi vya namna mfanano na viigizi.

(o) Bainisha maneno yafuatayo yapo katika ngeli gani kisha tunga sentensi mwafaka:
(i) Manukato (ii) Uwati

(p) Eleza maana ya methali ifuatayo:
"Avunjaye nazi ni lazima aafaidi tui.

**14.** A) **Eleza maana mbili za:**
Mwanaida alikwenda sokoni peke yake.

B) **Akifisha sentensi hizi.**
i) Hodi hapana wenyewe nini Juma alimwaka nitarudi kesho.

C) **Andika maana ya methali ifuatayo.**
Achanikaye kwenye mpini hafi na njaa.

D) **Tumia "O" rejeshi katika sentensi hii.**
Mwanafunzi ambaye hudurusu ndiye hupita mtihani.

E) **Andika sentensi ifuatayo kwa kunyambua maneno yaliyo kwenye mabano kwa usahihi.**
Dhambi za mwanadamu zilim____________ (fa) Bwana Yesu.

F) **Eleza maana ya misemo ifuatayo.**
i) Teka bakunja.

G) **Taja maana ya maneno yaliyopigwa mistari**.
Tulipogawa mkate kila mtu alipata sehemu moja kwa nane tu kwani tulikuwa wanane

H) **Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maelezo.**
i) Sikusoma kwa bidii ndiposa sikufaulu katika mtihani ule.
(Anza: Ningalisoma …………………………………………)
ii) Anakuja (andika katika wakati ujao hali timilifu)

I) **Eleza maana ya neno chungu kama lilivyotumiwa katika sentensi zifuatazo.**
i) Chungu yule ni mkubwa.
ii) Chungu kile ni kikubwa.

J) **Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo kama vivumishi.**
i) Sote. i) Zote.

K) **Andika nomino mbili kutokana na kitenzi safari.**

L) **Tumia viunganishi mwafaka kuunganisha sentensi hizi ziwe sentensi moja.**
Alikimbia kwa nguvu zake zote. Alishindwa, kulikuwa na mtu mwenye mbio kumliko.

L) **Eleza maana ya matumizi ya "<u>ka</u>" katika sentensi ifuatayo**.
Aliingia ndani, akaoga, akala kisha akalala.

N) **Taja sauti mbili za ving'ong'o**

O) **Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.**
Juma ameinjika chungu mekoni.

P) **Andika sentensi ifuatayo katika wingi wa udogo.**
Mtu/ mchoyo hamfai mwingine kwa vyovyote vile.

Q) **Kanusha sentensi hii;-**
Ukionana naye mwambie aje anione.

R) **Eleza na udhibitishe kwa mfano, matumizi <u>mawili</u> ya tu**.

S) **Changanua sentensi ifuaatayo kwa kielelezo visandu**.
Mwanafunzi aliyeleta kitabu chake amepongezwa

T) **Bainisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo**
Soroveya atapima wanunuzi viwanja.

U) **Nomino zifuatazo ni za ngeli gani?**
i) Insi …  ii) Soksi

# Isimu Jamii

1. Saidi : Hallo............Hallo....Huyo ni Bw. Mohamed?
Mohamed : Ndio...uko wapi...
Saidi : Shuleni...sasa...ulinifikishia ujumbe?
Mohamed : La. Parade ilikuwa imehitimishwa
Saidi : Sina credit. Nipigie tafadhali.
Mohamed : Sina pia, nitatuma sms
Saidi : Iwe saa hii eh?
Mohamed : Baada ya dakika tano
Saidi : Good day
Mohamed : Welcome

(a) Taja na uthibitishe sifa zinazojitokeza katika mazungumzo haya
(b) Eleza sababu za wazungumzaji kutumiambinu zifuatazo katika mazungumzo yao
(i) Mdokezo
(ii) Lugha mseto

2 . Lugha ya kiswahili inakabiliwa na matatizo mengi sana. Yataje na kuyaeleza.

3. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata:-***
Uchunguzi uliofanywa umeonyesha kuwa anasumbuliwa na uto mwingi mwilini. Uto unaweza kudondoshwa kwa kufanya mazoezi, kupunguza ulaji wa vyakula vya wanga na hata protini. Protini iwapo nyingi mwilini hugeuzwa kuwa glukosi ambayo huhifadhiwa mwilini. Hii huwa msingi wa unene pia ambao unahatarisha afya. Jamaa yake aliyeaga dunia alikuwa mgonjwa wa bolisukari ambayo inaweza kurithishwa. Kimsingi, lazima awe na welewa bora kabisa wa lishe. Mwenzake naye aliathiriwa na **aflatoxins** zilikuwa kwenye chakula alichokula.

(a) Sajili hii inapatikana wapi? Kwa nini?
(b) Taja sifa zinazohusishwa na sajili yenyewe

4. Fafanua mikakati mitano inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa kiswahili nchini Kenya

5 (a) Ni mambo yapi yanayochangia kudidimia kwa Kiswahili nchini Kenya.
(b) Mambo haya yanaweza tatuliwa vipi?

6. a) Bainisha kwa kutoa mifano sifa **tano** za lugha ya vijana '**sheng'**
b) Fafanua changamoto **tano** zinazozuia maenezi ya haraka ya lugha ya Kiswahili

**7.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata:-***
Niaje wasee! Ma-holiday ndizo hizo tena. Najua ma-mission ni mingi! Lakini jo, mambo imebadilika ! Ni kubaya maze. Usifikirie kila kitu unaona ni reality, ukadhani ni gold ! Hiyo siyo real life maze ! Round hii maze ni ''Ku-chill!'' Usipige ma-stunts zingine zitakuachа uki-regret later! NI POA KU- CHILL au aje maze?

a) Bainisha rejista ya mazungumzo haya
b) Kwa kurejelea kifungu andika sifa za rejista hii.
c) Kwa nini watu hutumia lugha zaidi ya moja.
d) Orodhesha hatua tatu zinazoweza kuchukuliwa kusuluhisha matatizo yanayokumba Kiswahili nchini.

8. ***Soma mzungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali :***
**A** : Ohh, dada Naomi
**B** : Dada Ruth (anamsogea kwa bashasha wanakumbatiana). Ahh Mungu asifiwe!
**A**: Asifiwe sana

**B**: Ehh dadangu, miezi ...mingi...sijakuona
**A**: dada wee...Nilitumwa huko kusini ...Kuwahubiria watu injili (mtuo mdogo)singeweza kukata...
**B**: Ehh, usiwe kama Yona
**A**: Habari ya siku nyingi?
**B**; Nzuri Mungu bado ameendelea kunibariki
**A**: Amen!
**B**: Nimeendelea kuiona neema yake
**A**: Amen! Asifiwe Bwana
**B**: Halleluya
**A**: Ni Mungu wa miujiza!
**B** : Amen. Hata nami nimeona neema yake
Bado niko imara katika wokovu katika siku hizi za mwisho
**A** : Amen !
**B** : Ni Mungu wa ajabu kweli !
**A** : Nilikumbana na matatizo lakini nikategemea sala
Kama Paulo na sila… Na nikashinda (anatua). Sikuweza kumpa shetani nafasi…maana ameshindwa
**B** : Ameshindwa kabisa

**<u>Maswali</u>**:-
(i) Hii ni sajili ya wapi ? Fafanua
(ii) Taja na ueleze sifa za sajili hii
(iii) Taja na ueleze mambo **mawili** muhimu yaliyosaidia katika maenezi ya Kiswahili Afrika mashariki na kati

9. Bw. Mosuka : Mheshimiwa spika, naichukua fursa hii kuipinga hoja iliyowasilishwa na mbunge wa Mahira, mheshimiwa Kochaberi kuhusu suala la kuavya....
(a) Hii ni sajili gani?
(b) Eleza sifa za mazungumzo ya sajili hii

10. Eleza juhudi tano zinazotumika kukiendeleza Kiswahili

11.` (a) Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha wa maabadini
(b) Matumizi ya lugha yoyote ile huthibitiwa na mambo fulani. Fafanua **matano** kati ya hayo

12. **AZIZ** : Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways beba! 46 Adams mbao kenyatta, railways!
**SHIKU** : Namba nane ngapi?
**AZIZ** : Mbao ingia, blue.
**SHIKU** : Nina hashuu.
**AZIZ** : Blue Auntie.
**SHIKU** : Sina.
**AZIZ** **:** Ingia. 46 Adams mbao, kenyatta railways gari bebabeba.
**AHENDERA** : Mimi sinako shirini. Chukuako tu kumi.
**AZIZ** : Dinga inakunywanga petrol mzee.
**AHENDERA**: Kumi mingi.
**AZIZ** : Haaya ingia twende. Driver imeshon twende.

**<u>Maswali</u>**
(i) Eleza muktadha wa mazungumzo haya
(ii) Taja sifa **sita** za lugha iliyotumika katika mazungumzo haya

13. ***Kifuatacho ni kifungu kifupi cha mazungumzo. Kisome kisha ujibu maswali yaliyoulizwa:-***
Mzee Oluoch :....................................................................ni kweli hayo!

Mzee Mwenda : Ndio. Huyu mtoto wangu nimemsomesha mpaka akahitimu chuo kikuu na anafanya kazi ya uhasibu.

Mzee Oluoch : Na wangu amehitimu na sasa ana shahada ya uzamili. Yeye ni mhandisi mkuu. Chukua tu mbuzi hamsini na utukubalie kujenga uhusiano wa ukwe.

Mzee Mwenda : Je, mbuzi hao ni wa ‘mfuko’ au ni .......?

Mzee Oluoch : Kuna wa mfuko ......thelathini na hao wengine ishirini.

Mzee Mwenda : Basi lete hao ulio nao. Wengine hamsini watabaki deni. Utakuwa ukinilipa polepole. Idhini yangu nimetoa ili mipango iendelee.

(a) Mazungumzo ya aina hii hutokea katika muktadha wa aina gani?

(b) Eleza sifa **nane** za lugha inayotumika katika wa aina hii

# SEHEMU C (102/3 KISWAHILI
# KARATASI YA TATU
# {Ushairi, Fasihi}

## Ushairi

1. **SHAIRI 'A'.**

Umekata mti mtima
Umeangukia nyumba yako
Umeziba mto hasira
Nyumba yako sasa mafurikoni
Na utahama
Watoto Wakukimbia

Mbuzi kumkaribia chui
Alijigeuza Panya
Akalia kulikuwa na pala
Kichwani
Mchawi kutaka sana kutisha
Alijigeuza Simba
Akalia na risasi kichwani

Jongoo kutaka sana kukimbia
Aliomba miguu elfu
Akaachwa na nyoka

Hadija wapi sasa yatakwenda
Bwanako kumpa sumu ?
Hadija umeshika nyoka kwa mkia
Hadija umepitia nyuma ya punda

**SHAIRI 'B'**

Piteni jamani, Piteni haraka
Nendeni, nendeni huko mwendako
Mimi haraka, haraka sina
Mzigo wangu, mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuweka

Vijana kwa nini hampiti ?
Kwa nini mwanicheka kisogo ?
Mzigo niliobeba haupo.

Lakini umenipinda ngongo na
Nendako
Haya piteni ! Piteni haraka ! Heei !

Mwafikiri mwaniacha nyuma !

Njia ya maisha ni moja tu.
Huko mwendako ndiko nilikotoka Na
nilipofikia wengi wenu Hawatafika.

Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati
Lakini kama mungepita mbele
Na uso wangu kutazama
Ningewambia siti miaka Mingi.

(a) Haya ni mashairi ya aina gani ? Toa saabu
(b) Washairi hawa wawili wanalalamika. Yafafanue malalamishi yao
(c) Onyesha jinsi kinaya kinavyojitokeza katika tungo hizi mbili
(d) Ni vipi Hadija :-
    (i) Amekata mti mtima ?
    (ii) Amepita nyuma ya Punda
    (al.2)
(e) Toa mifano 2 ya uhuru wa mashairi kwa kurejelea mashairi haya
(f) Kwa kurejelea shairi '**B**' eleza maana ya:-
    (i) Mzigo
    (ii) Siri
    (iii) Kula nimekula
    (iv) Niko nyuma ya wakati

2. Sinisumbuwe akili, nakusihi e mwandani.
Afya yangu dhahili, mno nataka amani
Nawe umenikabili, nenende sipitalini Sisi
tokea **azali**, twende zetu mizumuni
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini
Kwa nguvu za kirijali, Mkuyati uamini Kaafuri
pia kali, dawa ya ndwele fulani
Nifuateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu akiwa hali, tumbo lina walakini,
Dawa yake ni subili, au zongo huanoni
Zabadili pia **sahali,** kwa maradhi yalo ndani
Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini
Daktari k'ona mwili, tanena kensa tumboni
Visu visitiwe makali, tayari kwa pirisheni
Ukatwe kama fagili, **tumbo nyangwe** na maini
Nifuateni sipitalini, na dawa ziko nyumbani?

Japo maradhi **dhalili**, kutenguliwa tegoni
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani
Wambiwa damu kaliti, ndugu msaidieni
Watu wakitaamali, kumbe ndiyo bunani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mizimu wakupa kweli, Wakueleze undani.
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu thamani
Utete huku wawili, wa manjano na kijani
Matunda pia asali, vitu vyae shamoni
Nifuateni sipati, na dawa zi langoni?

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka
(b) Mtunzi alikuwa na lengo gani alipotunga shairi hili
(c) Mbona mshairi hataki kwenda hospitalini
(d) Eleza umbo la shairi hili
(al. 6
(e) Kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika ushairi ?
(f) Andika maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye shairi :-
(i) Dhalili –..........................................................................................................................
(ii) Azali -.............................................................................................................................
(iii) Sahali -.........................................................................................................................
(iv) Tumbo nyanywe ............................................................................................................

3. **WAFULA KABILIANA NA KISU**

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tulichinja ili uwe mwanamme, Eewe
mpwa wangu, kisu kikali ajabu ! Iwapo
utatingiza kichwa, Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu, Simama
jiwe liwe juu,
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,

Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,

Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa,
Iwapo wewe ni mme, Kabiliana
na kisu kikali, Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri

**Maswali**

(a) Hili ni shairi la aina gani ? Thibitisha
(b) Ni nani anayeimba shairi hili na analiimba kwa nani ?
(c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume
(d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili
(e) Taja shughuli zozote **mbili** za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili
(f) Eleza kwa mifano, uhuru wa kishairi katika shairi hili
(g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili ?
(i) Mbari
(ii) Msununu
(iii) Ngariba
(iv) Uvundo

4. **HATIMA YANGU**

1. Mke wangu wameshanipoka Ndugu zangu, wamedai ububu
Wazazi kuzoea kunigombeza

2. Juzi mali lilimbikiza
Furaha lilitanda
Makanwa yalijaziwa
Hoi hoi ikawa desturi

3. Kilabu tulikwenda
Nyama tulichoma Mahali
tulizuru Tuliteremsha!

4. Leo mambo yamenigeuka Wao masahibu siwaoni
Matumbo yakaninguruma
Kama radi ya mvua

5. Nyumbani nimebaki pweke
Mke amenitoroka
Watoto wameparara
Skuli kugharamia
Imegeuka balaa belua

6. Ndipo nimeamua
Afadhali kitanzi badala ya balaa
Kumbe kupanga ndiyo maana
Maisha na waasia

(a) Eleza mambo muhimu yanayoelezwa katika shairi hili
(b) Fafanua sifa mbili za anayezungumza katika shairi
(c) Dondoa na ufafanue mbinu zozote mbili za lugha katika shairi hili
(d) Eleza maana ya:-
  (i) Ndugu zangu wamedai ububu
  (ii) Kumbe kupanga ndiyo maana

5. 1. Nitampa nani, sauti yangu ya dhati
Kwa kipimo gani, ingawa kiwakatiti
Amefanya nini, la kutetea umati
Kipimo ni kipi?

2. Yupi wa maani, asosita katikati
Alo na maoni, yasojua gatigati
Atazame chini, kwa kile ule wakati
Kipimo ni kipi?

3. Alo mzalendo, atambuaye shuruti
Asiye mafundo, asojua mangiriti
Anoshika pendo, hata katika mauti
Kipimo ni kipi?

4. Kipimo ni kipi, changu mimi kudhibiti
Utu uko wapi, ni wapi unapoketi
Nje kwa mkwapi, au ndani kwa buheti
Kipimo ni kipi?

**Maswali**

a) Eleza umbo la shairi hili
b) Taja na ueleze jinsi mwandishi alivyotumia uhuru wa ushairi
c) Eleza ujumbe unaowasilishwa na mshairi
d) Andika ubeti wa **tatu** katika lugha ya nathari
e) Taja bahari **tatu** zinazojitokeza katika shairi na utoe sababu
f) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi hili

i) Katiti
ii) Gatigati
iii) Mangiriti

6. **<u>KIPI NIKITENDE?</u>**

. Tayari ni sarakani, niambie yote
johara, Mosi nimpe shukrani, kanizaa bira
zira,
Wapo haiko hisani, ningefaa kwa uparara**,** Kipi
takachokitenda, ni nene heko kwa mama?

. Miezi tisa tumboni, yote nina kajinyima,
Kanikopa uchunguni, safari ndefu kazima'
Kama kinda kiotani, kiniasa huyu mama' Kipi
takachokitenda, ninene heko mama ?

. Baba siku jana madadi, **<u>kawa vingaito mambo,</u>**
Kaolewa na asadi, kachalazwa kwa **<u>wimbombo</u>**,
Kaona – bali jadili, kuchao puani bombo,
Kipi takachokitenda, ninene heko mama?

. Kila kuchao zarani, kupalilia kondeni,
Kachanika mpinini, chungu povuka motoni,
Kaviyariya fingani, kinijali jikoni,
Kipi tukachokitenda , ninene heko mama?

. Wa siku hizi vijana, wakahujuru nyumbani,
Wengine wao jagina, kawa lofa mutaani, Hali
ukashiba nina, afikapo tu, "**<u>kongoni!"</u>** Kipi
takachokitenda, ninene heko mama?
. Nawe bwana siwe maya, vita hasha kiwa kombo,
Tena simfanye yaya, ya kikoa ndio mambo,
Simtende ya hizaya, siwe mwao kila jambo,
Kipi takachokitenda, ninene heko mama?

. Sasa jamvi nakuja, kisa nimesakarika,
Naomba niliyotaja, tatia manani kaka,
Nenayo yasiwe ngoja, ili nipokee baraka,
Mema nitamtendea, apate futahi pia.

**<u>Maswali</u>**
(a) Eleza umbo la shairi hili
(b) Kwa nini msanii amshukuru mamaye ?
(c) Ni kina nani wanaokashifiwa na msanii ? Kwa nini ?
(d) Onyesha tofauti katika ujumbe iliyoko katika beti nne za kwanza na mbili zinazofuata
(e) Toa majina mengine yenye maana sawa na haya yaliyotumiwa katika shairi hili :
(i) Mama
(ii) Dawati
(iii) Imara/thabiti
(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika kaika shairi:

(i) Kawa vangaito mambo
(ii) Wimbombo
(iii) Kongoni

7. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata**

**MWANAMKE**

1. Namwona yu shambani,
Na jembe mkononi,
Analima,
Mwanamama,
Mavuno si yake, Ni
ya mume wake.

2. Namwona viwandani,
Pia maofisini,
Yu kazini,
Hamkani,
Anabaguliwa,
Na anaonewa.

3. Namwona yu nyumbnai,
Mpishi wa jikoni,
Yaya yeye,
Dobi yeye, Hakuna
malipo, Likizo
haipo.

4. Namwona kitandani, Yu uchi **maungoni.**
Ni mrembo
Kama chombo,
Chenye ushawishi, **Mzima
utashi.**

5. Namwona mkekani,
Yuwamo uzazini,
Apumua,
Augua,
Kilio cha kite,
Cha mpiga pute.

6. Kwa nini mwanamke,
Ni yeye peke yake,
Heshimaye,
Haki anakosa,
**Kwa kweli ni kosa**

***(Muhammed Seif Khatib)***

7. (a) "**Shairi hili ni la kukatisha tamaa**". Fafanua dai hili kwa kutoa mifano **minne**
(b) Eleza umbo la shairi hili

(c) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari
(d) Taja tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi zima utoe mifano **miwili** ya jinsi ilivyotumika
(e) Onyesha mifano miwili ya ubabadume inayojitokeza katika shairi hili (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika shairi:
(i) mzima utashi
(ii) maungoni

8. **KIACHE KINACHONG'AA**

Katu siwe na harara, wala moyo kukupapa,
Usichukue hasira, na moyo kutapa-tapa,
Utaharibu na sura, mwishowe uende kapa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Mbeleye kina madhara, kile kinachokukukwepa,
Mbele yake ni hasara, si chema kitakutupa,
Hutaipata ijara, kuchuma ama kukopa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Hicho jangwa la Sahara, si mnofu ni mfupa,
Hakina njema ishara, humtupa mwenye pupa,
Kibovu kama tambara, hupasuka kama chupa, Kiache
kinachokwepa, mbeleye kina madhara
Kitaleta ufukura, si huko wala si hapa,
Kina mengi mazingira, na mbele kitakuchapa,
Sijitie usogora, ukavimbisha mishipa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Si kazi yenye ujira, mshahara kukulipa,
Ya cheo chenye kinara, na heshima wakikupa,
Mbele haina imara, japo leo wajitapa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Japo kazi ya biashara, kutwa wauza makopa,
Uwe mtu na kipara, Mwananchi ama Yuripa,
Bora uwe na busara, fedha tajaza mapipa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara
Usione kinang'ara, huku chapiga marapa, Ukimbilie
kupora, moyo wako kukuzipa,
Kitakugeuza chura, mbele yake utaapa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Usitupe sarara, nyuma kisogo kuipa,
Ukaenda kwa papara, kiumbe mbele kitanepa,
Kwanza tumia fikira, uchague njema chapa, Kiache
kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Na sisemi masihara, hakika kweli nawapa
Mlio pwani na bara, wa Mufindi na wa lupa
Maneno haya kitara, muarifu na Wachepa,
Kiache kinachokwepa, mbeleye kina madhara

Tamati niliyochora, ya shikeni si kuepa
Kisha muwe na basira, na Mola kumuogopa,
Kinachokwepa si nyara, ufunge ndani ya kwapa, Kiache
kinachokwepa, mbeleye kina madhara

(a) Eleza hii ni bahari gani ya shairi
(b) Eleza dhamira ya mshairi
(c) Fafanua hasara nne zinazoletwa na tamaa - vile ving'aavyo
(d) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumika katika shairi
(e) Andika ubeti wa tano katika lugha ya nathari
(f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi
(i) Kuchuma
(ii) Kisogo kuipa

9. Alipokwenda kwao, mamaye alimwambia, Nipa
fedha au nguo, nataka kwenda tumia!
Nikosapo hivi leo, nipa kisu tajitia !
Huzunguka akilia kwa maana ya uketo

Ndipo mamaye kawaza, pamwe na kuzingatia,
Fedha zako umesoza, na leo zimekwisha,
Kisu sikukukataza, twaa upate jitia!
Mbele zangu n'ondokea! Wende na ukiwa wako!

Ulipogeuka nondo, nguo ukazingilia,
Kakaka kwa vishindo, usisaze hata moya,
Leo wanuka uvundo, wambeja wakukimbia!
Mbele zangu n'ondokea ! Wende na ukiwa wako!
Ukijigeuza nyama, kama Simba ukilia,
Watumwa ukawaegema, ukawla wote pia, Pasi
kuona huruma, kutoa wahurumia,
Mbona hukuzingatia? Wende na ukiwa wako!

Si mimi naliokupa, **ukata** huo, sikia!
Kwamba utakuja hapa, nipate kuondolea,
Naapa thama, naapa, sina la kukutendea!
Mbele zangu n'ondokea! Wende na ukiwa wako!

Tamati, nalikomile, ni hayo nalokwambia, Hapahitaji
kelele na kujirisha mabaya,
Na kwamba yakutukie, sema yapate n'elea!
Zidi radhi kuniwea ! Wende na ukiwa wako!

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka
(b) Ni maudhui gani yanayojitokeza katika shairi hili
(c) Taja na ueleze tabia za mnenewa katika shairi hili
(d) Mshairi ametumia uhuru wa utunzi. Taja sehemu mbili alikotumia uhuru huo
(e) Eleza umbo la shairi hili
(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi :-
(i) Uketo
(ii) Ukata

10 . ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali*** Msituni nikakuta, nyuki wamo mzingani,
Kwa juhudi wanakita, mara nje mara ndani,
Husuda wameikata, hata hawasengenyani,
Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja

Mchwa nao nikaona, wamejenga masikani,
Wafanya bidii sana, uvivu hawatamani,
Wao husaidiana, tena hawadanganyani,
Mchwa wadudu wa chini, wanaishi kwa umoja

Nalo jeshi la siafu, hutandawaa njiani,
Laenda bila ya hofu, maana ajiamini,
Silaha zao dhaifu, meno, tena hawaoni Wa kuwatadia nini ? Kwani wanao umoja.

Nao chungu wachukuzi, nyama warima njiani,
Masikini wapagazi, mizigo yao kichwani,
Ingawa si wachokozi, wakali ukiwahini,
Katu hawafarakani, wanadamu kwa umoja.

Sisi ni wana Adamu, mbona hatusikizani,
Tusitietie hamu, ukubwa kuutamani,
Wachache wataalamu, tuwasadi kwa imani,
Hii "Huyu awezani," yatuvunjia umoja

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka.
(b) Ni sifa zipi nne zinazopewa wanaozungumza.
(c) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia uhuru wake katika shairi hili.
(d) Eleza muundo wa shairi hili.
(e) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari.
(f) Taja mafunzo mawili unayopata kutokana na wahusika wanaozungumziwa.
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hilo.
(i) Chungu
(ii) Tuwasadi

11. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Twamshukuru Mwenyezi. Kamwe wingi ukarimu
Alo na kiti cha enzi, Mola wetu akramu Kutupa
kitu azizi , lugha kutakalamu
Lugha ni kitu kitamu, ujuwapo kutumia

Lugha mkuu mlezi , aleaye binadamu
Hata wanyama ja mbuzi, wema lugha wafahamu
Hafuguwa simulizi, izaayo tabasamu
Lugha huwa ni imamu, ujuwapo kutumia

(3) Lugha hodari mkwezi, akweaye tata ngumu
Huzifyeka pingamizi, zizushazo uhasama
Ikazidisha mapenzi, wapendanao kudumu
Lugha huyeyusha sumu, ujuwapo kutumia

(4) Lugha ndiye mpagazi, mazito kuyahudumu
Pia hupanga vizazi, pasi mbari kudhulumu
Aidha hufanya kazi, ikawa mustakumu
Lugha kwayo ni timamu, ujuwapo kutumia

(5) Lugha ni mpelelezi, maovu kuwakasimu Huwatowa palo wazi,
kashuhudia kaumu
Yasifiwa na wajuzi, kuwa ni kitu adhimu
Lugha mkuu hakimu, ujuwapo kutumia

(6) Lugha huizuwa kazi, kutatiza mahakimu Huwaacha kanwa
wazi, wakili kitakalamu
Muhalifu na jambazi, wakaishinda hukumu
Urongo huwa timamu, ujuwapo kutumia

(7) Lugha iwe ni kiongozi, Kizungu au Kiamu Iwekapo waziwazi,
silabi na tarakimu Huyakimu maongezi,yakasikizwa kwa hamu
Lugha huwa ni muhimu, ujuwapo kutumia.

(8) Lugha ni mapinduzi, wanyonge na wajukumu
Kadhalika ni jahazi, ya nahodha muhitimu
Kufa maji haiwezi, si vina si miizamu
Lugha maji zam-zamu, ujuwapo kutumia

**Maswali.**

(a) Eleza maudhui ya shairi hili

(b) Eleza muundo wa shairi hili

(c) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nadhari/ nadharia
(d) Taja huku ukitoa mifano, mbinu tatu za lugha alizotumia mshairi kuwasilisha ujumbe
(e) Eleza maana ya msamiati kama ulivyotumika
(i) Azizi (ii)
Uhasimu
(iii) Adimu.

12. ***Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali :-*** **SHAIRI A:**

Tunda la elimu zote, wasema wanazuoni,
Ni kwamba mtu apate, kumtambua manani. Ndipo
hadhi aipate, akumbukwe duniani.

Elimu bila ukweli, haizidi asilani Giza na
nuru muhali, katu havitengamani,
Uwongo uje kwa ukweli, itue nuru moyoni.

Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani, Ni
bora yashinda mali, taji la wanazuoni,
Elimu njema miali, iangazayo gizani.

Mtu hachomwi na mwiba, na viatu mguuni,
Ulimwengu una miiba, tele tele majiani,
Elimu ukiishiba, U salama duniani.

Wafu ni wasiosoma, watazikwa ardhini,
Hai ndio waulama, wapaao maangani,
Elimu jambo adhima, aso nayo maskini

Elimu ina malipo, utayalipwa mwishoni Pale
uitafutapo, ujira usitamani
Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.

Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni, Wao
wameongolewa, na ni taa duniani.
Kweli wanapojua, watoe bila kuhini.

Elimu bila amali, mti usio majani,
Haumtii kivuli, aukaliaye chini,
Inakuwa mushkeli, wa kushuri insani,

**SHAIRI B**

Inakera moyo
Hii anga ambayo
Huwasonya njiani

Watokao mashambani
Wa kusalimu kwa bashasha Wanaoshinda
kivulini.

Chini ya mwembe Wa
umma.

Inakera moyo
Hii sebule ambayo
Huwahini mezani
Wagotao nyundo kutwa
Wa kukabili chakula
Wanastarehe daima

Chini ya paa
La umma.

**Maswali**

(a) Pendekeza kichwa kifaacho kwa kila shairi la A na B

(b) Haya mashairi ni ya aina gani?

(c) Taja sifa zozote **tatu** za kishairi katika shairi B

(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa :-

(i) Katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa saba katika shairi la A

(ii) Katika ubeti wa nne wa shairi la B

(e) Fafanua kwa mukhtasari maudhui ya mashairi yote mawili

(f) Andika ubeti wa mwisho wa shairi la A katika lugha nathari

(g) Taja na uonyeshe jinsi idhini ya ushairi ilivyotumika katika shairi la A

(h) Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi:-

(i) Maulama
(ii) Wameongolewa
(iii) Wagotao
(iv) Huwahini

13. ***Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo:-***

**CHEMA HAKIDUMU**

Chema hakidumu, kingapendekeza,
Saa **ikitimu**, kitakuteleza, Ukawa
na hamu, kukingojeleza,
Huwa ni vigumu, kamwe hutaweza.

Chema sikiimbi, kwamba nakitweza,
Japo mara tumbi, kinshaniliza,

Na japo siombi, kipate n'ongeza, Mtu
haniambi, pa kujilimbikiza.

Chema mara ngapi, kinaniondoka,
Mwahanga yu wapi? Hakukaa mwaka,
Kwa muda mfupi, aliwatilika,
Ningefanya lipi, ela kumzika?

Chema wangu babu, kibwana Bashee,
Alojipa tabu, kwamba anilee,
Na yakwe sababu, ni **nitengenee**, Ilahi
wahhabu, mara amtwee.

Chema wangu poni, kipenzi nyanyangu,
Hadi siku hini, Yu moyoni mwangu, Yu
moyoni ndani, hadi kufa kwangu,
**Ningamtamani**, hatarudi kwangu.

**Maswali**

(a) Eleza dhamira ya mwandishi
(b) Fafanua umbo la shairi hili
(c) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari
(d) Taja na kutoa mfano mmoja wa tamathali yoyote ya lugha inayojitokeza katika shairi
(e) Taja mbinu nne za uhuru wa mshairi huku ukitolea kila mbinu mfano
(f) **Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na vile yalivyotumika**:-
(i) Nitengenee
(ii) Ningamtamani
(iii) Ikitimu

14.. ***Soma shairi na kisha uyajibu maswali yafuatayo:-***

1. Ni sumu, sumu hatari
Unahatarisha watoto
Kwa ndoto zako zako leweshi
Za kupanda ngazi
Ndoto motomoto ambazo
Zimejenga ukuta
Baina ya watoto
Na maneno laini
Ya ulimi wa wazazi

2. Ni sumu, sumu hasiri
Unahasiri watoto
Kwa pupa yako hangaishi
Ya kuwa tajiri mtajika
Pupa pumbazi ambayo
Imezaa jangwa bahili
Badala ya chemichemi
Ya mazungumzo na maadili
Baina ya watoto na mzazi

3. Ni sumu, sumu legezi
Unalegeza watoto
Kwa mazoea yako tenganishi Ya
daima kunywa 'moja baridi'
Mazoea mabaya ambayo yanafunga katika klabu
Hadi saa nane usiku
Huku yakijenga kutofahamiana
Baina ya watoto na mzazi

4. Ni sumu, sumu jeruhi Unajeruhi watoto kwa pesa,
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi
Na kisha kwenye madawa ya giza baridi
Barabara inayofikisha kwenye giza baridi la kaburi la asubuhi

**<u>Maswali</u>**

(a) Pendekeza kichwa kwa shairi hili
(b) Fafanua maudhui ya shairi hili
(c) Ni kwa njia gani kinachozungumziwa kinajenga ukuta?
(d) Dondoa tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi na uzitolee mfano
(e) Eleza umbo la shairi hili
(f) Uandike ubeti wa nne kwa lugha nathari
(g) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi ;
  (i) Giza baridi
  (ii) Yanakufunga katika klabu

# Fasihi Simulizi

***1. Soma kisha ujibu maswali***

Lala mtoto lala x2
Mama atakuja lala
Alienda sokoni lala
Aje na ndizi lala
Ndizi ya mtoto lala
Na maziwa ya mtoto lala
Andazi lako akirudi
Pia nyama ya kifupa
Kifupa, kwangu, wewe kinofu
Kipenzi mwana lala x2

Titi laja x2

Basi kipenzi lala
Baba atakuja lala
Aje na mkate lala
Mkate wa mtoto lala
Tanona ja ndovu lala

**Maswali**

(a) Huku ukithibitisha jibu lako eleza huu ni wimbo wa aina gani?
(b) Eleza sifa za wimbo wa aina hii
(c) Onyesha umuhimu wa wimbo huu
(d) Eleza amali kuhusu jamii zinazojitokeza katika wimbo huu
(e) Tambua mbinu zozote **mbili** za utunzi zilizotumika katika wimbo huu
(f) Taja vitendo **viwili** vinavyoambatana na uimbaji wa aina hii ya wimbo
(g) Wimbo huu una wahusika wangapi? Wataje

2. ***Soma hadithi hii halafu ujibu maswali ulivyoulizwa***

Hapo zamani za kale, Mungu alituma wajumbe wawili waende duniani. Wajumbe hawa ni Kinyonga na Mjusi. Kwanza alimtuma Kinyonga na kumwagiza akaseme “wanadamu hamtakufa.” Kinyonga alienda kwa mwendo wa kuduwaa, akasimama hapa na pale akila matunda ya miti. Kwa sababu ya hali hii alichelewa sana kufikisha ujumbe kwa binadamu.

Baada ya muda kupita, Mungu alimtuma Mjusi na ujumbe akaseme, “Mwanadamu sharti kufa.” Mjusi aliunyanyua mkia akafyatuka pu! Mbio akawahi duniani kabla ya kinyonga kuwasili. Kwa haraka alitangaza agizo kuu, “Wanadamu sharti kufa!” Akarejelea haraka kwa Mungu. Baada ya muda kinyonga naye akafika duniana na kutangaza, “Wanadamu hamtakufa!” Wanadamu wakapinga mara na kusema, “La! Tumeshapata ujumbe wa Mjusi, wanadamu sharti kufa! Hatuwezi kupokea tena neno lako! Basi kulingana na neno la mjusi, wanadamu hufa.

**Maswali**

(a) (i) Hadithi hii huitwaje?
(ii) Toa sababu zako
(b) Eleza **sifa tatu** zinazohusishwa na ngano za fasihi simulizi katika hadithi hii
(c) Kinyonga ni mhusika wa aina gani?
(d) Hadithi hii ina umuhimu gani?
(e) Taja njia zozote **nne** za kukusanya kazi za fasihi simulizi
(f) **Tambulisha vipera hivi**:-
(i) Kula hepi

(ii) Sema yako ni ya kuazima
(iii) Baba wa Taifa

3. (a) Fafanua sifa **tatu** za ushairi simulizi
   (b) Wawe na kimai ni nini katika fasihi simulizi? Eleza faida zake
   (c) Ainisha mambo yanayobainisha muundo wa nyimbo
   (d) Jadili muundo wa kitendawili
   (e) Bainisha tamathali za usemi zilizotumika katika methali zifuatazo:-
      (i) Ujana ni moshi ukienda haurudi
      (ii) Usipoziba ufaa utajenga ukuta
   (f) Jadili kwa kina matatizo ambayo huenda yakakabili fasihi simulizi katika jamii ya kesho kisha utoe mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na hali hii

**4.** ***Soma wimbo/shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata***

**MUITALIA ANAZWE**

Saa kumi alfajiri
Sote tuliamshwa
Safari tuliianza
Lazima tuimalize
Maji ukiyavulia nguo
Lazima uyaoge

Wazee kwa vijana waliimba
Muitalia lazima anazwe
Mashamba yao walilia
Uui! Jikaze wavulana
Hawataki rangi hii

Wengi wanauliza
Mwitalia alikuja lini? Na ataondoka lini?
Mnaze huyu mlowezi
Hatuchoki
Hatuchoki
Lazima yeye anazwe

Vifaranga na mbuzi
Mbavu zao zahesabika
Meee! Sauti zilihinikiza kote
Haya yote hakika, ni madhila ya Muitalia
Nguvu kweli tunayo
Simama mbele tunayo
Simama mbele uone !
Muitalia ondoka !
Au nikuondoe kwa nguvu

**Maswali**

(a) Taja madhila yaliyosababishwa na Muitalia katika makala haya.
(b) Thibitisha kuwa utungo huu ni wimbo.
(c) Eleza maana inayojitokeza katika mistari ifuatayo:-
   (i) Mbavu zao zahesabika.
   (ii) Haya yote hakika, ni madhilia ya Muitalia.
(d) Huu ni wimbo wa aina gain? Eleza ukitoa ushahidi
(e) Eleza kwa sentensi mbili au tatu shughuli muhimu za kiuchumi za watu wanaimba wimbo huu

(f) Taja mbinu za lugha zilizotumiwa katika wimbo huu. Toa ushahidi
(g) Taja mafunzo mawili yanayotokana na wimbo huu

5. (a) Eleza maana ya miviga kisha uonyeshe inakotumika
(b) Eleza sifa za miviga
(c) Onyesha umuhimu wa miviga

6. Ni nini maana ya wimbo ?
Ni nini maana ya nyimbo zifuatazo.
Tenzi
Kongozi
Sifo
Wawe
Tendi
(a) Eleza umuhimu wa nyimbo
(b) Eleza sifa za wimbo wa aina ya Bembelezi

7. (a) Nini maana ya khurafa/kharafa?
(b) Fafanua sifa **tano** za kharafa
(c) Elezea mbinu **nne** za kutongolea hadithi

8. (a) (i) Ngomezi ni nini katika fasihi simulizi?
(ii) Eleza sifa zozote mbili za ngomezi
(b) Onyesha tofauti kati ya vikundi hivi:
(i) **Hekaya**
**Hurafa**
(ii) **Visakale**
**Visasili**
(iii) **Ngano za mtanziko**
**Ngano za mazimwi**
(c) (i) Vitendawili ni nini?
(ii) Fafanua kwa mifano, mbinu zozote nne za lugha zinazopatikana katika vitendawili
(d) Soma kifungu hiki cha wimbo kisha ujibu maswali yafuatayo :

**Kuumeni** : (Waliimba) Tumeupata mpilipili na maua yake. Chikicha x2
**Kukeni** : (Wimbo wao kwa sauti tofauti)
Tausi waendaa x2
Tausi waenda wamuacha mama kwenye banda
**Kuumeni** : (Wakijibu wimbo) Mwacheni aendee x2
Mwacheni aende akaone mambo ya nyumba
**Kukeni** : Mama ataota nini x2
Ataota nini, hana mtu wa kumletea kuni
**Kuumeni** : Ataota moto wa magunzi, wa magunzi, wa magunzi.
Twamchukua , kisura wetu, kisura wetu, kisura wetu.
Tausi ni wetu, sasa, ni kito chema, ni kito chema ni kito chema.

**Maswali**
(i) Wimbo huu ni wa aina gani na unastahili katika hafla gani ?
(ii) Fafanua ujumbe uliojikita katika utungo huu

9. ***Soma kifungu kifuatacho kisah ujibu maswali yafuatayo :***

(vigelegele vya harusi vililia alilili ; x3)
**Kuumeni** : (waliimba) Tumeupata mpilipili na maua yake chikicha x2
**Kukeni** : (wimbo wao kwa sauti tofauti) Tausi waendaa x2
Tausi waenda wamuacha mama kwenye banda.

**Kuumeni** : (wakijibu wimbo) Mwacheni aendee x2
Mwacheni aende akaone mambo ya nyumba.
**Kukeni** : Mama ataota nini x2.
Ataota nini, hana mtu wa kumletea kuni.
**Kuumeni** : Ataota moto wa magunzi, wa magunzi wa magunzi. Twamchukua, kisura wetu, kisura wetu, kisura wetu.
Tausi ni wetu sasa, ni kito chema, ni kito chema ni kito chema.

(a) (i) Wimbo huu ni wa aina gani, na unastahili katika hafla gani ?
(ii) Bainisha wahusika Kuumeni na Kukeni
(iii) Fafanua ujumbe uliojikita katika utungo huu
(iv) Wimgo huu una umuhim;u gain hafia ulioimbiwa?
(v) Tambua mtindo uliotumika katika utungo huu
(b) Taja na ujadili aina nyingine **sita** za nyimbo

10. a) **Taja sifa za tanzu zifuatazo za fasihi simulizi**
i) Hurafa
ii) Mighairi
iii) Miviga
b) Eleza umuhimu wa ngomezi katika jamii
c) Eleza umuhimu wa mafumbo
d) Eleza tofauti kati ya malumbano ya utani na mawaidha

11. (a) Huku ukizingatia sifa za kimuundo za methali, jadili matumizi ya tamathali za usemi sifuatazo:-
(i) Istiari/sitiari
(ii) Tashihisi
(iii) tashbihi
(b) Vitanza ndimi vina dhima gani katika jamii?
(c) Taja majukumu matatu ya nyimbo katika fasihi simulizi
(d) Eleza sifa tatu za ngano za mtanziko
(f) Eleza sifa tatu za Nyiso
(e) Fasihi simulizi ina sifa ya kuhifadhiwa akilini. Eleza udhaifu wa uhifadhi wa akilini (al. 4)

12. (i) Eleza maana ya vitanza ndimi.
(ii) Taja na ufafanue umuhimu wa vitanza ndimi katika jamii .

# MASWALI YA NGUU ZA JADI

## a). UFAAFU WA ANWANI NGUU ZA JADI

1.Anwani ya riwaya ya nguu za jadi ni ya kijazanda .Thibitisha kwa kurejelea riwaya nzima ala 20

## b).Maswali ya mandhari katika riwaya ya Nguu za Jadi

2.Eleza umuhimu wa mandari ya ofisi ya chifu mshabaha (al.20)

3. Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisa (al 20)

4. Eleza umuhimu manhari ya mahakamani

5. eleza umuhimu wa mandhari ya nyumbani kwambungulu(al.10)

6. Eleza umuhimu wa mandhari ya mkahawa wa Saturn

7. Eleza umuhimu wa mandhari ya read Bead lodines ( al. 10)

8. Eleza umuhimu wa mandhari ya majaani (al. 10)

9. Eleza umuhimu wa mandhari wa uga wa taifa ( al.20)

10. eleza umuhimu wa mandhari ya nyumbani kwa mrima(al.20)

11. eleza umuhimu wa mandhari ya hospitalini (al. 12)

12. eleza umuhimu wa mandhari ya ponda mali(al.10)

13. eleza umuhimu wa mandhari ya kanisa la mtukufu marko(al.20)

14. Eleza umuhimu wa mandhari ya nyumbani kwa mungwasha ( al.20)

## C ).MASWALI KUHUSU MAUDUI KATIKA RIWAYA YA NGUU ZA JADI

15 .Jadili jinsi mwandishi wa riwaya ya nguu za jadi ameangazia dhana ya matumaini ( al 20)

16. fafanua maudhui ya ajira ya kazi yanavyojitokeza riyawani

17. Suala la ajira na kazi linakumbwa na Changamoto katika jamii. Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi(al.10)

18..Fafanua namna utengano umejidhihirisha katika riwaya ya Nguu za jadi.(al.20)

19. Eleza namna haki za wahusika mbalimbali zimekiukwa katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

20. “Binadamu ni viumbe katili" Thibitisha ukweli wa madai haya kwa kurejelca riwaya va Nguu za Jadi.(al.20)

21..Fafanua jinsi wahusika mbalimbali wamedhihirisha mapenzi katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

22 ..Eleza jinsi mwandishi wa riwaya ya nguu za jadi ameangazia asasi ya ndoa.(al.20)

23."Asasi ya ndoa imekumbwa na Changamoto tele".Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.12)

24.Fafanua nafasi ya dini inavyojitokeza katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.10)

25. “Mwanamke ana nafasi kubwa kiujenga jamii yake". Jadili kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

26. Kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi, onyesha jinsi mwanamke amechangia kuilemaza jamii yake.(al.20)

27..Fafanua jinsi wahusika mbalimbali wamekengeuka katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

28. “Jamii imempa mwanamme nafasi bora kulikomwanamke Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya nguu za jadi.(al20)

29.Fafanua madhara/athari za ulevi katika jamii kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

30. Fafanua nafasi ya wazazi katikajamii kwamujibu wa riwaya ya Na za Jadi.(al.20)

31. Fafanua namna umaskini umejitokeza katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

32. Fafanua madhara ya umaskini yanavyojitokeza katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

33.Fafanua namna mwandishi wa riwaya yaNguu za Jadi amaeangazia suala la elimu.9al.20)

34..Elimu imekumbwa na changamoto tele.Jadili kwa kutolea mifane kutoka riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

35. Fafanua namna wahusika mbalimbali wamewajibika kwa kurejelea iwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

36.“Mataifa mengi Barani Afrika yanakumbwa na tatizo la uongozi mbaya”.Jadili kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

37.Fafanua madhara ya uongozi mbaya kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

38.Mwandishi wa riwaya ya Nguu za Jadi anadhamiria kujenga jamii mpya. Thibitisha.(al.20)

39. binadamu ni viumbe salitiThibitisha kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

40. “Maisha ni mabadiliko" Tetea kauli hii kwa kurejeleariwayaya Nguu za Jadi.(al.20)

41. “Chuki na uhasama ni mwiba unaokwaza maendeleo katika jamii".

42. Eleza namna siasa imeangaziwa katika riwaya ya Nguu za jadi.(al.20)

Wanasiasa wanatafuta wafuasi wa kuwaunga mkono. Mwamba alitafuta wake na Sagilu pia.

43.“Vita vya kikabila vina madhara mengi katika jamii”. Fafanua kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

44.Fafanua namna maudhui ya malezi yameangaziwa kayika riwava ya Nguu za Jadi.(al.20)

45.Eleza changamoto zinazokumba malezi kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

46. tamaa mbele mauti nyuma. Thibitisha ukweli wa methali hii kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

47.. “Binadamu ni utu” Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

48.“Ufisadi ni kikwazo cha maendeleo katika jamii. Fafanua kulingana na riwaya va Nguu za Jadi.(al.20)

.49.Fafanua dhana zifuatazo zinavyojitokeza katika riwaya ya Nguu za jadi .

(i)Ubaguzi. (al.8)

(ii)Mapendeleo.(al.4)

50. "Binadamu ni viumbe wasiojali". Eleza ukirejelea riwaya ya Nguu a Jadi.(al.20)

51.Fafanua maudhui ya utamaduni yanavyojitokeza katika riwaya ya guu za jadi.(al.20)

52.“Utamaduni mkongwe ni kikwazo katika maendeleo ya mwanamke katika jamii" Jadili kwa kutolea mifano kutoka riwaya va Nguu z Jadi.(al.10)

53.Wahusika mbalimbali wamesheheni vitisho katika riwaya va Nguu za Jadi. Jadili.(al.20)

54.Fafanua jinsi wahusika wamesheheni usherati/uzinzi/ufuska katika iwaya va Nguu za Jadi.(al.20)

55. "Unasaba umechochea jmii kutopiga hatua kimaendeleo". Jadili kurejelea riwaya ya Nguu za

56.Fafanua mogogoro inayojitokeza katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.12)

57.Fafanua utamaduni wa kisasa unavyojitokeza katika riwaya ya Nguu za jadi(al.20)

58.Eleza uozo uliopo katika jamii kwa kurejelea riwava ya Nguu za Jadi.(al.20)

59. Fafanua jinsi wahusika wanadhihirisha unafiki katika riwaya ya Nguu za jadi.(al.20)

60.“Binadamu wanaendeshwa na ubinafsi katika jamii ya kisasa".Thibitisha kwa kurejelca riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

61..“Haki za Watoto kama vizazi vya kesho zimekiukwa" Thibitisha kwa rejelea riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

62. Mwandishi wa riwaya ya Nguu za jadi amemuumbua mwanamume Fafanua.(al.20) Jadili nafasi hasi ya wahusika wa kiume katika riwaya. Wanaume ni:

63. Mwandishi wa riwaya ya Nguu za Jadi amewachora wanaumme kama wakombozi wa jamii. Fafanua.(al.20)

Rejelea nafasi Chanya ya wahusika wa kiume riwayani

64.. Fafanua mbinu -ishi amabazo wahusika katika riwaya ya Nguu za jadi. Wametumia kukabiliana na madhula yanayowakumba (al.20)

## d) MASWALI KUHUSU MBINU ZA UANDISHI KWA RIWAYA NGUU ZA JADI

65. Fafanua matumizi za barua katika riwaya ya Nguu za Jadi(al.20)Barua va mpenzi wa Mrima.

(a)Usaliti-Sagilu anamsaliti Mangwasha kimapenzi kwa kuwa na uhasian

(b) Barua ya Mtemi Lesulia kwa Afisa Mkuu wa ardhi.

(c)Barua ya Msajili wa ardhi kwa Chifu Mshabaha.

(d) Barua ya Sagilu na Sihaba kwa Mbaji.(Uk.98)

(e) Barua ya Sagilu kwa Mrima. (Uk.10)

66. Fafanua umuhimu wa hotuba ya Lonare kwa wananchi.(al.20)

67. Jadili namna matukio mbalimbali yamesadifu katika riwaya ya

Nguu za Jadi.(al.20)

68..Fafanua matumizi ya jazanda katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)..

69.Fafanua matumizi ya ishara/taashira katika riwaya ya Nguu za jadi.(al.20)

70..Mwandishi wa riwaya ya Nguu za Jadi amefanikiwa kutumia ethali katika kazi yake. Eleza kwa kutolea mifano.(al.20)

71. Fafanua matumizi ya kinaya katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

72. Fafanua matumizi ya hadithi ndani ya hadithi katika kukuza vipengele vifuatavyo: (i)Maudhui

(ii)Wahusika    Rejelea:

Kisa cha Lilith (uk.81-82)

(i)  Jinsi kinakuza maudhui (al.10)

(ii) Jinsi kinakuza wahusika(al.10)

73. Kisa cha kijana mmoja ambaye aliugua ugonjwa wa Pediculosis orporis(uk.131-132)

i) Jinsi kinakuza maudhui(al.10)

(ii) Jinsi kinakuza wahusika(al.10) i)Jinsi kinakuza maudhui(al.10)

(ii)  Jinsi kinakuza wahusika(al.10)

74.. Eleza jinsi mwandishi wa riwaya va Nguu za Jadi ametumia mbity rejeshi katika kazi yake.(al.10)

75.Fafanua matumizi ya davoloiia katika riwava va Nguu za Jadi.(al.20) (i).Dayolojia kati ya Mangwasha na mumewe  mrima .

(ii).Dayalojia kati ya Mangwasha na rafiki yake,Mbungulu.

(iii) Dayolojia kati ya Mangwasha,Sagilu na Chifu Mshabaha.

(iv)Dayalojia zinazomhusisha Lonare vi) Dayalojia zinazomhusisha Mtemi Lesulia,(uk.78) Vi)Dayolojia kati ya  mashauri na Ngoswe .

Vii) Dayolojia kati ya mtemi lesulia na mwanawe ngoswe (uk.129)

(viii) Dayalojia katiya Lombo na Mashauri.

76.. Fafanua matumizi ya uzungumzinafsi katika riwaya ya Nguu za Jadi.(al.20)

77..Fafanua matumizi ya taharuki katika riwaya ya Nguu za Jadi,(al.20)

78..Eleza matumizi ya chuku katika riwaya ya nguu za jadi (al.12)

## e) MASWALI KUHUSU WAHUSIKA; KATIKA RIWAYA NGUU ZA JADI

Katika sehemu hii nimeangazia:

Jinsi mhusika wanajenga maudhui mahususu riwayani.

Jinsi mhusika wanajenga maudhui kwa jumla riwayani.

SifaChanya za mhusika

Sifa hasi za mhusika

Jinsi mhusika amejenga ploti

Jinsi mhusika amejenga wahusika wengine

Jinsi mhusika amechangia kuijenga jamii yake.

Jinsi mhusika amechangia kuibomoa jamii yake

MANGWASHA

Ni mwanawe Mzee Shauri na Bi. Tesi.

Ni mhazili wa Chifu Mshabaha.

Ni mkewe Mrima na mamake Sayore na Kajewa.

Ni mshiriki wa karibu wa Lonare kisiasa na rafiki wa Mbungulu.

## 79..Eleza jinsi Mangwasha anajenga maudhui ya uvumilivu (al.5)

80..Eleza jinsi Mangwasha anajenga maudhui ya matumaini

81.. Eleza jinsi Mangwasha amedhihirisha ujasiri

82.Eleza jinsi Mangwasha amejenga .maudhui ya uwajibikaji katika riwaya ya nguu za jadi .(al.20)

83. Eleza jinsi mangwasha amejenga maudhui ya ukengeushi .(al.20)

84.Eleza jinsi Mangwasha anajenga maudhui ya dini.(al.20)

85..Elezajinsi Mangwasha amejenga maudhui ya mapenzi.(al.10)

86. kurejelea riwaya nzima,thibitishakuwa Mangwasha ni wenye bidii(al.10)

87. Mangwasha ni kielelezo bora cha wanawake katika jamii.

Fafamua.(al.20) Mangwasha

ni:

88. Eleza nafasi ya Mangwasha katika kujenga maudhui katika riwaya ya uu za Jadi.(al.20)

89. Eleza mchango wa Lonare katika kutetea haki katikajamii

90. Eleza mchango wa Lonare katika ukombozi wa jamii yake.

91.Dhihirisha kuwa Lonare ni mzalendo.(al.6)

92. Lonare ni mshauri mwema.Thibitisha.(al.8)

93.Fafanua jinsi Lonare amejenga maudhui katika riwaya:Lonare amejenga maudhui ya:

.94.Lonare ni kielelezo cha kuigwa katika jamii. Jadili.(ala.10) ni:

95.Eleza jinsi Mrima amejenga maudhui ya usaliti.(al.10)

i.Mapuuza

(ii)Ufisadi

96.. Eleza jinsi Mrima amejenga maudhui riwayani.(al.20)

**PIA TUNA;**

- **MIONGOZO YA**: MAPAMBAZUKO,BEMBEA NA NGUU ZA JADI
- **MASWLI NA MAJIBU YA**:
- MASWALI NA MAJIBU YA MAPAMPAZUKO YA MACHWEO
- MASWALI NA MAJIBU YA BEMBEA YA MAISHA

# MWISHO WA MASWALI JIBU NGUU ZA JADI 2024

# MASWALI YA MAPAMBAZUKO YA MWACHWEO NA HADITHI NYINGINE

1. Fafanua changamato wanazokumbana nazo waajiriwa katika hadithi Harubu ya Maisha (alama 20)
2. Jadili matumizi ya pombe haramu na athari zake katika hadithi kila mchezea wembe (alama 20)
3. Fafanua wa ufaafu wa anwani Fadhila za Punda (alama 20)
4. Fafanua dhiki zinazowakumba raia katika hadithi ya Msiba za Kujitakia (alama 20)
5. Jadili ufaafu wa anwani Mapambazuko ya Machweo alama 20
6. Urumo umekita mzizi katika jumuiya ya Mapambazuko ya Machweo. Jadili alama 20
7. Miti katika misitu ilizidi kuangamizwa kwa makali ya shoka lakini miti ilizidi kulifurahia shoka...miti ikafikiri shoka ni mmoja wao!"
    a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
    b) Bainisha mbinu zozote mbili katika mkutadha huu. (alama 4)
    c) Eleza sifa mbili za shoka. (alama 2)
    d) Kwa kurejelea hadithi ya msiba wa kujitakia, jadili mbinu zinazotumiwa na viongozi kuingia mamlakani. (alama 10)
8. "tafadhali nisamehe...ni barua ilinikawiza..."
    a) Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)
    b) Tambua kipengele kimoja cha kifani kilichotumiwa katika dondoo hili.

       (alama 2)
    c) Eleza barua hii na matokeo yake. Alama 6)
    d) Jadili dhima ya msemaji katika kuendeleza maudhui ya hadithi. (alama 8)

9.a) Kwa kuzingatia hadithi ya harubu ya maisha, jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa. (alama 5)

b) Kwa kuzingatia hadithi ya harubu ya maisha, fafanua matatizo yanayowakumba wafanyikazi. (alama 10)

c) Jadili dhana ya utatu inavyojitokeza katika diwani ya mapambazuko ya machweo na hadithi nyingine. (alama 5)

10. ..iwapo penzi hili litatia doa, basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya kulitupa penzi langu kama jongoo na mti wake..."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. (alama 4)
c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)
d) Eleza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti. (alama 6)

11. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo, jadili maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii.

(alama 20)

i. Toba ya kalia
ii. Ahadi ni deni
iii. Nilitamani
iv. Pupa

12. Wanaume katika mataifa mengi barani afrika wametawaliwa na ubabedume. Jadili kauli hii ukirejelea hadithi ya "Fadhila za Punda" (al.20)

13. Huku ukitolea mifano mwafaka ,eleza jinsi ambavyo haki za watoto/vijana zimekiukwa katika hadithi ya Mapambazuko ya Machweo

14. Mwandishi katika hadithi ya Msiba wa Kujitakia alifaulu kutumia mbinu ya uwili. Thibitisha. (al. 20)

15. Mwandishi wa hadithi ya "mapambazuko ya machweo" uwajibikaji kwa kiasi kikubwa mno. Illihirisha ukweli na kauli hii (al.20)

16. Wafanyikazi katika nchi nyingi zinazoendelea wanakumbwa na

19.“mwanangu, nizike duniani unifunike…”

a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (al.4)

b) Taja na utolee mfano mbinu moja ya kimtindo inayojitokeza katika dondoo hili

(al.2)

c) Ukirejelea hadithi ya" Mzimu wa Kipwerere," fafanua jinsi imani katika mambo ya kichawi yamejikita katika jamii. (al. 14)

20.Fafanua jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika hadithi ya Nipe Nafasi (alama 20)

21."thank you. U mteja wa pekee, unajua kuthamini huduma nzuri unapopewa."

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (al.4)

b) Taja na ueleze mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. (al.4)

c) Kwa kurejelea hadithi ya "kila mchezea wembe," fafanua changamoto zinazowakumba watumiaji wa vileo kupita kiasi. (al. 12)

22. "...iwapo penzi hili litatia doa, basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya kulitupa penzi langu kama ongoo na mti wake...

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. (alama 4)

c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)

d) Eleza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti. (alam 6)

23.Kwa kurejelea hadithi ya Ahadi ni Deni, fafanua namna uwajibikaji umejitokeza. (alama 20)

24."kwa kweli, nimeungulika sana miaka yote hii kwa unyama tuliomtendea Jack.. ."

a) eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) jadili umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (alama 6)

c) jadili ukatili aliokuwa ametendewa mhusika jack kulingana na dondoo hili. (alama 5)

d) kwa kurejelea mhusika jack, jadili maudhui ya nafasi ya vijana. (alama 5)

25. Onyesha namna mwandishi wa hadithi ya nipe nafasi alivyodokeza maudhui ya taasubi ya kiume. (alama 20)

26. Ndoa ni taasisi iliyokuzwa katika hadithi fadhila za punda. Fafanua alama 20

27....wajua siku hizi huwezi kuamini yeyote apitaye na hasa akiomba msaada au umekula kututapeli?"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Eleza umuhimu wa msemewa wa maneno haya katika kujenga maudhui kwenye hadithi hii. (alama 10)
c) Eleza sifa za msemaji wa maneneo haya. (alama 5)

28. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo, jadili maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii. (alama 20)

a) Toba ya kalia
b) Ahadi ni deni
c) Nilitamani
d) Pupa

29. Rachel wangari katika hadithi ya Mapambazuko ya Machweo ametumia mbinu ya jazanda kwa upana. Jadili (alama 20)

30. Swala la elimu limepewa kipaumbele katika hadithi ya Sabina. Jadili (alama 20)

31. Fafanua jinsi yusuf shoka hamad katika hadithi mzimu wa kipwerereameshughulikia swala la ushirikina na unafiki alama 20

32. Umaskini ni donda sugu katika hadithi kifo cha suluhu, huku ukitoa hoja ishirini jadili (alama 20)

33. Eleza jinsi ubabedume umejitokeza katika hadithi ya Nipe Nafasi (alama 20)

# MASWALI YA BEMBEA YA MAISHA

1. Anwani bembea ya Maisha inaafiki tamthiliya hii. Jadili kwa kutoa hoja ishirini (alama 20)

2. Kwa kurejelea tamthilia hii eleza namna mila na desturi zinavyoweza kuzua migogoro katika jamii.

(alama 20)

3. A. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali.

"La! Kila mbegu ipandwayo haina budi kuzaa na izaapo mazao yake huvunwa. Mtu huitakasa sahani

akijua itamfaa tena. Kinacholelewa hakina budi kulea."

a) Fafanua muktadha wa mancno haya. (alama 4)

b) Taja mbinu nne zilizotumika hapa. (alama 8)

c) Eleza sifa nne za mnenaji (alama 8)

4. A. Soma dondoo kisha ujibu maswali.

"Kumbuka, mrina haogopi nyuki. Marehemu mamangu alizoea kutuambia kuwa nguvu hazimwishi mwanadamu wala hazipotei bure — humalizwa tu na mabuu. Mwanangu, usifanye hofu. Nikujuavyo

mimi, hukuingia katika bahari si yako. Wala hakuna refu lisilokuwa na ncha. yote yana kikomo ati! Ipo

siku haya yote yatapita. Mkulima hodari libasi yake huwa imechakaa na kuchoka lakini moyoni anabaki

safl kama theluji kwa kutosheka na tija ya sulubu zake. Huwezi kumlinganisha na mkulima wa nguo safi

zilizopigwa pasi zikanyooka."

a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b) Fafanua sifa moja ya mnenaji inayojitokeza katika dondoo hili (alama 2)

c) Fafanua mbinu zilizotumika (alama 8).

d) Onyesha kuwa msemewa hakuingia bahari ambayo si yake (alama 6)

5. Soma dondoo kisha ujibu maswali.

Eti alama! My foot! Eti ameshuka nafasi darasani lakini akapandisha alama...

a) Eleza maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

b) Jadili sifa tano za mnenaji. (alama 10)

c) Tathmini umuhimu wa mnenaji katika tamthilia. (alama 8)

6. Soma dondoo kisha ujibu maswali.

"Ukilazwa tayari unakuwa umeonja seli,: Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema. Amri na

vitisho kama askari. Unashindwa kama UUguze moyo ama ugonjwa. Katika wodi hewa iliyojaa harufu

ya dawa imezagaa, vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura. Yaani hali nzima haikupi matumaini

ya kutoka ukiwa bora. Matumaini yanadidimia. Tumaini lako unaliweka katika sala".

a) Changanua mtindo wa dondoo kwa kurejelea hoja tano. (alama 10)

b) Fafanua namna mandhari ya dondoo hili yalivyochangia usukaji wa tamthilia. (alama 10)

7. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali.

'...wanajikuta katika vuta n'kuvute inayochochewa na mitazamo ya kitamaduni, uhalisia wa mambo

pamoja na matamanio ya wahusika binafsi. Baina yao kuna mitikiso inayotishia familia, ndoa na mahusiano ya kijamii. Kuna shutma, shaka, tuhuma na mivutano. Lakini pia kuna hongera, imani,

ushirikiano, upendo, kutanabahi, na mshikamano. Katika huu mseto wa mambo ipo sauti imara.. ."

a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Hakiki mtindo wa dondoo hili. (alama 2)

c) Fafanua mitikiso saba inayotishia mahusiano ya kijamii ya tamthilia hii. (alama 14)

8. Mwandishi wa Bembea ya Maishaameipa uzito mbinu rejeshi. Eleza. (alama 20)

9. Soma dondoo hili na ujibu maswali.

"Mtu anaishi na wanawe ambao wiki nzima anawaona wakiwa usingizini; wamelala fofofo.. .Nyumba ni ya yaya."

i. Weka maneno haya kwenye muktadha wake. (alama 4)

ii. Fafanua maudhui yanayojitokeza kwenye dondoo. (alama 2)

iii. Fafanua manufaa saba ya mazingira ya dondoo hili. (alama 14)

10. Soma dondoo hili kisha ujibu maswali.

‘Maisha yetu ni mfano wa mbegu iliyopandwa. Mbegu hiyo haina budi kuoza kwanza ndipo ioteshe mche

upendezao. Mche huo wa asili ya mbegu iliyooza, hatimaye hutoa zao la mbegu nyingi ajabu. Ukitazama

vizuri, mbegu ile haifi bali huchukua mkondo mwingine wa maisha. Huchukua umbo)ipya lipendezalo

hasa ikiwa itakuwa imeangukia ardhi nzuri.. -Sasa rudini msaidie kuzalisha mbegu nyingi nzuri. Nyinyi

mmebahatika kuwa mbegu nzuri istahiliyo kupandwa."

Hakiki ukweli wa maneno haya kwa kurejelea Bunju,Neema na wahudumu hospitalini. (alama 20)

11. Bembea ya Maisha ni tamthilia inayohimiza mshikamano wa kijamii. Jadili. (alama 20)

12. Mwanamke anaonyesha maumbo mbalimbali, mazuri na mabaya.

13. Elimu ni mafundisho aali yatolewayo darasani au katika jamii. Jadili kwa kurejelea tamthilia ya Bembea

ya Maisha (alama 20)

14. "Imani na itikadi huthaminiwa sana na jamii ya watu". Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia

ya bembea ya Maisha (alama 20)

15. Mwandishi wa tamthilia hii ameshughulia sana suala la Mabadiliko katika jamii. Fafanua (alama 20)

16. Eleza jinsi mwandishi watamthilia ya Bembea ya maiisha alivyofanikiwa kutumia ishara katika kazi (alama 20)